# Nipashe

Alhamisi Mei 9, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579913

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13



## Gwajima akimbilia TCRA, polisi wamkingia kifua video ya ngono

UKURASA 2




# KILIMANJARO YAZIZIMA

• **Msafara** mwili wa Dk. Mengi watumia saa 6 kutoka KIA-Hai, Waziri Mkuu kuongoza mazishi leo... *Endelea ukurasa wa 2*






Wananchi wa Mji wa Bomang'ombe, wakiwa wametandika khanga barabarani ili gari lenye mwili wa Dk. Reginald Mengi lipite juu yake kama ishara ya heshima kwa marehemu, wakati ukipitishwa kuelekea Machame jana. **Picha ndogo:** Gari maalum likiwa tayari kuubeba mwili baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA). **PICHA ZOTE: GEOFFREY MUSHI**

## Staili mpya ya ubakaji yabainika

UKURASA 3

## 1,200 waugua Dengue Dar, Kinondoni, Ilala tishio

UKURASA 3

**MICHEZO** **OKWI, KAGERE SASA KUMALIZA MIPIRA TFF** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Lowassa: Dk. Mengi aliuchukia umaskini kwa vitendo

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, amesema atamlilia aliyekuwa Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Regnald Mengi, kutokana na kuwa kielelezo cha mtu halisi aliyeuchukia umaskini kwa vitendo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyopatikana jana jijini Dar es Salaam, Lowassa alimwelezea Dk. Mengi kama mtu aliyeishi maisha yake na kuwanyanyua wengine katika kuupinga umaskini.

"Umekuwa na mchango mkubwa sana katika maendeleo ya taifa letu na watu wake. Umeacha alama kubwa ya upendo, moyo wa kutoa na unyenyekevu kwa jamii alama ambayo Watanzania tutakumbuka nayo daima," alisema.

**SHIVYAWATA WAMLILIA**

Nalo Shirikisho la Vyama vya Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA) Mkoa wa Dodoma, limemlilia marehemu Dk. Reginald Mengi, huku likisema alikuwa msaada kwao, hivyo ndoto zao walizokuwa wakitegemea kutoka kwake kuwainua kiuchumi zitakuwa zimefutika.

Katibu wa Shivyawata Mkoa wa Dodoma, Justin Ng'wantalima, alisema ndoto ya watu wenye ulemavu waliyokuwanayo kabla ya kifo cha Dk. Mengi walitegemea kuwa ipo siku wataondokana na umaskini.

Alisema alikuwa sauti kwa walemavu, watoto, yatima na wasio na uwezo na alijitoa bila kujali kuwa anapata kitu gani kwenye maisha yake.

"Dk. Mengi kwa upande wetu sisi watu wenye ulemavu alikuwa mtu ambaye hakuwa mbinafsi na alipenda kuona wenye ulemavu siku moja tunaondokana na umaskini," alisema.

Naye katibu wa Chama cha wasioona mkoa wa Dodoma, Enock Mbawa, alisema Kutokana na umuhimu aliokuwanao kwa watu wenye ulemavu, Dk. Mengi kwa upande wao alikuwa kama Mungu wa pili wa kwao kutokana na mambo aliyowafanyia kwa misingi ya kiroho.

Hata hivyo ni matumaini kwetu watu wenye ulemavu watajitokeza wengine watakaochukua jukumu la kuwajali kama ilivyokuwa kwa Dk. Mengi ambaye aliamua kwa dhati kutoka moyoni kuwajali na kuhakikisha mahitaji yanayowaguza wanayapata.Imeandikwa na Salome Kitomari (Dar) na Peter Mkwavilla (Dodoma)

# Dk. Mengi aiteka Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi, HAI**

SHUGHULI za kiuchumi, kilimo, usafirishaji na huduma nyingine za kijamii katika maeneo mbalimbali ya wilaya ya Hai na barabara kuu ya Arusha/Moshi, jana zilisimama kwa zaidi ya saa tano, kupisha msafara wa magari ya kusindikiza mwili wa Mwenyekiti wa Makampuni ya IPP, Dk. Reginald Mengi.

Mamia ya wananchi wa miji ya Kia, Bomang'ombe, kwa Sadala, Mashine Tools na Nshara wakifunga barabara kwa saa zaidi ya tano.

Wananchi hao ambao wengine walisindikiza gari lililobeba mwili huo huku wakiimba nyimbo, kubusu gari, kutaka mwili ushushe wabebe jeneza, kufagia barabara, kutandika khanga, kubeba mabango, kumwaga maua na kulala barabarani, yote ni kumuenzi Dk.Mengi.

Mwili wa Dk. Mengi uliwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (Kia) saa 3:40 asubuhi kwa ndege ya Shirika la Precision Air na kupokelewa na viongozi mbalimbali akiwamo Mkuu wa mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, wabunge, wakuu wa mikoa, wilaya, wakuu wa taasisi mbalimbali, viongozi wa dini na siasa wa mikoa ya Kanda ya Kaskazini.

Katika mji wa Bomang'ombe, maelfu ya wananchi walisimama katikati ya barabara kuu ya Moshi-Arusha wakiwa wamebeba matawi ya miti, wengine wakigalagala katikati ya barabara na wengine wakiimba nyimbo za majonzi.

Mamia ya waombolezaji waliusindikiza mwili wa Dk. Mengi wakikimbia kwa miguu kutoka makutano ya kwenda uwanja wa ndege wa Kia-Arusha/Moshi hadi eneo la darajani nje kidogo ya mji wa Bomang'ombe ambapo vikosi vya Jeshi la Polisi vililazimika kuwasogeza waombolezaji kupisha msafara huo.

Shule mbalimbali hasa sekondari na shule za msingi, maduka ya biashara, baa na hoteli zilizopo pembezoni mwa barabara kuu ya Moshi-Arusha walifunga kwa muda mfupi na kukusanyika kando ya barabara wakiimba nyimbo za kujifariji.

MAJALIWA, NDUGAI KUONGOZA MAZISHI

Akizungumza na waandishi wa habari katika uwanja wa ndege wa Kia, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Mghwira alisema Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwasili mkoani humo leo asubuhi na ataongoza maelfu ya waombolezaji katika mazishi ya Dk. Mengi atakayezikwa kesho.

Kwa mujibu wa Mghwira, viongozi wengine wa kitaifa watakaoshiriki mazishi hayo ni pamoja na Spika wa Bunge, Job Ndugai.

Waliowasili na mwili huo ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, Mkuu wa mkoa wa Njombe, Christopher Ole Sendeka, Mbunge wa Vunjo, James Mbatia na

INAENDELEA UK. 8

# Gwajima akimbilia TCRA, polisi wamkingia kifua video ya ngono



Mchungaji wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, akitoa ufafanuzi kwa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kuhusishwa kwake na video ya ngono inayosambazwa katika mitandao ya kijamii. Kulia ni mkewe. **PICHA: MIRAJI MSALA**

**Elizabeth Zaya na Mary Geofrey**

ASKOFU wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephath Gwajima, amesema amepeleka maombi kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ili imtafute mtu aliyemchafua kwa kusambaza video ya ngono mtandaoni akidai kuwa ni ya Askofu huyo.

Gwajima aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kukanusha juu ya video hiyo ya ngono inayodaiwa kuwa ni yake na kudai kwamba ni njama za kumchafua.

Askofu Gwajima alisema tayari ameshaanza kufanyia kazi mtu aliye nyuma ya njama hizo za kumchafua na kwamba anaamini kwamba TCRA itafanya kazi yake na kumbaini.

"Nimewaomba TCRA wamtafute na ndiyo nataka kuona kama sheria ya makosa ya mtandao inafanya kazi, kwa sababu kuna watu wanachafuliwa na wanaowachafua wanapatikana, haiwezekani na mimi nichafuliwe halafu wahusika wasipatikane, ninaamini kwamba na huyu aliyenichafua atapatikana," alisema Gwajima.

Askofu Gwajima pia alihusisha tukio hilo na masuala ya kisiasa akiamini kwamba ni mbinu za kumnyamazisha asizungumze kuelekea katika uchaguzi mkuu mwaka kesho.

Alisema zipo njama zinazofanywa na baadhi ya watu ambao wanajaribu kumwanzishia matukio ya kumuumiza ili akose nguvu sauti ya kusema kwa sababu wanaamini kwamba amekuwa akizungumza ukweli.

"Nilichojifunza ni kwamba tangu mwanzo mimi napenda nchi ya Tanzania, mahubiri yangu, misemo, mafundisho na 'character'

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA



Magari yakipita kwa tabu kwenye maji ya mafuriko katika eneo la Jangwani, kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# 1,200 waugua Dengue Dar, Kinondoni, Ilala yatajwa hatari

**Na Waandishi Wetu**

WATU 1,200 wa Mkoa wa Dar es Salaam, wameugua ugonjwa wa homa ya Dengue huku mtu mmoja akiripotiwa kupoteza maisha, huku Wizara ya Afya ikitoa tahadhari.

Maeneo yaliyokumbwa na ugonjwa huo ni Ilala, Kariakoo, Upanga, Kisutu, Buguruni na Tabata wilayani Ilala.

Maeneo mengine ni Ubungo, Mbezi wilayani Ubungo na Msasani, Masaki na Kinondoni wilayani Kinondoni.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Yudas Ndugile, alieleza takwimu hizo wakati akizungumza na Nipashe kuhusu hali ya ugonjwa huo katika jiji hilo, lenye wakazi takribani milioni tano kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012.

Alisema idadi hiyo ya wagonjwa ni kwa mujibu wa taarifa za kuanzia Januari hadi Mei mwaka huu ambazo zimekusanywa katika hospitali mbalimbali ndani ya mkoa huo.

"Kwa kipindi cha Januari hadi Mei mwaka huu, jumla ya wananchi 1,200 wameugua homa ya dengue na mtu mmoja kupoteza maisha katika mkoa mzima wa Dar es Salaam," alisema Dk. Ndugile.

"Na wagonjwa wengi wanatoka katika maeneo na kata za Ilala, Kariakoo, Upanga, Kisutu, Buguruni, Tabata, Mbezi, Ubungo, Kinondoni, Msasani, Masaki," alitaja Dk. Ngugile.

Aidha, Dk. Ngudile alisema katika kudhibiti ugonjwa huo wametoa tahadhari kadhaa zikiwamo za kuangamiza mazalia ya mbu kama vifuu, makopo, vyungu chakavu, matairi chakavu,na kufukia madimbwi kwenye maeneo ya makazi.

Alisema pia wananchi wanatakiwa kuchukua tahadhari na kusafisha maeneo ya ofisi, shule, vyuo, gereji, stendi za mabasi, masoko, maeneo ya mama lishe, baa, sehemu wanazouza vinywaji, hoteli, migahawa na hosteli za wanafunzi.

Dk. Ngudile alisema, wamefanya kazi ya upuliziaji dawa za kuua mbu katika maeneo ya shule, vyuo, gereji, masoko, kwa mama lishe, kwenye baa, grosari, hoteli, migahawa, hosteli za wanafunzi na stendi za mabasi.

Pia aliwataka wanachi kuchukua tahadhari za kupata ugonjwa huo kwa kuzuia kunga'atwa na mbu kwa kutumia chandarua chenye

INAENDELEA UK. 8

## Asasi sasa zalia na mbinu mpya ya ubakaji

**Na Enock Charles**

ASASI sita za Kiraia zimeiomba Serikali kuchukua hatua za haraka kukomesha mbinu mpya ya vitendo vya ubakaji wanavyofanyiwa wanawake wilayani Mwanga mkoani Kigoma ambao umepatiwa jina la 'teleza' wakitumia kujipaka mafuta machafu na kinyesi li wasikamatwe.

Asasi hizo zikiongozwa na taasisi ya utafiti isiyo ya kiserikali (Twaweza), Kituo cha Sheria na haki za binadamu (LHRC), mtandao wa kijamii wa jamii forum na mtandao wa mabadiliko (Change Tanzania) zimeeleza kusikitishwa mtindo huo mpya wa ubakaji na kuiomba Serikali kuchukua hatua za haraka ili kuwanusuru wanawake mkoani humo.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti ya Twaweza Aidan Eyakuze, alisema matukio wanayofanyiwa wanawake hao ni ya kikatili na kwamba serikali inapaswa kuliona hilo na kuchukua hatua za haraka ili kuwanusuru wanawake mkoani humo.

"Haya matukio yaliyoibuka Kigoma yanasikitisha, tunatakiwa kuchukua hatua za haraka ili kuwakomboa hawa wanawake na kufanya jitihada sio tu kwa tukio hili la Teleza ila kuhakikisha kuwa hakuna mahali nchini ambapo wanawake hao wanaonewa " Alisema Eyakuze.

INAENDELEA UK. 8


**MAJEMBE AUCTION MART LTD**
**(VIJANA WA KAZI)**
**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

MAJEMBE AUCTION MART LTD. KWA IDHINI TULIYOPEWA NA HALMASHAURI YA WILAYA YA KARATU S.L.P 190 KARATU, TUTAUZA KWA MNADA WA HADHARA MAGARI NA MASHINE MBALIMBALI TAREHE 25/05/2019 SIKU YA JUMAMOSI KUANZIA SAA TANO ASUBUHI.

| NO. | REG.NO | LOT NO. | MAKE | HALI YAKE |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SM 8108 | KDC/2018/01 | LANDROVER PUMA | HALITEMBEI |
| 2. | SM 6354 | KDC/2018/02 | LANDROVER 110 S/W | HALITEMBEI |
| 3. | T800 QLN | KDC/2018/03 | ISUZU TIPPER TON 7 D / INJECTION | HALITEMBEI |
| 4. | SM 21396 | KDC/2018/05 | ISUZU FSR TIPPER | HALITEMBEI |
| 5. | CW5602 | KDC/2018/05 | COMBINE HARVEST FIAT AGR | LINATEMBEA |
| 6. | SM 3616 | KDC/2018/06 | YAMAHA AG 125 | LINATEMBEA |
| 7. | SM5718 | KDC/2018/07 | YAMAHA DT 125 | LINATEMBEA |
| 8. | UNKNOWN | KDC/2018/08 | YAMAHA AG 125 | LINATEMBEA |

**Masharti ya mnada**
1. Ukaguzi utaruhusiwa siku 2 kabla ya mnada.
2. Mununuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa kwenye mnada (au zaidi) na salio la 75% litalipwa ndani ya siku kumi na nne (14).
3. Endapo mshindi atashindwa kulipa salio la 75% kwa muda uliotolewa atakua amepoteza haki yake na mali itauzwa tena.

**Kwa mawasiliano zaidi wasiliana nasi kwa simu:**
**0767 608090,0784 773900/ 0786 1203012**

215217902



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 17//04/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMAPLI tarehe 12 /05/2019 kampuni ya S.S.F Co.LTD** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR** kuelekea **KAGERA** gari hilo lenye namba za usajili: **T794 DFQ /T 243 DCT.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 18.50
   Upana - mita 2.84
   Kimo - mita 5.20
3. NJia itakayotumika **DAR hadi KAGERA** kupitia **MWENDAKULIMA** gari litasafiri muda wa mchana tu(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215218702

## Prof. Ndalichako avipa changamoto vyuo vikuu utafiti

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Prof. Joyce Ndalichako, amevitaka vyuo vikuu nchini kuchapisha utafiti wao kwenye machapisho ya ndani na nje ya nchi ili kuvifanya kutambulika kimataifa badala ya kuishia kwenye maonyesho. Akizungumza jana wakati wa kufunga maoyesho ya utafiti mbalimbali yaliyoanza Jumatatu wiki hii, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) chini ya kauli mbiu ya utafiti kwa maendeleo jumuishi na endelevu, alisema utafiti ndiyo jambo linalokipaisha chuo kitaifa na kimataifa.

Alisema kila mwaka kuna taasisi za nje zinapanga vyuo vikuu duniani, na kwamba vyuo vya ndani havishiki nafasi nzuri kwenye utafiti kutokana na kutochapisha tafiti zao. "Kitaaluma tuko vizuri, lakini kinachotuangusha ni kwa sababu wanaangalia taaluma na utafiti, kinachotushusha nafasi ya vyuo vikuu vya Tanzania ni machapisho siyo ya kutosha. Inawezekana hata huu utafiti niliouangalia unaishia kwenye maonyesho, hauendi kwenye machapisho.

Waziri huyo alivitaka vyuo vikuu hivyo kutoa machapisho mbalimbali katika majarida ambayo yanatambulika kitaifa na kimataifa.

Aidha, alikipongeza UDSM kwa kutenga Sh.bilioni moja kwa ajili ya wahadhiri na wanafunzi kuendeleza utafiti, na kuvitaka vyuo vingine kuiga mfano huo kwa kuwa utafiti ndiyo muhimili wa elimu ya juu.

"Fedha mnazo tunawalipa fedha nyingi sana kupitia ada za wanafunzi, tunalipa mishahara, fedha mnazo kupanga ni kuchagua ila nawashauri mchague kufanya utafiti," alisema. Alisema wizara inaunga mkono uamuzi wa UDSM kubadili muundo wa ufundishaji kwa kufanya utafiti, ubunifu, teknolojia na ujasiriamali katika kutatua matatizo ya jamii, ili kuwa na wahitimu ambao wanaweza kujiajiri na kuajiri wengine.

Kwa mujibu wa Prof. Ndalichako, wakuu wa nchi za Afrika katika mkutano wa 23 walipitisha mkakati wa miaka 10 wa Sayansi, teknolojia na ubunifu kwa bara la Afrika, ambao ni sehemu ya agenda ya muda mrefu uliojikita katika kuendeleza eneo hilo kama dhana na viwezeshi vya kufikia maendeleo ya bara hilo.

Awali, Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. William Anangisye, alisema maonyesho hayo yatakuwa yanazunguka kwenye vyuo vilivyo chini ya UDSM, kwa kuwa utafiti ni kiungo muhimu kwa chuo, wadau na umma kwa ujumla.

"Wiki ya utafiti ndiyo mahali UDSM inaweza kurudi katika falsafa yake ya kuwatumikia Watanzania, tunataka kuwaonyesha wadau kuwa sisi ni sehemu ya jamii na siyo kisiwa kilichojitenga kisichofikiwa na watu wengine,tunayo ajenda, sera na dira ya chuo ya mwaka 1961 tunaiendeleza," alibainisha. Alisema katika kutoa msukumo kwenye utafiti na ubunifu wanatoa fedha kwa kutumia vyanzo vyake vya ndani, na kwamba walimu kutumia nafasi hiyo vizuri. "Fedha zipo kwa sasa itatusaidia kuwabana ambao hawachapishi, na kama umekaa kwa miaka saba hujachapisha andiko lolote kama Daktari au Profesa itabidi tukupeleke ukafundishe shule ya sekondari. Fedha hizi zitawezesha kuandika na kuchapisha kwenye majarida ya kimataifa, zitatolewa kwa uwazi na ushindani kwa kila mwalimu wa UDSM," alisema.

# Biteko: Watorosha madini wanatembea na mlango wa jela

**Na Rose Jacob,** MWANZA.

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amesema watoroshaji wa madini watambue wanatembea na kifungo na mlango wa jela ubavuni, na kwamba hakuna huruma yoyote kwa wale watakaobainika, ikiwamo kufilisiwa mali zao zote.

Biteko ameyasema hayo jijini Mwanza wakati akizindua soko la madini la kimataifa katika jengo la kitega uchumi la Rock City Mall, ambalo linakamilisha idadi ya masoko 13 yaliyofunguliwa katika mikoa inayojihusisha na shughuli hiyo, ikiwa ni kutimiza lengo la serikali la kuhakikisha sekta hiyo inaifikisha nchi kwenye uchumi wa kati ifikapo 2025.

Aidha, Biteko alisema leseni 33,000 ambazo zilikuwa zimeshikiliwa na watu, wizara imezifuta na watawapatia wachimbaji wadogo, imejipanga kuongeza wafanyakazi ambao sio rasmi ili kuepuka urasimu katika uendeshaji wa kazi katika masoko ya madini, wakati wakisubiri taratibu za kiutumishi kwa ajili ya kutoa ajira.

"Uzinduzi wa soko hili unatoa majibu kwa maswali ya wananchi kuhusu changamoto ya utoroshwaji wa rasilimali za madini ambayo imedumu kwa muda mrefu, sasa sitegemeii kusikia eti kuna watu wanatorosha madini... ambaye atabainika asije akailaumu serikali, adhabu ni kifungo na kuzitaifisha mali zake, maana atakuwa ametaka mwenyewe," alisema Biteko.

Kadhalika, Biteko alisema Tume ya Madini itaratibu bei za madini ndani ya soko hilo na kuhakikisha mchimbaji anapata stahiki zake, serikali inapata mapato yake na mfanyabiashara naye anufaike, kutaondoa uwezekano wa wanunuzi wa madini kuibiwa na wajanja wachache wanaojifanya wana madini kumbe hawana.

Mwakilishi wa wafanyabiashara ya madini mkoani Mwanza, Makono Kaniki, alimuomba Waziri Biteko kuwasaidia kutatua changamoto ambazo zinawakabili, ikiwa ni upatikanaji wa kibali maana kimekuwa kikipatikana Dodoma,ofisi ya ukaguzi iliyopo kiwanja cha ndege Mwanza iko nje inahatarisha usalama wa wauzaji madini na utitiri wa kulipia ushuru kutoka sehemu nyingine kwenda mahali pengine.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella, alisema, mkoa huo unatarajia kuwa na uchimbaji mkubwa wa dhahabu kupitia mgodi wa Nyanzaga uliopo wilayani Sengerema ambao kwa sasa upo kwenye mchakato wa kupata leseni.

"Mkoa una jumla ya leseni za utafiti wa dhahabu 57, uchimbaji mdogo 356 na uchimbaji wa kati 13, maeneo yanayozalisha madini aina ya dhahabu kwa wingi katika mkoa huu yapo wilayani Kwimba, Misungwi na kwa kiasi kidogo katika Wilaya ya Sengerema na almasi ni kiwango kidogo katika maeneo ya Mabuki na Mwamanga wilayani Misungwi," alisema Mongella.

Naye meneja wa NMB Kanda ya Ziwa, Abraham Augustino, alisema wanaunga mkono juhudi za serikali ya Rais John Magufuli za uanzishaji wa masoko ya madini, kwa kuwa hata wao wanaufaika kwa shughuli za kibenki na wameshaanza kuwakopesha wachimbaji wadogo na kuwapatia semina.




Abiria wakilisukuma basi ili kulinasua kwenye tope baada ya kukwama katika eneo la Kimambi, likitokea wilayani Liwale mkoani Lindi, kuelekea, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Vyakula, vinywaji, mafuta vyapaisha mfumuko wa bei

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFUMUKO wa bei wa Taifa kwa mwaka ulioishia mwezi Aprili, 2019 umeongezeka hadi asilimia 3.2 kutoka asilimia 3.1 kwa mwaka ulioishia mwezi Machi 2019.

Hali hiyo inamaanisha kuwa kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia mwezi Aprili, 2019 imeongezeka kidogo ikilinganishwa na kasi iliyokuwepo kwa mwaka ulioishia mwezi Machi, 2019.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Mkurugenzi wa masuala ya kitakwimu kutoka ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Irenius Ruyobya, alisema kuongezeka kwa mfumuko huo kumechangiwa na kuongezeka kwa bei za baadhi ya bidhaa za vyakula na sisizo za vyakula. Alisema baadhi ya bidhaa za vyakula ambazo zilichangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei wa mwezi Aprili, 2019 ni pamoja na samaki kwa asilimia 12.2, mafuta ya kupikia kwa asilimia 9.9, matunda kwa asilimia 12.6, maharage kwa asilimia 13.3 na mihogo mibichi kwa asilimia 8.5.

"Kwa upande mwingine, bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei wa mwezi Aprili, 2019 ni pamoja na mavazi kwa asilimia 3.8, huduma za vyakula na vinywaji kwenye migahawa kwa asilimia 4.6, huduma za malazi kwenye nyumba za wageni kwa asilimia 6.1, gesi ya kupikia kwa asilimia 2.6, mkaa kwa asilimia 10.9, gharama za kumuona daktari hospitali za binafsi kwa asilimia 6.6 na dizeli kwa asilimia 8.5 alisema.

Aidha alisema kuwa mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwezi Aprili,2019 umeongezeka hadi asilmia 0.9 kutoka asilimia 0.1 kwa mwaka ulioishia mwezi Machi, 2019.

Akizungumzia hali ya mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki, alisema Uganda mfumuko wa bei kwa mwaka unaoishia mwezi Aprili, 2019 umeongezeka hadi asilimia 3.5 kutoka 3.0 kwa mwaka ulioishia mwezi Machi,2019.

Hata hivyo, alisema nchini Kenya mfumuko wa bei kwa mwaka unaoishia mwezi Aprili, 2019 umeongezeka hadi asilimia 6.58 kutoka asilimia 4.35 kwa mwaka ulioishia mwezi Machi, 2019.



Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano,, Mhandisi Isack Kamwelwe (wa pili kulia), akikata utepe kuzindua mkataba wa huduma kwa wateja wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), jijini Dodoma jana. Wengine ni maofisa waandamizi wa mamlaka hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wabunge walia uhaba wa watumishi afya

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WABUNGE wameitaka serikali kuajiri watumishi wapya ili kutatua changamoto ya uhaba wa watumishi katika sekta ya afya nchini.

Wakichangia bungeni jijini Dodoma jana mjadala wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka ujao, wabunge walisema vituo vingi vya kutolea huduma za afya nchini vinakabiliwa na uhaba wa watumishi.

Mbunge wa Mpwapwa, George Lubeleje (CCM), alisema pamoja na serikali kufanikiwa katika ujenzi wa zahanati na vituo vya afya, changamoto iliyopo sasa ni upungufu wa watumishi wa idara ya afya.

Alisema kutokana na kada hiyo kukabiliwa na changamoto hiyo, anaishauri serikali iongeze watumishi katika vituo vya afya, zahanati na hospitali, hasa za wilaya na kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa dawa.

Mbunge wa Viti Maalum, Zainabu Vulu (CCM), mbali na kuzungumzia changamoto ya uhaba wa watumishi, alisema serikali ina jukumu la kuhakikisha kila mtu anapata elimu ya huduma ya afya na ikiwezekana uwekwe utaratibu ambao kila Mtanzania atamudu bima ya afya.

Mbunge wa Bukene, Seleman Zeddy (CCM), aliitaka serikali kuhakikisha zahanati 12 zinakuwa na waganga ili wagonjwa wapate huduma za uhakika.

"Hili litakwenda sambamba na ilani yetu

INAENDELEA UK. 26

# Mkataba huduma za wateja TCRA sasa kudhibiti rushwa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema kuanzishwa kwa mkataba wa huduma kwa mteja wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), utapunguza vitendo vya rushwa kwa kuwa hakutakuwapo masuala ya kuonana uso kwa uso kati ya mtoa huduma na mteja.

Aidha, baada ya kukamilika usajili wa laini za simu kwa kutumia alama za vidole, matukio ya wizi kwa kutumia simu na matumizi ya lugha chafu yatakuwa historia.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, alipokuwa akizindua mkataba huo ambao unalenga kutekeleza majukumu yake kwa uwazi ili kutimiza dhana ya uwajibikaji, jijini hapa.

Alisema rushwa itapungua maana mambo ya uso kwa uso yatapungua.

"Kwa kuwa kwa sasa tunakutana uso kwa uso kwenye utoaji huduma kwa wananchi lakini sasa upo mfumo rahisi," alisema.

Pia alisema utawezesha wahandisi kuzungumza na kwa simu bila kuonana na mteja na kwamba hali hiyo itapunguza majibu mabaya kwa wananchi ambayo yanaweza kutolewa na watoa huduma hao kwa kuwa akifanya hivyo, atabainika.

Aliwataka wananchi kutumia sekta ya mawasiliano kuleta maendeleo na kuboresha maisha yao.

Akizungumzia wizi kwa kutumia simu, Waziri huyo alisema baada ya muda mfupi, hakuna atakayeibiwa simu wala kutumia lugha chafu.

INAENDELEA UK. 26

## Wananchi walipwa bil. 1.9/- kupisha maji

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Maji imelipa jumla ya Sh.1,913,832,491 ikiwa ni fidia kwa wananchi waliokuwa na makazi kando kando ya Bonde la Mto Ruhila ambalo ni chanzo cha maji cha Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA) mkoani Ruvuma.

Wananchi hao wamekuwa wakifuatilia malipo yao kwa miaka 15 iliyopita tangu mwaka 2003. Malipo hayo yamefanyika kwa awamu tatu; awamu ya kwanza kiasi kilicholipwa ni Sh. 500,000,000/- na awamu ya pili na ya tatu kiasi kilicholipwa ni Sh.1, 413,832,491.

Taarifa ya Wizara ya Maji ilieleza jana kuwa kazi hiyo ya kuwalipa wananchi hundi zao imesimamiwa na SOUWASA.

Taarifa ilieleza kuwa idadi ya wananchi waliolipwa fidia ni 723. Hata hivyo, idadi ya wananchi wapatao 80 hawakujitokeza kuchukua hundi zao ambazo bado zipo katika Ofisi za Mamlaka, wananchi waliobaki wanaombwa kufika katika ofisi hizo kuchukua hundi zao.

CAPITAL RADIO

POPOTE ULIPO SIKILIZA CAPITAL RADIO KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.capitalradioco.tz @capitalradiotanzania @CapitalRadiotz capitalradiotz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Dk. Mengi upumzike mahali pema peponi

**ALIYEKUWA** Mwenyekiti Mtendaji wa IPP, Dk. Reginald Mengi, aliyefariki dunia mapema wiki iliyopita baada ya kuugua kwa muda mfupi Dubai, Falme za Kiarabu, atazikwa leo kijijini kwake wilayani Hai, Mkoa wa Kilimanjaro.

Dk. Mengi ambaye alizaliwa Mei 29, 1942, tangu alipofariki dunia ameelezewa na makundi mbalimbali ya jamii kwa matendo meme aliyotenda kwa muda wote wa uhai wake wa kuishi duniani wa miaka 77.

Amezungumziwa kwamba alitenda mambo mengi mazuri, kikubwa kikiwa ni kuuchukia umaskini, hivyo kutumia muda wake na rasilimali alizozimiliki kuwasaidia watu wengine katika jitihada za kujikwamua katika umaskini.

Uthibitisho kwamba Dk. Mengi alitenda mazuri mengi duniani kwa jamii umedhihirishwa kwa jinsi kifo chake kilivyoigusa sana jamii nzima.

Mapokezi ya mwili wake kutoka Dubai Jumatatu kuanzia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam hadi katika Hospitali ya Jeshi la Lugalo kuhifadhiwa, ni moja ya uthibitisho huo kuwa alikuwa ni mtu wa watu wote.

Makundi yote ya jamii bila kujali watoto, vijana, watu wazima, wazee, wenye ulemavu na kujitokeza katika mitaa mbalimbali kumlilia vinathibitisha kuwa jamii imeondolewa na mtu muhimu aliyewagusa wengi.

Katika shughuli ya kuuaga mwili wake juzi jijini Dar es Salaam umati uliojitokeza na salamu zilizotolewa na makundi mbalimbali ya jamii, ikiwamo serikali ni uthibitisho mwingine.

Kadhalika, mapokezi makubwa ya mwili wake katika Uwanja wa Ndege Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) jana, wakati ukitoka Dar es salaam kwenda kijijini kwake wilaya ya Hai kwa ajili ya mazishi leo, pia ni uthibitisho kuwa alikuwa anapendwa na kukubalika kwa wengi.

Mengi yamezungumzwa na mengine yataendelea kuzungumzwa juu yake kuhusiana na mchango wake mkubwa alioutoa kwa jamii, lakini jambo la msingi kwa jamii baada ya kumpumzisha leo katika nyumba yake ya milele ni kila mmoja kujitathmini kama katika maisha yake ametenda mambo memgi na yenye hoja kwa jamii ambayo yatamfanya athaminike na kugusa wengi kama marehemu Dk. Mengi.

Mambo aliyoyafanya Dk. Mengi katika kusaidia jamii ni mengi na kwa kukumbushia machache ni kusapoti uhifadhi wa mazingira, kusaidia vita dhidi ya umaskini, kupiga vita rushwa, kutoa ajira kwa wananchi, kuwezesha watu wenye ulemavu na mengine mengi ambayo hayawezi kutosha katika safu hii.

Ni kweli kwamba nafasi yake katika jamii itakuwa vigumu kuiziba, lakini tunamini kuwa wapo watu ambao wataweza kujitolea kujitoa kwa ajili ya kuisaidia jamii kama alivyofanya marehemu.


Hatuwezi kusema zaidi, kikubwa tunaamini kuwa Mungu atasikia maombi na sala ambazo wengi wamemuombea Marehemu Dk, Mengi katika kipindi chote cha msiba na maombolezo, ikiwamo siku ya leo ya kuupumzisha mwili wake katika nyumba yake ya milele.

Tunamuomba mwenyezi Mungu aipumzishe roho ya Dk. Mengi mahali pema

peponi, lakini tukiamini kuwa ushauri aliouacha katika kitabu chake cha I Can', I Must', I Will', kitabaki kuwa urithi kwa kila Mtanzania ambaye ana ndoto za kujikwamua kutoka kwenye umaskini. Bwana alitoa, Bwana ametwaa, jina lake lihidimiwe. Amina.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Asante Makamba, mazingira ndiyo yaamue kuhusu plastiki

**SERIKALI** imesisitiza msimamo wake kuwa, haina mpango wa kuongeza muda kwa wamiliki wa viwanda vinavyozalisha mifuko ya plastiki iliyopigwa mafuruku na kufafanua kuwa zuio hilo litakuwa la sheria.

Inawataka wafanyabiashara na wazalishaji wa mifuko wasipoteze muda kuomba muda wa matumizi ya mifuko hiyo, badala yake wazingatie kile ambacho imewaelekeza.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira ) January Makamba, alisema hayo katika kikao chake na wazalishaji. Aliweka wazi kwamba, hakuna kurudi nyuma katika vita dhidi ya mifuko hiyo.

Makamba anasema, hatua ya kupiga marufuku mifuko hiyo, lengo lake ni kulinda afya za wananchi na mazingira, hivyo serikali haiwezi kurudi nyuma na imeashaamua kuwa Juni Mosi ndio mwisho wa mifuko hiyo.

"Madhara yanayotokana na matumizi ya mifuko hiyo ni makubwa, hivyo siyo rahisi kwa mtu kuona katika hali ya kawaida. Wizara, itahakikisha hatua hiyo inafanikiwa bila vikwazo na wananchi wataendelea kuelimishwa.

"Katazo la kitu kama hiki halikosi vikwazo, kelele na hata vitisho kutoka kwa watumiaji na wazalishaji. Hivyo, tumejipanga kukabiliana na yote hayo. Katika kukabiliana na zuio hili, changamoto ni nyingi ikiwamo kutokuwa na ufahamu mpana wa wananchi juu ya athari zake, lakini tumejipanga kuhakikisha linafanikiwa na hatua muhimu zaidi ni kutoa elimu kwa wananchi," anasema.

Anasema, elimu ya kutosha itatolewa kuhusu madhara ya mifuko ya plastiki na njia mbadala zitaanza kutumika wakati wa kipindi cha zuio na kwamba, serikali imejipanga jinsi ya kukabiliana na changamoto zitakazojitokeza.

Waziri anasema, kinachotakiwa ni ushirikiano kutoka kwa wazalishaji hao na wananchi kwa ujumla, kwa vile mazingira ni suala muhimu kwa kizazi cha sasa na kijacho, hivyo ni jukumu la kila mmoja kuyalinda.

Nimejaribu kueleza kwa kirefu kile kilichosemwa na waziri, kutokana na ukweli kwamba jambo hilo halikuanza jana wala juzi, bali la miaka mingi.

Limekuwa likisemwa, lakini utekelezaji umesuasua.

Muda huo ungetosha kwa wahusika kujipanga badala ya kuibuka tena na kuanza kuomba kuongezewa muda huku wakijua kwamba serikali ilianza 'kubipu' kuhusu mifuko hiyo zaidi ya miaka mitano iliyopita.

Kunaendelea kuomba muda ili wajiandae, ni sawa na kuendelea kuweka rehani afya za Watanzania na mazingira yao kwa ujumla. Ni muhimu wakaangalia uwezekano wa kuzalisha mbadala, kuliko kung'ang'ania kisichowezekana.

Ikumbukwe huko nyuma, aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais anayehusika na Mazingira, Dk Terezya Huvisa, aliwahi kutoa muda wa miezi mitano kwa wazalishaji na wauzaji.

Jambo la kushangaza ni kwamba, serikali imetangaza kufikia Juni mosi mwaka huu, ambayo ni wiki tatu zijazo, ndio mwisho wa mifuko hiyo, halafu wanajitokeza tena kuomba kuongezewa muda.

Wakumbuke ni miaka mingapi imepita tangu walipopewa muda wa miezi mitano ya kuachana na uzalishaji na uuzaji wa mifuko hiyo, halafu leo wanakuja tena na hoja hiyo hiyo ya kutaka kuongezewa muda.

Madhara ya mifuko hiyo yamekuwa yakielezwa mara kwa mara na wataalamu wa afya, sasa wazalishaji na wauzaji wanapoomba kuongezewa muda, maana yake wanataka waendelee kuweka rehani afya za Watanzania.


Bidhaa zote za plastiki na hasa mifuko laini inatajwa kuchangia katika uchafuzi wa mazingira kwa kuharibu udongo, kuleta gesi za sumu na hivyo kusababisha madhara ya kiafya kwa binadamu.

Katika hilo kweli 'Hapa kazi tu' kwani salama za marufuku tumeaza kuzipata kupitia ujumbe katika simu zetu za mkononi.



# HUZUNI 1942 - 2019






Gari maalum likiwa tayari kwaajili ya kuubeba mwili wa marehemu Dk. Reginald Abraham Mengi, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), jana.



Umati wa wananchi na waombolezaji wakisubiri kuupokea mwili wa Dk. Mengi.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Nshara, wakiwa kando ya barabara wakishuhudia msafara wakati mwili wa Dk. Mengi ukipelekwa Machame.



Wananchi wa Mji wa Bomang'ombe, wakiwa wametandika kanga barabarani ili gari lenye mwili wa Dk. Mengi lipite juu yake kama ishara ya heshima kwa marehemu.



Gari lenye mwili wa marehemu likiwa limezongwa na wananchi na waombolezaji ili waweze kumuaga mpendwa wao.



Askari wakijitahidi kuwasogeza pembeni wananchi, ili msafara uweze kupita. **PICHA ZOTE: GEODFREY MUSHI**

# Asasi sasa zalia na mbinu mpya

INATOKA UK. 3

Gazeti hili lilipomtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma Martin Otieno ili azungumzie taarifa hizo halikufanikiwa kumpata baada ya simu kuita bila kupokelewa na hata alipotumiwa ujumbe mfupi wa maandishi haukujibiwa.

Akisimulia baadhi ya matukio hayo mwanasheria wa Taasisi ya utafiti ya Twaweza, Annastazia Rugaba, alisema matukio hayo yamekuwa yakijirudia mkoani humo.

"Matukio haya ni mengi sana hapa tunasikia wale walioumizwa na kupiga kelele, lakini kuna wengine wengi wanakaa kimya kwa kuogopa fedheha " alisema Annastazia na kuongeza: "Kuna mama wa miaka 36 ameingiliwa mara 6 akajeruhiwa mara nne, 2017 aliingiliwa mara tatu ,2018 aliingiliwa mara moja, 2019 ameingiliwa mara mbili."

Kwa upande wake mmoja wa waathirika wa vitendo hivyo ambaye ni mkazi wa mkoa huo Ramla Issa, vitendo hivyo vimekithiri zaidi katika eneo la Mwanga Kusini mkoani Kigoma na kwamba hadi sasa wanawake 45 wamebainika kutendewa ukatili huo ikiwamo kujeruhiwa kwa mapanga na visu.

"Mimi nilivamiwa na mtu mmoja usiku nikiwa nimelala, alikuwa na lengo la kunibaka, na katika harakati za kubishana naye na alivyoona kwamba nimekataa ndipo alinikata na panga na katika kujiokoa likawa limekata mikono yangu yote miwili,,"alisema Ramla.

Aliongeza: "Wakati ananishambulia nilipiga kelele na nikasikia kama vishindo vya watu wanakuja na ndipo alikimbia, msaada niliopata ni wa kupelekwa hospitali nilitapakaa damu hadi usoni, walifika watu na kunisaidia kwenda polisi, nilipofika nilistushwa na jinsi walivyonipokea na kuniuliza vipi wamefanikiwa? nilijisikia vibaya sana, " Ramla anaeleza.

Ramla alisema wabakaji hao katika mbinu yao hiyo mpya wamekuwa wakijipaka mafuta machafu au kinyesi cha binadamu wanapokwenda kutekeleza ukatili wao kama kinga ili pia isiwe rahisi kuwakamata kwa mikono.

# 1,200 waugua Dengue Dar

INATOKA UK. 3

dawa kitandani.

Alisema pia wananchi watakiwa kupaka mafuta ya kufukuza mbu mikononi na miguuni na kuvaa nguo ndefu kufunika mwili kama mikono, miguu na mgogo.

Alisema Manispaa zote za mkoa huo zinatekeleza mpango wa upuliziaji wa viuatilifu katika madimbwi yanayotuamisha maji katika kudhibiti ugonjwa huo.

"Kila Manispaa imetekeleza na zinaendelea kutekeleza hili kwa lengo la kuhakikisha ugonjwa huu hauendelei kuenea kwa watu wengi lakini pia kupunguza kasi ya uzalianaji wa mbu hawa wenye virusi vya homa na dengu," alisema Dk. Ngudibe.

Kadhalika, alivitaka vyombo vya habari kuendelea kuelimisha jamii kuhusu kuwapo kwa ugonjwa huu ili wananchi waendelee kuchukua tahadhari.

Aliwataka pia wamiliki wa maeneo yenye mikusanyiko ya watu kuchukua tahadhari ili kuepusha kuenea kwa ugonjwa huu kwa watu wengi zaidi.

"Wito wangu kwa vyombo vya habari viendelee kuelimisha wananchi wa mkoa huu na mikoa ya jirani kuhusu ugonjwa huu. Wananchi wachukue tahadhari ili kuepuka maambukizi," alisema Dk. Ngudibe.

Pia aliwataka wananchi kwenda kwenye vituo vya kutolea huduma za afya wanapohisi dalili za homa ya dengu ili kuwahi kupata matibabu.

Kwa mujibu wataarifa iliyotolewa na Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Mohames Kambi Aprili 12, mwaka huu, watu 304 walikuwa wameripotiwa kuugua ugonjwa huo katika mikoa ya Dar es Salaam (252) na Tanga (52).

**WAZIRI ATOA TAHADHARI**

Wakati huo huo, serikali imewataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa dengue ambao umekuwa tishio nchini.

Akiwasilisha bungeni juzi hotuba kuhusu makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha , Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema mlipuko wa ugonjwa huo mwaka huu ulianzia Januari na kwamba hadi kufika Machi, wagonjwa 523 wametolewa taarifa.

Kati yao, 467 wametoka Dar es Salaam na 56 wametoka Mkoa wa Tanga.

Alisema wizara imeshakamilisha mpango mkakati wa kudhibiti ugonjwa huo ambao unajumuisha kujenga uwezo wa watumishi wa afya katika kutambua, kupima, matibabu na udhibiti wa mbu wanaoueneza.

"Ninatoa wito kwa wananchi kuwa makini wapatapo homa na wahakikishe wanakwenda kupata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya ili waweze kupimwa na kupatiwa tiba sahihi," alisema.

Waziri huyo pia alisema wizara yake imeboresha utoaji wa taarifa mapema za magonjwa ya milipuko kwa njia ya kielektroniki (e-IDSR) kuanzia ngazi ya vituo vya kutolea huduma.

Alibainisha kuwa hadi kufikia Machi mwaka huu, mikoa 25 kati ya 26 imekwisha kuanza kutoa taarifa kwa njia hiyo ya elektroniki.

**KUHUSU DENGUE**

Homa ya dengue ni ugonjwa wa kitropiki unaosababishwa na virusi vya dengue maarufu kama dengue.

Homa ya dengue pia hujulikana kama, homa ya kuvunja mifupa kwa sababu inaweza kuwafanya watu wawe na maumivu makali hadi wahisi kama mifupa yao inavunjika.

Dalili za ugonjwa huu huanza siku tatu hadi kumi na nne baada ya kuambukizwa.

Baadhi ya dalili ni homa kali, kuumwa na kichwa, kuota vipele kwenye ngozi na maumivu kwenye misuli na maungio.

Kwa watu wachache, homa ya dengue inaweza kubadilika na kuwa aina zinazohatarisha maisha.

Dalili kubwa ni ile ya kuvuja damu, ambayo huifanya mishipa ya damu inayobeba damu.

Kwa kawaida matibabu huchukua siku tatu hadi saba hadi mgonjwa kupona na hakuna dawa ya chanjo inayofanya kazi kuwakinga watu dhidi ya virusi vya dengue.

**Imeandikwa na Mary Geofrey (Dar na Sanula Athanas (Dodoma).**

# Dk. Mengi aiteka Kilimanjaro

INATOKA UK. 2

baadhi ya wafanyabiashara akiwamo rafiki wa Dk. Mengi, Felix Mosha.

**RATIBA YA MAZISHI**

Ratiba ya mazishi hayo iliyonyesha kuwa mwili Dk. Mengi baada ya kupokelewa waombolezaji mbalimbali watatoa heshima za mwisho na utazikwa kwenye makaburi ya familia nyumbani kwake Kisereni, Kijiji cha Nkuu Sinde, Kata ya Machame Mashariki, Wilaya ya Hai.

Leo Alhamisi), mwili wa Dk. Mengi utaondolewa eneo la Nkwasero Machame na kupelelekwa Moshi Mjini katika kanisa kuu la Usharika wa Moshi wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ambako wananchi wote wa Mkoa wa Kilimanjaro watapata fursa ya kutoa heshima za mwisho kabla ya kuanza ibada ya mazishi.

Baadae mchana mwili wake utarejeshwa tena Kijiji cha Nkuu Sinde, Kata ya Machame Mashariki ambako ndiko makazi yake ya milele yalipo nyumbani kwake Kisereni.

Ibada ya mazishi hayo ya Dk. Mengi itaendeshwa na Mkuu wa KKKT, Askofu Dk. Fedrick Shoo ambaye atasaidiwa na maaskofu wengine wastaafu Dk. Erasto Kweka na Askofu Dk. Martin Shao.

Maaskofu wengine watakaoshiriki ni pamoja na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Arusha, Mhashamu Askofu Isaac Amani.

**SALAMU ZA KKKT**

Akitoa salamu za KKKT, Mkuu wa Kanisa hilo, Askofu Dk. Fredrick Shoo, alisema kuwa kanisa halina la kusema zaidi ya kumwambia Mwenyezi Mungu asante kwa kuwapa mtu huyo muhimu.

Askofu Dk. Shoo alisema kuwa, watu wengi wamekuwa wakielezea jinsi ambavyo Dk. Mengi amegusa maisha yao na kudai kuwa marehemu alikuwa ni zawadi kutoka kwa Mungu.

Askofu huyo alitumia nafasi hiyo kumuomba Mwenyezi Mungu kuwafariji wale wote waliokuwa na msiba huo pamoja na familia kwa ujumla.

"Tunapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa ajili ya kutupa Dk. Mengi kwa kipindi chote tulichokuw anaye na tuiombee familia ipate nguvu katika kipindi hiki kigumu," alisema Dk. Shoo.

# Gwajima akimbilia TCRA, polisi wamkingia kifua

INATOKA UK. 2

zangu, naipresent Tanzania," alisema Askofu Gwajima na kuongeza:

"Nafasi yangu katika taifa ni kusema, tena kwa usahihi bila kumung`unya maneno, na ndiyo maana watu wamekuwa wakijaribu kuleta matukio kunifanya nikose sauti, kwamba wanipige ili nisiseme. Sasa nawaambia kwamba hawawezi kunimaliza nguvu na sasa hivi ndiyo nimeanza na safari hii nitapiga kali kuliko zile zilizopita."

Gwajima alisema hakuna mtu ambaye anaweza kujirekodi mwenyewe video mbaya kama hiyo iliyokuwa ikisambaa halafu akatuma mwenyewe.

"Ninaomba kila mtu atumie akili yake, kwamba ni mwanamume gani ambaye anajamiiana halafu, ajirekodi, halafu atume mwenyewe, hakuna mjinga wa namna hiyo duniani. Huyo mtu aliyesambaza hiyo video aliweka 'image za aina mbili tofauti' kichwa ni cha mwingine na mwili ni wa mtu mwingine, halafu mkono unaoonekana ni wa baunsa," alisema Askofu Gwajima.

Aliongeza: "Huyu mtu alitumia picha ya familia ambayo nilipiga na familia mwaka 2008 nikiwa kifua wazi ambayo tuna haki ya kupiga picha za namna hiyo kama familia, na video hiyo nilianza kuiona jana(juzi) asubuhi, kwa hiyo hatua za awali ambazo nimezichukua, nimekwenda Polisi nimechukua RB, na kuiomba TCRA imtafute huyu mtu."

Askofu Gwajima alisema Jumapili ataanza upya kupambana na watu wanaomchafua, huku akijitapa kwamba vita hiyo itakuwa kubwa zaidi ya iliyokuwapo mwaka jana. "Ninamuonya huyu mtu ambaye yuko nyuma ya haya na endapo atashindwa kufanya yale yanayompasa kufanya, Jumapili nitaanza kumgawia vitu vyake, nitarudisha jumapili zileeee ambazo watu walikuwa wanakusanyika kutoka sehemu mbalimbali kuja kusikiliza," alisema Askofu Gwajima.

"Nitawapa update, naifanyia kazi na nakaribia mwishoni ya nani kwa nini na anatuma kutoka wapi, lakini anayetuma yuko hapa Tanzania na ni yule yule ambaye anatakiwa asagwe vipande vipande na atapotea kwa mara nyingine tena."

Kwa upande wake mke wake alisema yeye anafahamu ukweli na anamwamini mume wake.

"Mimi ni jasiri kama simba, ukweli nina ufahamu, mume wangu nina mfahamu na nina mwamini na ukweli ndiyo huo hakuna mtu anayeweza kuubadilisha, niko pamoja na yeye, nitasimama pamoja na yeye na Mungu akiwa upande wetu hakuna takayekuwa juu yetu," alisema.

**Wakati huo huo** Jeshi la Polisi, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, lilisema linafanyia uchunguzi video hiyo na kusema kwamba Askofu Gwajima si mtuhumiwa wa video ya ngono inayosambaa mitandaoni. Alisema video hiyo ina lengo la kumchafua mtumishi huyo wa Mungu ambaye ni muathirika wa tukio hilo na amemtaka kuwa mtulivu wakati Jeshi la Polisi linaendelea na upelelezi wa tukio hilo.

Kamanda wa Polisi, Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Lazaro Mambosasa, aliyesema hayo mbele ya waandishi wa habari jana katika mkutano wake wa kutolea ufafanuzi wa tukio hilo lililozua taharuki kubwa kwenye mitandao ya kijamii.

Alisema Jeshi la Polisi Makao Makuu, Kitengo cha Upelelezi wa Makosa ya Jinai, linalifanyia kazi suala hilo na kuwataka waumini wa kanisa lake kuwa watulivu wakati wakiendelea na kazi hiyo.

"Nimewaita nitoe taarifa ya tukio lililotokea jana (juzi) na kuleta hisia mbaya kwa jamii, picha hizo zinaonekana Askofu Gwajima na mwanamke ambaye ameficha uso wake. Jana (juzi) kulikuwa na taarifa angeitwa kuja kutoa taarifa kuhusu hili. Ninachoweza kusema Gwajima katika hili si mtuhumiwa na Baba Askofu Gwajima katika hili ni muathirika," alisema Mambosasa.

Alisema katika hali ya kawaida halikuonekana kama tukio ambalo lingeweza kutokea ndani ya jamii na lina lengo la kumchafua mtumishi wa Mungu na kwamba uchunguzi umeshaanza tangu juzi.

Aliwataka Watanzania kuwa watulivu na kuacha kutolea majibu suala hilo kwa sababu wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo ili kuwabaini waliohusika.

Alisema atakayebainika kuhusika na tukio hilo atachukuliwa hatua za kisheria bila kujali nafasi yake ndani ya jamii.

Kamanda Mambosasa alisema wakazi wa Dar es Salaam wanatakiwa kuwa watulivu wakati wakifanya uchunguzi na upelelezi wa kina wa tukio hilo.

HABARI KITAIFA

# NEMC sasa kuhuisha sera kukabiliana mazingira bahari

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limejipanga katika kuboresha mazingira katika ukanda wa Bahari ya Hindi ili kwenda sambamba na malengo ya kituo cha mazingira kimataifa (GEF)

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, wakati wa warsha ya kujadili Uhuishaji wa Sera Kukabiliana na Mazingira ya Bahari ya Hindi

iliyoandaliwa na Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa (UNEP) na

kuwakutanisha wadau wa sekta za umma na binafsi, Mwenyekiti wa NEMC, Prof. Esnati Chaggu, alisema programu italeta mafanikio katika usimamizi wa mazingira baharini.

"Programu hii itakuwa na tija kubwa kwa Taifa katika kuilinda Bahari na viumbe vilivyomo, lakini muhimu zaidi kwa watu wote wanaoendesha shughuli zao za uchumi kupitia Bahari ya Hindi," alisema Prof. Chaggu.

Aliongeza kuwa uboreshaji wa sera utasaidia kuongeza thamani ya mazao yanatokanayo na bahari na hivyo kuinua uchumi kwa wananchi wa maeneo ya ukanda wa pwani na taifa kwa ujumla

"Tuwashukuru wenzetu wa UNEP kwa kuleta mradi huu ambao utasaidia kuongeza thamani ya mazao ya bahari, hivyo kuwa na soko la uhakika ndani na nje ya nchi kwa kuwa mradi utahakikisha mazingira ya bahari yanakuwa salama," alisema.

Meneja wa Mradi huo kutoka Programu ya Mazingira ya UNEP, Sinikinesh aliyataja mambo manne muhimu katika utekelezaji wa mradi huo ambayo yataiweka Tanzania na mataifa yaliyopo magharibi mwa Bahari ya Hindi katika nafasi nzuri ya kuongeza

thamani ya mazao ya Baharini. "Mradi huu unatekelezwa katika nchi tisa na umejikita katika kusaidia mabadiliko ya sera, Kupunguza changamoto kupitia ushiriki wa jamii endelevu katika usimamizi wa rasilimali endelevu, kupunguza changamoto zilizopo sekta binafsi na kuzijengea táasisi na jamii uwezo ili kuongeza thamani ya mazao na sughuli zingine baharini," alisema.

Mratibu wa Mradi huo kutoka NEMC, Rose Mtui, alisema mradi huu utasaidia kuinua uchumi kwa jamii mbalimbali zinazotegemea

uchumi wake kupitia bahari

"Utekelezaji wa mradi huu utakuwa na faida kubwa kwani utabadilisha changamoto nyingi na kuwa fursa, hivyo kuongeza mapato kwa jamii

zinazotegemea Bahari kama kitega uchumi lakini kwa kuyatunza mazingira ya bahari kutaongeza thamani ya mazao ya baharini, hivyo kuwa na uhakika wa soko," alisema Mtui.

Mradi huo utatekelezwa Kenya, Comoro, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Seychelles, Somalia, Afrika Kusini na Tanzania, na utagharimu dola za Marekani milioni 8.8 zitakazotumika katika kuwajengea uwezo taasisi na jamii, maboresho ya sera, kupunguza changamoto kupitia ushiriki wa jamii pamoja na kushughulikia changamoto zilizopo katika sekta binafsi.



Mwenyekiti wa NEMC, Prof. Esnati Chaggu, (kulia), akifurahi jambo na Meneja wa Mradi kutoka Programu ya Mazingira ya Umoja wa Mataifa, Sinikinesh Beyene (kushoto), baada ya warsha ya kujadili mradi wa uhuishaji wa sera ya kukabiliana na mazingira ya Bahari ya Hindi kumalizika jijini Dar es Salaam.(katikati) ni Mkurugenzi wa Utafiti za Mazingira na Usimamizi wa Mfumo ekolojia, Joseph Kombe. **MPIGAPICHA WETU**

# Msako vitambulisho wamachinga nyumba kwa nyumba

**Na Gurian Adolf,** KATAVI

SERIKALI ya Wilaya ya Mpanda mkoani Katavi, imetoa siku saba kwa wajasiriamali wadogo wanaofanya biashara wawe na vitambulisho na endapo watakaidi, wataanza kukamatwa.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Lilian Matinga, aliyasema hayo wakati akilihutubia baraza la Madiwani wa Manispaa ya Mpanda.

Alisema anatoa siku saba kwa wafanyabiashara wadogo na wajasirimali ambao hawaja pata vitambulisho wawe wamepata na ifikakapo Jumatatu ya wiki ijayo na yeyote ambaye hatakuwa na kitambulisho hataruhusiwa kufanyabiashara na akikaidi atakamatwa.

Alisema kuanzia Jumatatu ataongoza askari wa polisi kukamata wafanyabiashara wadogo wote ambao watakuwa wanafanyabiashara bila vibali, na msako huo atakuwa wa nyumba kwa nyumba.

Matinga alisema kuwa wilaya ya Mpanda ilipokea vitambulisho 25,000, lakini cha kushangaza hadi sasa ni vitambulisho 2,000 tu ndiyo vilivyotoka wakati Serikali imewajali wafanyabiashara hao kwa kuwapa vitambulisho ili wasibughudhiwe.

Naye Meya wa Manispaa ya Mpanda, Willy Mbogo, alisema baadhi ya wafanyabiashara wadogo wanashindwa kuwa na vitambulisho vya ujasiriamali kutokana na uwezo mdogo wa kifedha kwa kushindwa kulipia Sh. 20,000 za vitambulisho.

Alisema kutokana na kuwa na uwezo huo mdogo wa kifedha, baadhi yao wamekuwa wakiomba Serikali iwapunguzie kiwango hicho cha pesa .

Katibu Tawala wa Wilaya ya Mpanda, Sosisten Mayoka, alisema wilaya hiyo imeshaweka utaratibu wa kupokea fedha kidogo kidogo kutoka kwa wafanyabiashara wanaoona hawana uwezo wa kulipa kiasi hicho kwa mara moja, na baada ya kufikisha Sh. 20,000 wamekuwa wakipewa vitambulisho hivyo.

# Waganga, Ma-DC wapewa jukumu la dengu

**Na Dege Masoli,** TANGA

MLIPUKO wa ugonjwa wa dengu uliyoukumba mkoa wa Tanga umeilazimu ofisi ya afya kuwataka waganga wakuu wa wilaya na wakuu wa wilaya za mkoani kuchukua tahadhari kwa kutoa elimu kwa umma kujihami.

Hayo yalielezwa na Afisa wa Afya Mkoa wa Tanga, Jumanne Magoma, alipokuwa akitoa taarifa ya hali ya ugonjwa wa dengu na Chipungunya ilivyo katika Mkoa wa Tanga.

Alisema Mkoa wa Tanga ulikumbwa na mlipuko wa ugonjwa huo Januari 2, mwaka huu kwa kumpata mtu mmoja na baadae wengine waligundulika.

Alieleza kuwa hadi kufikia Machi 31, jumla ya watu 165 walihisiwa kuugua dengu na kwamba baada ya vipimo, 61 walibainika kuwa na ugonjwa na walianza kupatiwa huduma.

Magoma alieleza kuwa wagonjwa waliokutwa na ugonjwa huo walitibiwa na kwamba hakuna waliyopoteza maisha wala idadi kuongezeka baada ya hapo.

Alieleza kuwa baada ya kutokea kwa mlipuko huo jamii imekuwa ikielimishwa ili kutambua viashiria na namna ugonjwa huo unavyoweza kubainika na kuwataka wananchi kuchukua tahadhari ikiwamo usafi wa mazingira.

Aliongeza kuwa waganga wa wilaya na wakuu wa wilaya walishapewa jukumu la kutoa elimu kwenye maeneo yao kwa kuzishirikisha kamati za ulinzi lengo likiwa kudhibiti ugonjwa huo kuenea katika maeneo mengine ya mkoa huo.

Aliwataka wananchi wanapoona dalili za ugonjwa huo wakimbilie kwenye vituo vilivyopewa jukumu la kupima dengu ambavyo pamoja na Hospitali ya Rufani ya Bombo. Zingine ni Burhan, Agakhan na Shufaa.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na Wabunge Peter Serukamba wa Kigoma Kaskazini (kulia) na David Silinde wa Mbozi Magharibi, katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: OWM**

# Wizara yajitetea upendeleo mikopo

NAIBU Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, amesema taarifa za Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), kuwapendelea vigogo wake kwenye utoaji wa mikopo si za kweli.

Mgumba alitoa kauli hiyo jana bungeni alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Ulanga (CCM), Goodluck Mlinga, aliyehoji kwanini benki hiyo hutoa mikopo kwa upendeleo hasa kwa wake za vigogo wake. Mlinga alisema benki hiyo imekuwa ikitoa mikopo kwa upendeleo kwa kuwaacha baadhi ya wanawake na kutoa kwa wake wa vigogo wake.

Katika majibu yake, Mgumba alikanusha madai hayo na kueleza kuwa benki hiyo imeanzishwa kwa lengo la kukuza uchumi.

Mgumba alisema wanaopata mikopo ni wale ambao wametimiza vigezo.

"Tumetoa maelekezo wanawake wajiunge na vikundi na vikundi ndiyo vitakuwa dhamana na tuliagiza asilimia 20 iende kwao na tumewaelekeza watoe mikopo kwa kina mama," alisema. Alisema hadi sasa, benki hiyo imeishatoa asilimia 33 ya mikopo.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Esther Mmasi, alitaka kauli ya serikali kuhusu ushiriki wa wanawake kwenye sekta ya kilimo.

"Changamoto kubwa inayowafanya wanawake wa Tanzania wasishiriki kwenye sekta ya kilimo ni ufinyu wa bajeti na mtaji kutoka taasisi za kifedha. Je, nini kauli ya serikali? mbunge huyo alihoji.

Mgumba akijibu swali hilo, alisema sekta ya kilimo inajumuisha sekta ndogo ya kilimo mazao, mifugo, uvuvi na misitu.

Alisema katika kutatua changamoto hizo, serikali inaendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2004.

Ripoti ya ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, kwa mwaka wa fedha 2016/17, ilieleza kuwa alibaini sehemu kubwa ya fedha za benki hiyo zimekopeshwa kwa watendaji wa benki hiyo.

# Wakala wa mafunzo ya uvuvi waanzishwa

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi, imeanzisha wakala wa mafunzo wa Uvuvi ili kuwapatia elimu vijana kuhusu masuala ya uvuvi ili nchi inufaike na rasilimali za uvuvi iliopo.

Hayo yalibainishwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalah Ulega, alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Asha Jecha. Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali imewaandaaje wananchi wanaoishi katika ukanda wa bahari ili wafanye uvuvi wenye tija. Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema serikali pia imeanzisha Taasisi ya Utafiti (Tafiri) ili kufanya tafiti na kuvumbua teknolojia itakayowasaidia kuleta tija kwenye tasnia ya uvuvi.

Alisema taasisi hizo husaidia kuwapa elimu na maarifa wadau wa uvuvi ili wavue kwa tija.

Alisema wizara ina mikakati mbalimbali inayolenga kuleta maendeleo katika sekta ya uvuvi na kuwasaidia wavuvi kimkakati na kuendelea kutoa elimu kwa wavuvi.

Alisema mikakati mingine ni pamoja na kuwekeza katika uvuvi wa Bahari Kuu kwa kufufua Shirika la Uvuvi (Tafico).

Hata hivyo, Ulega alisema wizara yake imeanzisha dawati la sekta binafsi ili kuwasaidia wavuvi kutatua changamoto zinazowakabili ikiwamo kupata mikopo kutoka taasisi za fedha.

# Serikali yafafanua umri ajira kwa mtoto

BUNGE limeelezwa kuwa sheria inakataza kuajiri mtoto chini ya miaka 18 isipokuwa katika mazingira maalum.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Ajira na Vijana, Anthony Mavunde, alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Kiteto Koshuma.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji kwanini serikali isiweke umri wa kuajiriwa kuwa ni miaka 21 hadi 35 ili kuwezesha vijana wengi wanaotoka vyuoni kupata ajira.

Akijibu swali hilo, Mavunde alisema serikali imeweka utaratibu huo kupitia Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Namba 6/2004 kifungu cha tano na ndiyo inayotoa maelekezo zaidi.

"Kutokana na kifungu hicho umri wa kuajiriwa ni miaka 18 na kuendelea pamoja na masharti yaliyotajwa katika kifungu hicho cha tano," alisema.

Mavunde alisema ni muhimu kuendelea kuhimiza waajiri wote kutii sheria za kazi na kuhakikisha vijana wote wenye sifa wanapomaliza mafunzo yao na kutimiza umri wa kuajiriwa wanaajiriwa.

Alisema vijana hao wanaajiriwa kwa kuzingatia fursa zilizopo kwa waajiri na masharti ya kazi husika.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Mbulu wamfagilia JPM kuwapiga jeki

Na Cynthia Mwilolezi, MANYARA

WILAYA ya Mbulu Mkoani Manyara imempongeza Rais John Magufuli, kwa kuwamwagia fedha za miradi ya afya, elimu na miundombinu na kuwezesha wilaya yao kupiga hatua kimaendeleo.

Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga, aliyasema hayo jana wakati akizungumzia maendeleo yaliyofanyika kwenye wilaya yao iliyoanzishwa mwaka 1905.

Mofuga alisema serikali ya Magufuli imefanikisha maendeleo mengi kwenye sekta mbalimbali ikiwamo ya afya, elimu, miundombinu na mingine.

Alisema serikali imefanikisha ukarabati mkubwa wa vituo vitatu vya afya vya Daudi, Tlawi na Dongobesh na ujenzi wa shule mpya za sekondari na msingi.

Pia serikali imetoa Sh.bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, ambayo inajengwa kwenye Kata ya Dongobesh.

"Tunapaswa kumpongeza Rais John Magufuli kwa mambo mengi, aliyotufanyia wilaya ya Mbulu ikiwemo jengo jipya la makao makuu ya halmashauri linalojengwa Dongobesh," alisema Mofuga.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Hudson Kamoga, alisema pia serikali imewapatia Sh. milioni 230 za madarasa ya shule za sekondari na Sh. milioni 171 za ujenzi wa nyumba ya watumishi wa sekondari ya Yaeda Ampa.

Alisema pia wamepewa Sh. milioni 141 kwa ajili ya Shule ya Sekondari Tumati na Sh. milioni 215 kwa sekondari ya Yaeda Chini na Sh. milioni 66 Sekondari ya Domanga.

Alisema kwenye Shule ya Msingi Mursul wamepatiwa Sh. milioni 46 na ujenzi unaendelea kama kawaida kwani mafundi wapo kazini.

"Kwenye Tarafa ya Dongobesh pekee serikali imetoa fedha Sh. bilioni 7 za ujenzi mbalimbali wa maendeleo, kwakuwa hapa pia ndipo panajengwa makao makuu mapya ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, hatuna budi kushukuru serikali kutuletea maendeleo makubwa na katika nyanja mbalimbali," alisema Kamoga.

Alisema kwenye bwawa la Dongobesh la umwagiliaji kwa kilimo, serikali pia ilitoa Sh. bilioni 2 kwa ajili ya kufanikisha shughuli hiyo.

Alisema Rais Magufuli amefanya mambo mengi ya maendeleo kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu kwa kipindi cha miaka minne tangu achaguliwe, tofauti na viongozi wenzake waliopita.




Mkurugenzi wa Watu na Utamaduni wa kampuni ya Sigara TCC Plc, Angela Mangecha (kulia), akizungumza katika kongamano lijulikanalo kama 'Woman of Influence', lililofanyika jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ushirikishaji wa vijana wahimizwa

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

WATANZANIA wametakiwa kuwathamini na kuwajali vijana, katika kuwashirikisha kwenye fursa mbalimbali zinazopatikana,ili watumie nguvukazi yao kujenga Taifa lenye mazingira mazuri ya biashara na maendeleo.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Shirika linalojihusisha na elimu juu ya utetezi na afya ya uzazi kwa vijana la DSW Tanzania, Peter Owaga, wakati akizungumzia fursa mbalimbali za vijana, katika mkutano uliowashirikisha wadau wa maendeleo mkoani hapa.

Owaga alisema kuwa swala la kuwezesha vijana ni la kila mmoja, kadri atakavyoweza kwani vijana wanahitaji kuwezeshwa katika nyanja mbalimbali, ikiwamo elimu na uwezeshwaji kwa ajili ya kuitendea kazi elimu hiyo.

Alisema shirika hilo limekuwa likitoa elimu juu ya ushawishi na utetezi kwa vijana, pamoja na afya ya uzazi, ambayo imekuwa ikiwasaidia kuondokana na changamoto mbalimbali zinazowakumba.

"Tumekuwa tukiwezesha vijana kupata taarifa sahihi ya afya na huduma rafiki kwa vijana na kuhamasisha vijana kupaza sauti zao, pindi kunapotokea masuala mbalimbali ya unyanyasaji

wa kijinsia, ili yaweze kupatiwa ufumbuzi wa haraka," alisema Owaga.

Jema Mwanuke kutoka kitengo cha dawati la jinsia Kituo cha Polisi Ngaramtoni, alisema wamekuwa wakitatua changamoto nyingi za unyanyasaji wa kijinsia, katika eneo la Ngaramtoni ambapo kwa kipindi cha mwaka jana, kesi mbili ziliripotiwa kuhusu wanaume wanaonyanyaswa na wake zao na kuzipatia ufumbuzi.

Afisa Maendeleo ya Jamii kutoka Halmashauri ya Arusha DC wilayani Arumeru, Getrude Darema, alisema bado kuna haja ya wazazi na walezi kupatiwa elimu kuhusu umuhimu wa kuripoti matukio ya ukatili wa kijinsia wanaofanyiwa watoto wao.

Getrude alisema changamoto iliyopo sasa ni wazazi wengi, kutotoa ushahidi wa kesi za ukatili wa kijinsia pindi zinapofika mahakamani, hivyo kuwa ngumu kushughulikia kesi hizo na baadhi ya watoto wanaofanyiwa ukatili huo, kuogopa toa taarifa kwa kuogopa vitisho wanavyopata.

# Nchi 15 kushiriki maonyesho ya utalii

Na Cynthia Mwilolezi, ARUSHA

NCHI 15 duniani zinatarajiwa kuhudhuria maonyesho ya kimataifa ya sekta ya utalii, yajulikanayo kwa jina la Kili Karibu Fair, yatakayofanyika Juni 7 hadi 9, mwaka huu mkoani hapa.

Aidha katika maonyesho hayo jumla ya waonyeshaji 450 wa masuala ya utalii, kutoka mikoa ya Arusha na Kilimanjaro na baadhi ya nchi zingine duniani watashiriki pia.

Mratibu wa maandalizi ya maonyesho hayo, Dominic Shoo, alisema maonyesho hayo yalikuwa yakifanyika kila mwaka na sasa wameamua kuunganisha mikoa miwili, Ili kutoa nafasi ya kukutanisha zaidi Taasisi na kampuni mbalimbali zinazojihusisha na utalii nchini na nje ya nchi.

"Hii ni katika kutangaza vivutio vya Utalii, kuongeza idadi ya watalii kuja nchini na kuinua mapato kwa taifa, sababu kupitia maonyesho haya watalii wengi wanakuja nchini na tunaingiza kipato na kuitangaza Tanzania," alisema.

Shoo alisema washiriki kwa mwaka huu wameongezeka kwa kiasi kikubwa, kwani idadi ya mwaka huu washiriki ni 450 tofauti na mwaka jana walikuwa 396.

"Ushiriki wa nchi za kigeni zinaisaidia sana nchi kujulikana vivutio vilivyopo na kuinua mapato ya sekta hii ya utalii na taifa," alisema.

Alisema katika sekta hiyo wamefanikiwa kupata watalii wengi kuja nchini kutokana na muunganiko wa matumizi ya mawasiliano kwa mfumo wa Kidigitali, ambao umechangia kwa kiasi kikubwa kuwasiliana na kuwafikia watoa huduma katika sekta hiyo.

Meneja Masoko wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Victor Kitansi, alisema nafasi ya maonyesho hayo yatatoa fursa= kubwa ya watazamaji kuona vivutio vitakavyokuwapo na kuinua sekta hiyo.

"Kuwapo kwa maonyesho haya yataimarisha uhusiano zaidi kati ya Tanzania na nchi zingine, kwani itaongeza idadi ya wageni kutembelea hifadhi kama Serengeti, Manyara, Tarangire na Mlima Kilimanjaro na Tanapa.





Afisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Shinyanga, Tedson Ngwale, akitoa elimu ya kupinga ukatili kwa wanafunzi wa shule ya msingi binafsi ya Little Treasure, iliyopo mjini humo juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Faini ya mifugo inayozurura mitaani juu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

HALMASHAURI ya Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro, imeongeza adhabu ya faini kwa mifugo itakayokamatwa ikizurura mitaani.

Adhabu hiyo imeongezwa kutoka Sh. 5,000 hadi 10,000 kwa kila mbuzi mmoja na kondoo atakayekamatwa, na 10,000 hadi 20,000 kwa kila ng'ombe.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa idara ya Mazingira Manispaa ya Moshi, Danford Kamenya, wakati wa kupanda miti katika Shule ya Sekondari ya Mawenzi, ambapo alisema kwa mifugo ambayo itakamatwa zaidi ya mara mbili, haitaruhusiwa kulipiwa faini na badala yake itapigwa mnada.

Kamenya alisema wameamua kuongeza faini hiyo kudhibiti mifugo ambayo imekuwa ikiachiwa na kuzurura ovyo mitaani na kuharibu miti ambayo imekuwa ikipandwa katika maeneo mbalimbali ya Manispaa hiyo.

"Katika kukabiliana na uharibifu wa miti unaosababishwa na mifugo, Halmashauri imeanza kutumia sheria ya kudhibiti mifugo inayozurura mitaani, na adhabu imeongezwa ili kuhakikisha wananchi wanakuwa waangalifu wa mifugo yao, ili kuepuka faini na kutaifishwa na kupigwa mnada," alisema Kamenya.

Aidha, alisema kwa mwaka huu Halmashauri hiyo inakusudia kupanda miti 500,000, kwa kushirikiana na wananchi na wadau ambapo itajumuisha miti ya matunda ya muda mfupi, ya vivuli na ya asili ambayo itapandwa kwenye msitu wa Rau na kwenye vyanzo vya maji.

Mdau wa mazingira, Said Hashim, alisema sheria pekee haitoshi kudhibiti uharibifu wa mazingira, hivyo kunahitajika kutolewa elimu ya kutosha kwa wananchi ili kuwajengea uelewa na kuwawezesha kutambua umuhimu wa kutunza na kulinda mazingira.

"Mtu kulipa 10,000 au 20,000 mfugo wake mmoja unapokamatwa haitoshi kwa kuwa wapo wanaoharibu mazingira kwa makusudi wakiona jukumu la kulinda ni la watu fulani na serikali, hivyo nashauri elimu itolewe ili kila mmoja aelewe kuwa mazingira ni rafiki kwake na kujituma katika kudhibiti uharibifu," alisema Hashimu.

# Wazazi wakumbushwa jukumu kulinda watoto

**Mary Mosha na Paul William,** SAME

WAZAZI wametakiwa kuhakikisha wanawalinda watoto wa kike dhidi ya mimba za utotoni ili kuwepuka kukatisha masomo yao na kujiharibia ndoto walizojiwekea hali itakayosaidia taifa kupunguza watu tegemezi.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angella Kairuki, alipoendesha harambee ya kuchangia ujenzi wa maabara ya kompyuta katika kituo cha watoto wanaoishi katika mazingira magumu cha Kanisa la Pentekoste Umoja (KPLU), wilayani Same.

Katika harambee hiyo jumla ya Sh. milioni 13.07 zilikusanywa, huku maabara hiyo ambayo itakuwa ni ya kisasa nchini inategemewa kugharimu Sh. milioni 37. Waziri Kairuki alisema suala la mimba kwa wanafunzi wa kike limekuwa tatizo kutokana na kukatisha ndoto za watoto hao na kuwa wapo baadhi ya wazazi wamekuwa wakichangia kutokana na kujisahau katika jukumu la malezi.

"Wilaya ya Same ni miongoni mwa wilaya zinazoongoza kuwa na idadi kubwa ya wanafunzi wanaobeba mimba katika Mkoa wa Kilimanjaro, lakini pia inashika nafasi ya juu Tanzania, nipongeze jitihada zinazofanywa na Wizara za Elimu, Tamisemi pamoja na juhudi za mkuu wa wilaya kupunguza mimba hizo," alisema Kairuki.

Waziri huyo alitoa rai kwa wazazi kuona umuhimu wa kuhakikisha wanawalinda watoto na kuwathamini waweze kutambuliwa kuwa wanahitaji kusoma mpaka hapo watakapomaliza elimu yao na sio kukatiza masomo yao.

Waziri Kairuki alisema kuwa kituo hicho kimeamua kuwajengea uwezo wa kuwa na ujuzi wa sayansi na teknolojia kupitia kompyuta ambapo kwa sasa soko la ajira uelewa wa Tehama una mchango mkubwa na katika ushindani, na kuwa mtu anayeelewa Tehama ana nafasi kubwa ya kupata ajira.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema kuwapo kwa maabara za kompyuta kutasaidia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi wilayani kwa kuwaongezea maarifa zaidi ya kile walichofundishwa na walimu.

Kuhusu mimba za utotoni, Senyamule alisema tatizo la utoro limepungua ambapo hadi kufikia mwishoni mwa Machi mwaka huu, kulikuwa na mimba 10, huku takwimu zikionyesha kuwa mwaka juzi wilaya hiyo ilifunga mwaka ikiwa na mimba 95 na mwaka jana walifunga wakiwa na mimba 28. Alisema kuwa, kwa mwaka huu idadi hiyo itapungua kutokana na hatua mbalimbali zinazochukuliwa, na sasa Mahakama wilayani Same imewahukumu watu wanne miaka 30 jela waliothibitika kuwapa ujauzito wanafunzi.

# Wajasiriamali wapewa neno

**Na Mary Mosha,** MWANGA

MKUU wa Wilaya ya Mwanga, Thomas Apson, amekitaka kikundi cha ujasiriamali cha ngozi kuwa na ubunifu na kuzalisha bidhaa zenye manufaa ya kuendeleza viwanda, ili ziweze kuwa na uwezo wa ushindani katika soko la ndani na nje ya nchi.

Apson aliyasema hayo wakati wa utiaji sahihi kati ya Costech, Shirika la Viwanda Vidogo (sido), Halmashauri ya wilaya ya Mwanga na kongano la ngozi la Usangi katika mradi uliodhaminiwa wa Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Sweden (Sida) kupitia na Sida.

Alisema kongano 55 nchini zilishindanishwa na kupatikana kongano 15 ambapo moja ilipatikana Kilimanjaro katika Wilaya ya Mwanga.

Alisema ni matarijio yake kuona wadau wote wakishirikiana katika mradi huo na kufanikiwa kunyanyua viwanda vidogo hususan vinavyoundwa na vikundi.

Alisema Sido na Costech wanapaswa kushirikiana ili kuendeleza mradi huo kikamilifu pamoja na kuunga mkono juhudi za serikali za kuanzisha na kuendeleza viwanda.

Katibu wa kikundi cha wajasiriamali wa ngozi (kiwango), Amir Mshana, alisema amefurahishwa na utiaji sahihi mkataba huo na kusema mchakato wa kupata ufadhili huo umechukua muda mrefu.

Aliomba serikali kusimamia vyema msaada wa mashine za uchakataji wa ngozi ambazo vitafungwa kwa ufadhili wa Sida kupitia sido.

Alisema kikundi hicho kinachakata ngozi kwa kutumia njia za asili na kwamba wangekuwa na mashine uzalishani ungekuwa wenye ubora zaidi na wa kisasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashari ya Mwanga, Zefrin Lubuva, alisema atashirikiana na kikundi hicho kuhakikisha mpango wa maendeleo ya biashara katika kunyanyua uchumi wa mtu mmoja na taifa kwa ujumla.

ama
ALHAMISI MEI 9, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 16

**Mkurugenzi Kinga, WHO wasimulia chanjo inavyonusuru watoto kufa**



Ukurasa 19

Kamanda Muslimu: Nimepunguza ajali, shida barabarani bado rushwa



Ukurasa 17

**'Mubashara' kuhusu homa ya manjano, chanjo yake**




# TIBA KWA MIONZI YA NYUKILIA

Ukurasa 14

# UN: Wanyama milioni hatarini kutoweka

**Mwandishi Wetu**

UMOJA wa Mataifa (UN), umeripoti kwamba kuna hatari ya takriban aina ya wanyama milioni moja kutoweka duniani, kutokana na uharibifu wa mazingira unaofanywa na wanadamu.

Uharibifu huo unaelezwa kufanyika kuanzia anga za angani, ardhini na majini, huku aina nyingi ya mimea nayo haiko salama.

Ripoti hiyo inagusa mfano wa nyuki walio muhimu katika ustawi wa vyakula, hadi misitu iko katika kasi kubwa ya kuteketezwa na binadamu.

Sababu mojawapo inatajwa kuwa watu duniani wameongezeka zaidi ya mara 10, kulinganisha na waliokuwapo mwaka 1970.

Katika hilo, inaelezwa haja ya mahitaji kama mavazi, mlo, na nishati wanaangukia katika kuteketeza mahitaji muhimu ya kimazingira.

Inaelezwa, kati ya mwaka 1980 na 2000, kuna jumla ya hekta milioni 100 za misitu ziliteketezwa hasa ikitajwa ukanda wa Amerika ya Kusin na Kusini Mashariki ya Asia.

Hadi sasa, kunaelezwa kilichopo katika msitu ni asilimia 13 tu ya kilichokuwapo mwaka hadi mwaka 2000, huku mijini ndiko kwenye uteketezaji una hali ya kutisha.



Uteketezaji misitu ukiendelea. **PICHA: MTANDAO.**

AFYA

# TIBA KWA MIONZI YA NYUKILIA

- Ocean Road yahudumia 2000 kwa mwaka
- Kitaifa wataalamu 5, Bugando nayo imeanza
- Tiba kuu; saratani, moyo, figo, tezi,ubongo



Mtaalamu wa Tiba ya mionzi wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Dk. Faraji Sabaya, akimuandaa mgonjwa kwa ajili ya uchunguzi. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Veronica Romwald**

MIONZI ya nyuklia inajulikana kutumiwa katika nchi nyingi zilizoendelea duniani, katika utengenezaji wa vilipuzi na mabomu, ambayo ni maalum wakati wa vita.

Inafahamika kwamba, mionzi ya nyuklia ni hatari zaidi kuliko mingine duniani. Hata hivyo, cha kushangaza ni kwamba kuna hatua ya kitaalamu ambayo mionzi inatumika katika namna mbadala ya matibabu ya magonjwa mbalimbali.

Nchini hivi sasa kuna huduma za uchunguzi na matibabu dhidi ya magonjwa ya saratani, ambayo kwa miaka 20 sasa inatumia mionzi hiyo.

> **Ni kama unavyoona kichupa chenye dawa ya quinine, mtu hupatiwa kwa njia ya dripu au kupitia mishipa yake.**

**DAKTARI BINGWA**

Hivi karibuni Nipashe ilizunguza na daktari bingwa wa kutibu na kuchunguza magonjwa mbalimbali kwa kutumia mionzi ya nyuklia, kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), Tausi Maftah, anasema taasisi hiyo ni ya kwanza nchini kuanza kutoa matibabu ya aina hiyo.

Anasema, kutokana na manufaa ya huduma hiyo ya uchunguzi na matibabu, serikali imeianzisha katika Hospitali ya Bugando mkoani Mwanza na kwamba inakusudia kuanzisha katika hospitali zake zingine za kanda.

"Watu wengi duniani wamezoea mionzi hii inatumika kutengeneza vilipuzi na mionzi. Ni kweli, lakini sasa watambue kwamba mionzi hii ipo aina nyingi tofauti na inaweza kutumika kwa tiba," anabainisha.

Dk. Tausi anasema ORCI tunaitumia mionzi hiyo kuchunguza, kutibu na tunaweza kushauri aina ya matibabu ya kumpatia mgonjwa husika.

"Kwa sababu, pamoja na kwamba sisi tunachunguza na kutibu saratani, lakini kwa kutumia mionzi hii, tuna uwezo wa kuchunguza magonjwa mengine ya ubongo, moyo, tezi ya thyroid (goita), figo, mfumo wa uchujaji wa 'lymph' (kwa wanaovimba miguu na kupata matende), mfumo wa endokraim.

"Tunaweza pia, kuchunguza mfumo wa nyongo na ini kwa ujumla utendaji kazi wake, lakini pia kwa watoto waliozaliwa na tatizo la kuziba kwa mfumo wa nyonga na magonjwa mengineyo.

"Kwa kutumia uchunguzi huo, tunaweza kushauri aina ya matibabu ya mgonjwa husika, ili kupata matokeo mazuri, mionzi hii inatibu saratani na magonjwa mengine pia," anafafanua.

**MIFUMO YA MIONZI**

Dk. Tausi mionzi hiyo ipo ya aina mbili, kwamba ipo ile ya asili na ipo ya kutengeneza kiwandani na kwamba mionzi wanayotumia kwa matibabu ni ile inayotengenezwa kiwandani.

"Hutengenezwa kwa mitambo maalum na kuhifadhiwa kwenye mfumo maalum viwandani, Tanzania huwa tunaagiza kutoka Afrika Kusini na Uturuki. Nchi zingine ambazo zinatengeneza ni Australia, Ufaransa, Marekani na Uingereza.

"ORCI tunachukua Afrika Kusini na Bugando (Mwanza) wao wanachukua huko Uturuki, huwa inatengenezwa katika mifumo tofauti ili tuweze kumpatia binadamu," anasema.

"Mionzi huwa katika mfumo ambao mtu hupatiwa kwa kumulikwa kwa mfano 'X-xays' yaani anaingizwa mahala anamulikwa na kutakiwa kutoka nje kwamba matibabu tayari.

"Mionzi ya nyuklia yenyewe ipo katika mfumo wa tofauti, ipo kama dawa (kidonge) au mtu hupatiwa kwa njia ya sindano kupitia mishipa yake ya damu," anabainisha.

Anaongeza: "Ni kama unavyoona kichupa chenye dawa ya quinine, mtu hupatiwa kwa njia ya dripu au kupitia mishipa yake."

Mtaalamu huyo anasema, uagizaji wake unapaswa kupata kibali kutoka Tume ya Nguvu za Atomiki (TAIC). Anaongeza: "Hawa ndiyo wanaratibu shughuli zote za mionzi Tanzania na ndiyo wanaotoa kibali cha kuagiza na kuingiza mionzi nchini.

"Na si kila mtu anaweza kuingiza mionzi hiyo, lazima naye atambulike kwamba anao ujuzi wa 'kuhandle' (kusimamia) mionzi hiyo na anapatiwa leseni na tume hiyo, wafanyakazi wa ORCI wa kitengo hiki tuna kibali."

**ODA ZINAVYOFANYWA**

Daktari huyo anasema kabla ya mionzi hiyo kuagizwa, mgonjwa hufanyiwa vipimo vyote muhimu kwani mionzi hiyo, huagizwa kwa oda maalum kutoka kiwandani.

AFYA

# TIBA KWA MIONZI YA NYUKILIA

"Lazima, tujue atahitaji kiwango gani cha mionzi kukamilisha tiba yake, ndipo tunatuma taarifa kiwandani na kuagiza kiwango kinachohitajika.

"Wataitengeneza kulingana na taarifa tuliyowatumia, iwapo tunahitaji mionzi ya kidonge au ya sindano katika matibabu ya mgonjwa wetu," anafafanua.

Kwa mujibu Dk. Tausi, mionzi hiyo husafirishwa kwa njia ya anga na kwamba huwa inahifadhiwa katika ustadi wa kipekee, ili kulinda ubora wake.

"Inakuwa imehifadhiwa katika chuma maalum kinaitwa kitaalamu 'lead shield' (anaionyeshaa). Ni chuma kizito ambacho kwa jinsi kilivyotengenezwa huilinda na kuizuia ile mionzi kutoka nje.

"Inafungwa, inasafirishwa, ikifikishwa, tuna kibali maalum ambacho tumepewa na tume na leseni hiyo inaonyesha kiwango gani cha mionzi tunapaswa kuagiza kuingiza nchini.

"Mionzi hii huwa ina tabia ya kuisha nguvu tofauti kabisa na dawa zingine za kawaida, hii kadiri inavyokaa nikiwa na dawa sasa hivi baada ya saa moja inaisha nguvu, iwe imefunguliwa au la," anasimulia.



Mtaalamu bingwa, Dk. Tausi Maftah, wa Taasisi ya Saratani Ocean Road (ORCI), akifafanua jambo kuhusu tiba ya nyuklia. **PICHA ZOTE: VERONICA ROMWALD.**

### INACHUNGUZWAJE?

"Wakati inaisha nguvu, inatoa mionzi. Unatafuta iwe 'stable' (imara) kwa sababu inakuwa ipo 'unstable' (haipo imara), zile 'radiation' (mionzi) inapotoa, ndipo tunazitumia kuchunguza. Lazima tuiwahi, kwani ikiwa 'stable' hatuwezi kuchunguza tena.

"Inatoa 'radiation' (mionzi) tofauti ambazo tunachukua na kumuweka mgonjwa. Sisi tunampatia mgonjwa na anakuwa na ile mionzi anatoa. Tunamuweka kwenye kamera ambayo ina uwezo wa kuiona ile mionzi inavyoenda mwilini na sisi tunatumia 'screen' maalum kuchunguza.

"Hizi ni radiation ambazo zinatumika duniani. Kwa wale waliosoma sayansi wanafahamu kitu kinaitwa 'periodic table.' Ndiyo hizo tunatumia. Ni Physics (Fizikia) na Chemistry (Kemia) fulani zinatumika, ni radiation ambazo zipo duniani," anabainisha.

### KINACHOFANYIKA

Dk. Tausi anasema, iwapo wanampokea mgonjwa, wanajua mionzi inayofaa kwa matibabu au uchunguzi dhidi ya ugonjwa unaomkabili.

Anasema huwa wanaangalia tabia ya ufanyaji kazi wa hicho kiungo na si maumbile, viungo vinafanya kazi na kwa jinsi zinavyofanya kazi kwa mfumo maalum, kulingana na jinsi zilivyoumwa.

"Kwa mfano, moyo kazi ni kusukuma damu lakini ili isukume inahitaji msukumo fulani, kuna vimelea vimeumbwa kufanya kazi hiyo. Sisi tunachukua dawa ambayo ina tabia sawa na zile chembe chembe tunachanganya na mionzi.

"Zitakwenda moja kwa moja kwenye moyo na hivyo tunaanza kuuchunguza ule moyo wake. vivyo hivyo, kwa viungo vingine vya mwili, ikiwamo figo ambayo kazi yake ni kuchuja taka mwilini zitoke kwa njia ya mkojo.

> "Kwa mfano, huduma ya upandikizaji figo imeanza nchini, kabla ya kufanya matibabu hayo lazima mtoa figo achunguzwe afya ya figo yake kabla ya kuitoa, hivyo wanakuja hapa.




Kifaa kinachotumika kuhifadhi mionzi ya nyuklia.

"Tunachukua dawa maalum tunaichanganya na mionzi ambayo itapita katika njia ile ile hadi kwenye figo na tutajua wapi penye tatizo," anasema Dk. Tausi.

"Hata katika mfumo wa chakula ni hivyo hivyo. Tunachukua dawa maalum zenye tabia sawa na chembe chembe za tumbo na kuichanganya na ile mionzi tutaweza kujua penye tatizo," anabainisha.

Anaongeza; "Hata tunavyochunguza tezi ya 'Thyoid' tunajua aina ya vichocheo vinavyoifanya ifanye kazi yake sawa sawa. Tezi hii husimamia ile 'metabolism' ya mwili, ubongo ufanye nini, chakula kisagwe namna gani, macho yaangalie nini yaani ile jinsi ya ufanyaji kazi ya mwili mzima.

"Tunajua jinsi ya kufanya na hivyo kuifikia tezi hiyo na kuichunguza kwa kutumia mionzi hii na inatuwezesha kujua kama ina tatizo au la," anasema.

### RUFANI KWA MAELFU

Anasema kila mwaka wanapokea, kuwachunguza na kuwatibu wagonjwa 2000 wenye magonjwa mbalimbali.

"Awali wataalamu wengi hawakujua kuhusu kitengo hiki, lakini sasa kuna mwamko, kwani serikali imeazimia kupunguza rufani za wagonjwa kwenda nje ya nchi. Kwa vipimo vinavyohitaji uchunguzi kwa kutumia mionzi ya nyuklia, inabidi wawalete huku ORCI.

"Kwa mfano, huduma ya upandikizaji figo imeanza nchini, kabla ya kufanya matibabu hayo lazima mtoa figo achunguzwe afya ya figo yake kabla ya kuitoa, hivyo wanakuja hapa.

"Hata wagonjwa wa moyo wanaletwa huku hasa kwa wale ambao wanahitaji kipimo hiki cha mionzi ya nyuklia," anabainisha.

### CHANGAMOTO

Bingwa huyo anasema, hadi sasa wataalamu wenye uwezo wa kutoa matibabu hayo nchini ni wachache na kwamba wananchi wengi hawajui kama kuna huduma hiyo, inayotolewa ORCI.

"Tupo watano nchi nzima. Sasa hivi serikali inasisitiza tupanue huduma za afya na tusipeleke wagonjwa nje ya nchi.

"Hivyo kuna mwamko wa kufanya uchunguzi kwa makini tatizo linalomsumbua mgonjwa. Sasa hivi wataalamu wanaamka na kutafuta huduma ya 'nyuklia scan' ilipo, hivyo wanaleta wagonjwa," anabainisha.

AFYA

# Mkurugenzi Kinga, WHO wasimulia chanjo inavyonusuru watoto kufa

- Surua, Rubella pacha, tofauti yao janga hili...
- Zijue balaa zinazomuanzia mtoto tumboni

**Na Yasmine Protace**

NI swali la msingi kujiuliza, chanjo ni nini na ina nafasi gani kiafya? Katika ufafanuzi wa kawaida, inatafsiriwa kuwa maandalizi ya kibaiolojia yanayotoa kinga ya mwili dhidi ya baadhi magonjwa kwa binadamu.'

Chanjo, ambayo kitalamu au lugha ya kiingereza inaitwa 'vaccine, inaelezwa kuwa njia bora zaidi kuzuia magonjwa ya kuambukiza. Kinga inayoenea kutokana na chanjo kwa kiasi kikubwa, inawezesha kuepuka maradhi kama kifua kikuu, polio, pepopunda na tetekuwanga.

Inashauriwa na madaktari, kwamba, watoto wadogo wapewe chanjo, ili iwakinge dhidi ya magonjwa na maradhi mabaya, kupitia dhana na nadharia "Kinga ni bora kuliko tiba."

Hivyo, kiafya jamii zimekuwa zikihamasishwa kuwapeleka watoto kliniki walio na umri wa kuudhuria kliniki, lengo ni kuwawezesha wasidhurike na magonjwa ya kuambukiza.

Ni sababu mojawapo inayoifanya serikali, mara tu mtoto anapozaliwa anaingizwa katika mipango na michakato ya kupatiwa chanjo za kinga.

Pamoja na serikali kutumia gharama kubwa kununua chanjo kwa ajili ya usalama wa watoto wasipate magonjwa, kuna baadhi ya wazazi bado hawawapeleki watoto kliniki kupata chanjo, kutokana na sababu mbalimbali, inayoangukia katika uelewa duni kuhusu manufaa hayo.

Ndiyo mana kuna mazingira ambayo hushuhudiwa sheria, elimu na uhamasishaji unafanyika kufanikisha.

### MPANGO WA CHANJO

Mpango wa Taifa wa Chanjo ulianza nchini mwaka 1975. Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kinga na Meneja wa Mpango wa Taifa wa Chanjo wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Dafrossa Lyimo, ana ufafanuzi wa hatua zinazochukuliwa kuhusu chanjo na kinga.

Wizara hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine, wakiwamo Shirika la Afya Duniani (WHO), wana ufafanuzi na elimu kuhusu hatua nchini zinazohusu chanjo na kinga.

"Tanzania walianza kutoa chanjo aina tano pekee, lakini mpaka kufikia sasa imevuka hatua na kufikia kutoka aina 15 za chanjo," anaeleza Dk. Dafrosa, akifafanua mpaka sasa kuna magonjwa 13 yanayozuilika kupitia chanjo hizo, hali inayonufaisha serikali, pia kupunguzia gharama za kutibu kitaifa.

Anasema, mikakati ya chanjo inaongozwa kidunia, mtazamo ukilenga kuwafikia watoto wote kwa usawa bila ya kuangalia umbali au mahali waliko.



Uzinduzi wa moja ya Wiki ya Chanjo wilayani Bagamoyo. **PICHA: MTANDAO**

> **wazazi, wanapaswa kufuata ratiba za kuwapeleka watoto kliniki kupata huduma, pia huduma za 'mkoba' zinatolewa na wauguzi wa vijijini.**



Waandishi wa habari mbalimbali wakifuatilia mafunzo yanayohusu chanjo, yaliyoandaliwa kwa pamoja na wizara inayohusika na afya na WHO. **PICHA ZOTE: YASMINE PROTACE.**

Dk. Dafrosa anataja mkakati mwingine ni kupunguza magonjwa yanayozuilika, huku akiainisha kwa kauli:"Tanzania inatoa chanjo tisa ambazo zinazuia magonjwa 13."

Anasema kuwa watu wakipewa chanjo ya surua, inapunguza vifo milioni 10.6 kwa mwaka duniani na anataja magonjwa yaliyoko katika mkakati wa kupunguzwa na kutokomezwa kuwa ni pamoja na polio, surua na Rubela.

### KLINIKI MUHIMU

Pia, anasema mkakati wa serikali unalenga kuwafikia watoto bila ya kubagua ili jamii iwapeleke watoto kliniki, kuanzia anapozaliwa hadi kufikisha umri wa miaka mitano.

Anasema wazazi, wanapaswa kufuata ratiba za kuwapeleka watoto kliniki kupata huduma, pia huduma za 'mkoba' zinatolewa na wauguzi wa vijijini.

Dk. Dafrosa anasema, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inasisitiza wazazi kuhakikisha watoto wao wanapata chanjo zote zinazotakiwa kwa wakati ili waepukane na magonjwa mbalimbali.

Akielezea magonjwa ya surua na rubella, ni kwamba yanafafana, lakini rubella athari yake kwa kinamama wanaoshika ujauzito, madhara yake ni mtoto atakayezaliwa hupata shida ya ini, anaweza kuwa na tundu kwenye moyo, figo na maeneo mengine.

"Surua na rubella dalili zake zinafanana kwa karibu sana. Unaweza kuja na dalili za surua, lakini mpaka ufanye vipimo kwa karibu sana, ndio unakuta ni Rubella, lakini chanjo zake ni moja," anachambua Dk. Dafrossa.

Kuhusu ugonjwa wa polio, anabainisha hatari yake ni kwamba kutoka kwa mtu mmoja anayeumwa, anaweza kuwaambukiza watu zaidi ya 200, ndio sababu wanahamasisha haja ya watu kupata chanjo, ili kuepuka matatizo hayo.

"Mtu akikuletea kidonge akikuambia chanjo, hiyo sio chanjo. Hiyo ni kinga tiba na unaweza kunywa muda wowote, mfano dawa ya kinga ya minyoo au mabusha, hiyo haina ratiba kila mwaka unakunywa, ya kwetu chanjo ina muda maalum," anaeleza Dk. Dafrossa.

Rai yake ni kwamba, wanajamii wanapaswa kumaliza dozi za kinga kwa wakati, wakifuata ratiba watakazowekewa na watalaamu.

Dk. Dafrossa anaifahamisha jamii kwamba, chanjo ni haki ya kila mtoto, hivyo wanapaswa wapeleke kwenye vituo vya kutolea huduma za afya, wakapate chanjo.

Anasema nafasi yake kiafya kwamba zinachangia kuokoa maisha ya wengi. Kaulimbiu ya mwaka huu: "Chanjo ni kinga, kwa pamoja tuwakinge."



Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kinga na Meneja wa Mpango wa Taifa Chanjo, kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Dafrossa Lyimo, akizungumzia jambo na waandishi wa Habari (hawapo pichani).

### MWAKILISHI WHO

Mwakilishi wa WHO na mtalaamu wa Chanjo, Dk. William Mwengee, anasema Tanzania imepiga hatua katika masuala ya chanjo, kwa kuhakikisha zinafika kwa wakati katika maeneo yote, pasipo kuwapo changamoto kama za usafiri au kifedha, ikiliganishwa na nchi zingine.

> **Surua na rubella dalili zake zinafanana kwa karibu sana. Unaweza kuja na dalili za surua, lakini mpaka ufanye vipimo kwa karibu sana.**

Dk. Mwengee, anasema Tanzania iko katika nchi zinazochukua hatua kufanikisha kuwepo chanjo kwa maradhi yanayozuilika yanadhibitiwa.

Anasema, hilo linathibitika hata kwa watoto wote wanaozaliwa hospitalini au nje ya hospitali, ikitoa ishara ya ufanikishaji kwa kiwango kikubwa.

"Magonjwa yanayozuilika ya chanjo, yanaua, tena yanaua kwa kiwango kikubwa sana. Hivyo tunao wajibu wa kutumia kalamu zetu (wanahabari) kupaza sauti juu ya watu wakapate chanjo" anaeleza Dk. Mwangee.

Kila mwezi wa Nne ni Wiki ya Chanjo Barani Afrika. Dhana yake ni kuitaka jamii ya Kiafrika, kama walivyo wenzao duniani, kuhakikisha wanakamilisha, ambayo ni kinga kwa watoto dhidi ya maradhi hatari kama vile polio, surua, rubella, kuhara, donda koo, kifaduro, pepopunda, homa ya ini, kifua kikuu, homa ya uti wa mgongo, na niumonia.

Wataalamu hao wameshaweka wazi kuwa, mtoto asiyepata chanjo, yuko katika hatari ya maisha yake na jamii inayomzunguka, kwa sababu anaweza kuambukizwa magonjwa na yeye kuambukiza wengine.

## 'Mubashara' kuhusu homa ya manjano, chanjo

HOMA ya manjano ni nini? Huo ni ugonjwa wa ini unaosababishwa na kirusi kinachoitwa 'Homa ya Manjano A' (HAV), kinachoambaa kutoka mtu mmoja hadi mtu mwingine kwa njia ya kugusana na walioathiriwa.

Pia, kuna uambukizaji kupitia vyakula, maji au vitu vyenye HAV. Dalili zake ni zifuatazo: Homa, uchovu, kukosa hamu ya chakula, kichefuchefu, kutapika; maumivu ya viungo na maumivu makali tumboni; kuharisha,hasa kwa watoto; kuwa na ngozi ya njano; mkojo mweusi na choo cha rangi ya udongo.


Ni kawaida dalili hizo huonekana kati ya wiki mbili na sita na mtu anapotibiwa hupotea ndani ya miezi 2, ingawa kuna watu wanaodumu nazo kwa miezi sita. Ikiwa una homa ya manjano 'A' anaweza kuwa nguvu za kuifanya kazi, huku kuna watoto wasioonyesha dalili, tofauti na wakubwa wanaonyesha kuathirika mara zote.

Unaweza kusambaza HAV bila ya kuwa na dalili? Homa ya manjano inasababisha matatizo ya ini na kifo.

### CHANJO YAKE

Chanjo ya Homa ya Manjano A ni ile isiyo hai (iliyouliwa). Mtu anahitaji dozi mbili kwa kinga ya kudumu ya muda mrefu.

Dozi hizo zinapaswa kutolewa katika ndani ya miezi sita.Watoto hupewa kila mara, kutoka siku ya kwanza anapozaliwa na siku ya pili, hadi umri miezi 12 hadi miezi 23.



Mgonjwa homa ya manjano na matibabu yake. **PICHA: MTANDAO**

Watoto wakubwa na vijana wanaweza kupewa chanjo baada ya miezi 23. Watu wazima, ambao awali hawakupatiwa chanjo, wanahitaji kulindwa dhidi ya homa ya manjano kupitia chanjo.

Kwa wanaosafiri kwenda mbali katika nchi ambazo kuna mikasa ya homa ya manjano A, wanapatiwa kinga dhidi ya binadamu na mifugo walioathiriwa.

Baadhi ya watu wana mzio (aleji) dhidi ya chanjo hizo, hivyo wanapopatiwa inatishia maisha yao. Wanashauriwa wasipokee chanjo, bali kumfahamisha mtoa chanjo kwa maelekezo au ushauri zaidi.

Pia, kuna baadhi ya watu wasiokula vizuri au wana hali duni kiafya, nao wanashauriwa kuahirisha chanjo na anapata maelekezo zaidi ya kiafya kutoka kwa daktari.

Ingawaje, katika upande wa pili wapo baadhi katika hali hizo za kiafya hupata madhara ya muda mfupi na yanaopotea yenyewe.

### MADHARA MADOGO

Matatizo yasiyo makubwa baada mtu kupokea chanjo, ni pamoja na maumivu au wekundu kwenye sehemu iliyodungwa sindano (kwa wenye ngozi nyeupe), maumivu ya kichwa, uchovu baaada ya kupokea sindano kwa muda wa siku moja hadi mbili.

Kuna watu kulingana na hali zao, huzimia baada ya utaratibu wa chanjo. Inaelezwa mtu akiketi au kulala chini kwa takriban dakika 15, kunamsaidia asizirai.

Hapo ni vyema mtu akihisi kizunguzungu baada ya chanjo, amfahamishe daktari wake kwa namna anavyoona au kuhisi kelele katika masikio.

Baadhi ya watu hupata maumivu makali begani yanayodumu muda mrefu, kutokana na sindano. Hata hivyo, yanatajwa kuwa matukio nadra. Katika kanuni za kitabibu kimataifa, usalama wa chanjo unafuatiliwa sana wakati wote.

### KINGA YA UGONJWA WA MANJANO

- Kupatiwa chanjo ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu.
- Kutumia kinga wakati wa kujamiiana
- Kuacha kuchangia vitu vyenye ncha kali kama sindano, wembe n.k
- Kutochangia mswaki
- Kuwa na mpenzi mmoja mwaminifu
- Kuto ongezewa damu ambayo haijapimwa na kuthibitika kuwa salama.
- Makala hii ni kwa mujibu wa taarifa za Idara ya Huduma za Kinga ya Afya ya Marekani na mitandao. **BBC.**

AFYA

# MEI 5 – 12; WIKI YA KIMATAIFA YA USALAMA BARABARANI

• Wagonjwa MOI 75% majeruhi bodaboda • Kila mwezi wagonjwa wapya wa ajali 500 • Ajali muuaji Na. 8; mwendokasi, ulevi tatizo



Ajali ya pikipiki. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Na Veronica Romwald**

MIAKA 11 sasa imetimia tangu serikali iliporuhusu usafiri wa pikipiki za miguu miwili na zile za miguu mitatu (Bajaji), kuanza kutumika kama vyombo vya usafiri rasmi mwaka 2008.

Usafiri huo ulianza taratibu katika maeneo ya mijini na kujizolea umaarufu mkubwa hata 'ukabatizwa' kwa jina la bodaboda, kwa namna madereva wake wanapenya katika maeneo mbalimbali kwa haraka.

Lakini mwanzo huo umetanguliwa na kuwapo usafiri huo katika mkoa wa Kagera, ukiwa na jina hilo hilo la bodaboda, ambalo mzizi wake ni kati nchi jirani ya Uganda, ambako jijini Kampala ni wa miaka nenda rudi.

Watu wengi hupenda kuutumia usafiri huo, kwani ni gharama nafuu zaidi ya teksi na madereva hao hupenya, hata kunapokuwapo na foleni kubwa, hivyo wanaweza kuwahi waendako na kwa sasa kundi kubwa la vijana limeajiriwa na wengine kujiajiri katika shughuli hiyo nchini kote.

**MAJERUHI MOI**

Waziri wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi. Hamad Yussuf Masauni Novemba mwaka jana, alinukuliwa akisema katika kipindi cha miaka 10, vyombo vya usafiri vimesababisha jumla ya majeruhi 38,237 na vifo 8,237.

Takwimu za Taasisi ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) mwaka 2016 zinaonyesha walipokea majeruhi 3,273 waliotokana na ajali za bodaboda.

Kati yao, madereva walikuwa 1,799 na abiria walikuwa 992 na watembea kwa miguu waliogongwa na bodaboda walikuwa 482.

Mwaka 2017; kulikuwapo majeruhi 3,467 kati yao madereva 1,486 na abiria 1,120 na watembea kwa miguu, waliogongwa na bodaboda 861.

Mkurugenzi wa MOI, Dk. Respicious Boniface, anasema tathmini inaonyesha kila mwezi wanapokea kati ya majeruhi 400 hadi 500, waliotokana na ajali mbalimbali.

"Asilimia 75 ya wagonjwa wanaokabiliwa na matatizo ya ubongo, mgongo na mishipa ya fahamu tunaowahudumia hapa MOI wanatokana na ajali mbalimbali hasa za barabarani, bodaboda," anasema.

> **Unakuta kabisa taa nyekundu imewaka ambayo kimsingi mtu anapaswa kusimama, lakini bodaboda anakatisha na kupita kwa lazima.**



Safari za pikipiki zinavyofanyika kwa hatari.

**VYANZO HATARISHI**

Shirika la Afya Duniani (WHO), inataja vyanzo hatarishi vitano vya ajali za barabarani inajumuisha mwendokasi, ulevi, kutokuvaa kofia ngumu kwa pikipiki, kutokufunga mkanda na kutoweka vizuizi vya watoto katika magari.

Nipashe ilizungumza na baadhi ya madereva wa bodaboda na abiria jijini la Dar es Salaam, waliobainisha mambo matano yanayochangia kuwapo changamoto hiyo ya ajali.

John Kisabo, ni dereva wa bodaboda, eneo la Mbezi, anayeasema madereva wengi wa bodaboda na bajaji, wamejifunzia kazi hiyo mtaani, kisha wanaingia barabarani.

"Mimi pia nilikuwa miongoni mwao, nilijifunza mtaani nikaingia kazini, niliendesha kwa kipindi cha mwaka mmoja, ndipo nikaenda chuo kujifunza ili nipate leseni niweze kuendesha hadi maeneo ya katikati ya mji," anasema, akiongeza kuwa aliwahi kupata ajali mara kadhaa na akalazwa hospitali.

Mussa Elius, ni dereva wa bodaboda eneo la Ubungo, anasema tamaa ya kutaka kuwahi kufika wanakopeleka wateja ili kupata fedha zaidi, inachochea ajali za barabarani.

"Ulevi nao ni kisababishi. Unakuta baadhi ya madereva wenzetu wanakuja kazini wakiwa tayari wamelewa," anasema.

Israel Elius, dereva wa Bajaji, Sinza Kijiweni, anasema jingine linalochangia ajali za barabarani kwa bodaboda na bajaji, ni kutotii sheria za usalama barabarani.

"Nadhani hili linachangiwa zaidi na wengi kuingia kazini pasipo kwenda chuoni kufundishwa hasa hizi alama. Unakuta kabisa taa nyekundu imewaka ambayo kimsingi mtu anapaswa kusimama, lakini bodaboda anakatisha na kupita kwa lazima.

"Sasa kwa hali ile mara nyingi unakuta ajali zinatokea katikati ya barabara, watu wanaumia, wanavunjika, wamejazana hospitalini ni hatari kwa kweli," anasema.

INAENDELEA UK.20

AFYA

## MEI 5 – 12; WIKI USALAMA BARABARANI

# Kamanda Muslimu: Nimepunguza ajali, shida barabarani bado rushwa

• Rasmi kufa nayo 'mguu kwa mguu' • Aiita kero 2; miezi 6 afuta nusu ajali

**Na Margaret Malisa,** aliyekuwa Dodoma



Ajali ambazo zimekuwa adha kubwa kwa usalama barabarani na utendaji wa askari kwa jumla. **PICHA: MTANDAO.**

"VITENDO vya rushwa, ndio vinaninyima usingizi kwa sasa. Hiyo ndio kero yangu namba mbili, "anatamka Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP) Fortunatus Muslimu

Anaendelea: "Lakini tayari nimekwishatafuta muorobaini wake wa kutokomeza kabisa rushwa barabarani. Kero ya kwanza ilikuwa ni ajali za barabarani, ambazo tumepunguza kwa kiasi kikubwa."

SACP Muslimu, alitamka hayo alipohojiwa na Nipashe mjini Dodoma, tarehe 17 Aprili mwaka huu, kupata ufafanuzi wa hali halisi ya ajali za barabarani, mikakati yake, mafanikio na vikwazo kuhusu anavyokutana navyo.

Hiyo ilikuwa katika hafla ya kufunga mafunzo ya wanahabri 17 waliopatiwa mafunzo ya zaidi miezi sita kuripoti habari za usalama barabarani, kwa ufadhili wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Kamati ya Blumberg.

### AJALI NCHINI

Kamanda SACP Muslimu, anasema ajali zimepungua kutoka 22, 739 mwaka 2009 hadi 3,746 za mwaka 2018, ikiwa ni mafanikio yatokanayo na ushirikiano kati ya Polisi na serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Afya, Jinsia, Wazee na Watoto.

Anasema WHO, Tamwa na Kamati ya Blumberg, kwa kiasi kikubwa wanatoa mchango wao wa hali na mali, kuhakikisha ajali zinapungua, huku wakitoa mafunzo kwa wanahabari, kuhusu namna ya kuandika habari za usalama barabarani.

"Tukizungumzia Aprili 16 (siku moja kabla ya mazungumzo na mwandishi), kwa saa 24 ni ajali tatu tu zimetokea nchi nzima," anasema SACP Muslimu na kuongeza:

"Hali haikuwa kawaida kama hapo awali. Sina budi kuwapongeza wadau mbalimbali tulioshirikiana nao katika kupunguza ajali."

Kamanda Muslimu anasema, katika kupambana na ajali wamejiwekea mkakati wa miezi sita kupunguza ajali kwa aslimia 45 na anasema, katika kutekeleza mkakati huo wanatoa elimu kwa makundi mbalimbali ya watumiaji barabara.

Anasema hilo linafanyika kupitia operesheni mbalimbali, kusimamia sheria na kuwaweka askari walezi katika 'vijiwe' vya waendesha bodaboda, ili waipate elimu kwa karibu.

> **Namba za wakuu wa vikosi vya usalama barabarani zimebandikwa katika mabasi yote ya usafiri, hivyo abiria wanatakiwa watoe ushirikiano kwa kupiga namba hizo ili kukomesha rushwa barabarani.**

"Nendeni mkawe mabalozi wa usalama barabarani, muwe tofauti na wale ambao hawakupata fursa ya kupata mafunzo haya.

"Tunaamini mchango mkubwa na nguvu ya vyombo vya habari katika kuelimisha jamii. Sekta ya habari imechangia sana kuleta mabadiliko haya," anatamka SACP Muslimu, alipofunga mafunzo hayo kwa wanahabari mjini Dodoma.

### RUSHWA IKOJE?

Kamanda Muslimu anasema kwa sasa nguvu kubwa ameielekeza katika mapambano dhidi ya rushwa, ambayo ndiyo inamuumiza kichwa.

"Natangaza vita vikali dhidi ya vitendo vya rushwa barabarani vinayofanywa na madereva na askari wa usalama barabarani, katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Mtoa rushwa na mpokea rushwa, wote wanafanya kosa la jinai, hivyo wanastahili adhabu kwa mujibu wa sheria,"anasema Kamanda Muslimu.

Katika kulikabili hilo, anasema ameshaweka mikakati mbalimbali ya kupambana na rushwa, mojawapo ni kuzuia na kupiga marufuku makondakta, hususani wa mabasi yaendayo mikoani, kushuka katika basi na kuwapelekea askari ratiba katika vibanda vyao barabarani.

Anaeleza imani yake kwamba, kufanya hivyo ni kiashiria kimojwapo cha rushwa na mbadala uliopo ni askari wa usalama barabarani wanapaswa kuingia ndani ya magari na kukagua, akiamini Kufanya hivyo:

"Nimetoa malelekezo kwa wakuu wote wa vikosi vya usalama barabarani mikoani, kuwa askari anapaswa kuingia ndani ya basi kukagua, badala ya kukaa ama nje au nyuma ya gari au kubaki kibandani, kumsubiri kondakta apeleke ile chati na kitabu cha ukaguzi..."



Kamanda wa Polisi Usalama Barabarani, SACP Fortunatus Muslimu, akiwa kazini. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

### ABIRIA JE?

Anasema, abiria nao wana mchango katika hayo ya kupiga vita rushwa, kwa kutoa taarifa kwa wakuu wa vikosi vya usalama barabarani, pindi wanapoona kuna viashiria vya rushwa wakati wako safarini.

"Namba za wakuu wa vikosi vya usalama barabarani zimebandikwa katika mabasi yote ya usafiri, hivyo abiria wanatakiwa watoe ushirikiano kwa kupiga namba hizo ili kukomesha rushwa barabarani," anasema SACP Muslimu.

### UREKEBISHAJI SHERIA

Pia, Kamanda Muslimu anasema pamoja na kupungua ajali za barabarani, Sheria ya Usalama Barabarani ya Mwaka 1973 iko mbioni kufanyiwa marekebisho ili iendane na wakati uliopo na iko katika hatua za mwisho, ipelekwe bungeni.

"Yapo mapungufu kadha wa kadha, ambayo yanahitaji kufanyiwa maboresho, yaendane na hali ya sasa. Pia iweze kukabiliana kikamilifu na changamoto za ajali za barabarani, pamoja na madhara yatokanayo na ajali hizo," anasema.

Kamanda Muslimu anadokeza baadhi ya maudhui yaliyotarajiwa kufanyiwa kazi katika marekebisho hayo ni: Mwendokasi, matumizi ya mikanda, kofia ngumu, matumizi ya vilevi na vizuizi vya watoto.

AFYA

# MEI 5 – 12; WIKI YA KIMATAIFA YA USALAMA BARABARANI

INATOKA UK.18

**MAONI YA ABIRIA**

Mkazi wa Magomeni, Mariam Issa, anasema huwa anatumia mara nyingi usafiri huo, hata hivyo kila anapotumia huwa na wasiwasi mwingi barabarani.

"Kulingana na kazi zangu, bodaboda ni usafiri ambao nautumia sana, kwa sababu huwa nahitaji kuwahi mjini kununua mzigo, ninafanya biashara ya genge.

"Pamoja na kwamba ninapanda bodaboda ili niwahi kununua mzigo na kuufukisha gengeni ili kuuza, lakini huwa naona bodaboda wana haraka zaidi. Hutaka kupenya hata unaona kabisa mnaweza kupata ajali, huwa nagombana nao kila ninapopanda. Ni hatari," anasema.


Mkazi wa Kigamboni, Hezron Kaiza, anaeleza kinachowatesa madereva wengi wa bodaboda na bajaji na hadi kufikia ajali za barabarani ni anachokiita 'ujana.'

"Ujana unawasumbua. Wana mihemko barabarani, wanaendesha ovyo, wanapiga honi bila mpangilio, utashangaa hata watu wazima walioingia kwenye biashara hiyo nao baadhi yao hufanya kama vile vijana. Yaani wana tabia zinazofanana, ni tabu tupu," anasimulia Kaiza.

Anaongeza: "Kusema kweli kukabiliana na ajali za barabarani lazima kila mmoja wetu afuate na atii sheria za usalama barabarani, hapo tutapona, vinginevyo kila siku watu watapoteza maisha."

**HALI HALISI DUNIANI**

Katika Ripoti ya Usalama Barabarani 2018 ya WHO, inakadiria kila mwaka zaidi ya watu milioni 1.35 hufariki dunia kwa ajali za barabarani. Hiyo ni sawa na vifo 3,400 kila siku.




> "Wana mihemko barabarani, wanaendesha ovyo, wanapiga honi bila mpangilio..

Idadi ya vifo 2018 imeongezeka ikilinganishwa na ripoti ya WHO ya mwaka 2015, ilivyokuwa na watu milioni 1.25.

Kwa mujibu wa ripoti mpya ya WHO, wanaoathirika zaidi na ajali za barabarani ni kundi la watoto wenye umri kati ya miaka mitano hadi 14 na vijana wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 29.

Kulingana na ripoti hiyo, ajali za barabarani zimekuwa sababu namba moja ya vifo vya watumiaji wa barabarani, wakiwamo watembea kwa miguu, waendesha baiskeli na wote wanaotumia vyombo vya moto.

Duniani, ajali za barabarani zinatajwa kuwa sababu namba nane ya vifo duniani. Hivi sasa WHO linaonya iwapo hatua hazitachukuliwa, huenda idadi itaongezeka kufikia sababu ya namba moja ifikapo 2030. Takwimu zinaonyesha kiwango cha vifo kutokana na ajali za barabarani katika kila watu 100,000 kipo juu katika nchi za Barani Afrika na Kusini Mashariki mwa Bara la Asia.

Kukabiliana nacho, Mpango wa Maendeleo Endelevu ya Dunia (SDGs), mataifa nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, wameweka lengo la kupunguza ajali kwa kiwango cha asilimia 50 ifikapo 2030.

**KAMANDA MUSLIMU**

Kamanda wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Fortunatus Muslimu, anasema pamoja na changamoto mbalimbali zilizopo, hali ya usalama barabarani kwa sasa nchini inaimarika.

"Idadi ya ajali inapungua. Vilevile idadi ya majeruhi na vifo nayo inapungua kwa mwaka jana, tukilinganisha na mwaka juzi ajali za barabarani zimepungua kwa kiwango cha asilimia 33," anabainisha.

"Kuhusu vifo kuna upungufu wa asilimia 31, ikiwa na maana ya kuokoa maisha ya watu 793 kwa kipindi cha mwaka mmoja katika kipindi cha mwaka 2018, idadi ya majeruhi imepungua kwa kiwango cha asilimia 32.

**TANZANIA JE?**

Maadhimisho ya Wiki ya Kimataifa ya Usalama Barabarani inayofanyika kati ya Mei 5 hadi 12, mwaka huu ikiwa na kaulimbiu 'Uongozi kwa Usalama Barabarani,' ni moja ya nyenzo ya kutoa majibu.

Hayo ni maadhimisho ya tano duniani, tangu yalipopitishwa na Umoja wa Mataifa mwaka 2015. Swali la kujiuliza, je Tanzania itaweza kufikia lengo la kupunguza ajali kwa kiwango cha asilimia 50 ifikapo 2030?

Mbunge wa Muheza na Mwenyekiti wa Mtandao wa Wabunge Masuala ya Usalama Barabarani, Balozi Adadi anasema: "Tumependekeza mabadiliko ya Sheria ya Usalama Barabarani tangu mwanzoni mwa mwaka jana. Tuna imani mabadiliko yatakayofanyika, yatapunguza kwa kiwango kikubwa ajali za barabarani."

# Waingereza wapunguza kuendekeza ngono

**London,** Uingereza

KATIKA siku za karibuni, imegundulika kuwa raia wa Uingereza wanafanya mapenzi kwa kiwango kidogo, tofauti na miaka ya nyuma, utafiti uliofanywa nchini humo umeeleza.

Utafiti huo uliochapishwa katika jarida la 'British Medical' unaeleza kuwa robo tatu (75) ya wanawake na wanaume raia wake hawajafanya mapenzi mwezi uliopita.

Idadi hiyo, ni ongezeko kwa takribani robo moja (25%), tangu mwaka 2001, takwimu zilizochukuliwa kutoka kwa watu 34,000.

Ripoti hiyo inaeleza kwamba zaidi ya nusu ya wanaume na wanawake wenye umri wa kati ya miaka 14 mpaka 44, ambao ni wajihi wa ujana, walifanya mapenzi wiki moja iliyopita.

Wapenzi wanaoishi pamoja au wanandoa, nao wanaelezwa kwamba, kiwango chao cha kufanya mapenzi kimeshuka zaidi.

Ni matokeo yanayojengwa na tafiti tatu zilizofanywa kitaifa, watafiti wakichambua tabia za washiriki wa ngono zilizofanywa katika miaka ya 1991, 2001 na 2012 na kutoa picha ya namna Waingereza wanavyojihusisha na ngono.

**KWA NINI IMEPUNGUA?**

Watafiti kutoka Shule ya Usafi na Dawa ya Kitropiki, unasema ushiriki wa tendo la ndoa umepungua, wengi wakitaka kuendelea kuhifadhi ubikira wao .

Pia, kundi la wenye umri chini ya miaka 25 na wale wasio na wapenzi, wanaonekana kuwa na unafuu kushiriki ngono. Kiwango chao kimeshuka.

Hicho ndicho kipo pia kwa wanandoa na wenye umri mkubwa au wapenzi wanaoishi pamoja kwa muda mrefu.

**KUNA MAANA GANI?**

Nusu ya wanawake (50%) na theluthi mbili (66%) ya wanaume katika utafiti uliopita, walisema wangependa kufanya mapenzi zaidi.

"Hamu ya kufanya mapenzi zaidi ilisikika kutoka kwa watu ambao wako katika ndoa au wapenzi wanaoishi pamoja," wanadokeza watafiti wakiongeza: "wanahitaji pongezi".

Mtafiti kiongozi, Profesa Kaye Wellings, anasema kasi ya maisha ya kisasa, inaweza kuwa sababu ya wengi kutofanya ngono kwa kiwango stahiki.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa wanaoathirika zaidi ni watu wenye uwezo wa wastani katika maisha. Profesa anaongeza: "Hawa ni wanawake na wanaume ambao mara nyingi wanapambana kazini, kuhudumia watoto na wana majukumu ya kuwatunza wazazi wao ambao wamekuwa wazee sasa."

Inawezekana shinikizo kubwa kutoka katika matokeo ya utafiti juu ya ngono unaweza kubadili mtazamo na watafiti hao wanaongeza kwamba, katika suala la usawa wa jinsia, inashauriwa wanawake kuwa wepesi kukutana na wenza wao, ili kukidhi mahitaji yao

Lingine linalotajwa ni kupunguza kukutana kimapenzi kati ya mwanamume na mwanamke, ni ongezeko la matumizi ya mitandao ya kijamii.

"Kufanya mapenzi kwa kiasi si jambo baya mara zote", anasema Profesa Wellings na kuongeza: "Ni jambo gani muhimu kwa watafiti, si kujua mara ngapi watu wanafanya mapenzi, lakini kwa nini muhimu kujua kutoshiriki kwao."

Kuna imani kwa baadhi ya watu kwamba, si watu wote wanafanya mapenzi sawa, wapo wanaofanya mara nyingi kuliko wengine.

Watafiti wana hoja kwamba ni jambo muhimu kuwa watu wanapaswa kutenga muda wa kufanya ngono, kwamba itawasaidia zaidi kisaikolojia.



# Biashara ya kiwanja yamtia matatani mwenyekiti mtaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MWENYEKITI wa Mtaa wa Tundu, Kata ya Nsalaga jijini Mbeya, Daudi Salila, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa amri ya Mkuu wa Mkoa, Albert Chalamila, kwa tuhuma za kushiriki kuuza kiwanja kwa watu watatu na kusababisha mgogoro.

Salila alikamatwa juzi baada ya Chalamila na maofisa wa Jiji la Mbeya kutembelea eneo hilo kwa ajili ya kushughulikia mgogoro uliokuwa unafukuta na kubaini ndiye chanzo chake.

Inadaiwa aliyekuwa mmiliki wa nyumba hiyo, Bastiani Kibona, alikitumia kiwanja hicho kama dhamana wakati anachukua mkopo kwenye chama cha akiba na mikopo cha Uwamu Saccos.

Mwanasheria wa Jiji la Mbeya, Triphonia Kisiga, alisema baada ya Kibona kuchukulia mkopo kiwanja hicho wakati mwenyekiti akishuhudia, baadaye akakiuza kwa watu wengine kabla hajarejesha mkopo, lakini mwenyekiti hakuchukua hatua zozote badala yake alishiriki kuuza.

Alisema hali hiyo ilisababisha mgogoro miongoni mwa wanunuzi hali iliyopelekea malalamiko hayo kufika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na ndipo wakaamua kwenda kufuatilia na wakabaini chanzo chake.

"Kibona aliuza eneo hilo kwa walalamikaji, huku akijua kuwa alichukulia mkopo Saccos, cha kushangaza zaidi ni kwamba mwenyekiti wetu wa serikali ya Mtaa alishuhudia mara ya kwanza wakati Kibona anachukulia mkopo kiwanja hicho, lakini baadaye akashuhudia wakati Kibona anauza kwa walalamikaji," alisema Kisiga.

Alisema walibaini mwenyekiti huyo alishirikiana na Kibona kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, na kwamba anastahili kuchukuliwa hatua na vyombo vya sheria.

Akitoa maelezo kabla ya kukamatwa na Polisi, Salila alikiri kushuhudia Kibona akichukulia mkopo kiwanja hicho, na kwamba hata wakati anatangaza kuiuza alishuhudia na akachukua hatua kwa kupeleka taarifa Saccos.

Alisema alipofikisha taarifa hizo Saccos, alijibiwa kuwa anatakiwa amwache Kibona auze eneo hilo ili akalipe fedha alizokopa ndipo akashiriki kuiuza, lakini kwa bahati mbaya Kibona hakwenda kulipa deni.

"Alikuja mzee (jina lake nimelisahau) ikaonekana yeye ndiye auziwe kiwanja na kweli akanunua, baada ya miaka mitatu mzee akiwa amejenga nyumba imefika kwenye lenta ikaonekana yule bwana (Kibona) hakwenda kulipa deni Saccos na ndipo wakaenda kuandika kuwa nyumba inauzwa ndipo mzee akashtuka," alieleza Salila.

Alisema baada ya Mzee huyo kushtuka alimshirikisha na yeye akamwambia kuwa alikuwa hajui kuwa Kibona hakwenda kulipa hela Saccos na akamwahidi kuwa shahidi wake mpaka mwisho.

Baada ya maelezo hayo ambayo hayakumridhisha Chalamila, aliamuru Jeshi la Polisi kumkamata kiongozi wakati tatizo hilo likishughulikiwa.

Alisema amebaini kuwa baadhi ya viongozi wa vijiji na mitaa wakiwamo wenyeviti na watendaji ndio wamekuwa vyanzo vya migogoro mingi kwenye jamii kutokana na kukiuka sheria za nchi.

"Wenyeviti wetu wa mitaa wanakiuka sheria na baadaye wanajikuta eneo moja linakuwa na wamiliki wawili ama watatu na kupelekea vilio, sasa tumeagizwa na mheshimiwa rais watu wote wanaosababisha vilio hivi lazima washughulikiwe," alisema Chalamila.



Mchuuzi wa machungwa akiyapanga wakati akisubiri wateja katika Soko la Buguruni, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JOHN BADI**

# Kinamama wajasiriamali walia mazingira magumu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANAWAKE wajasiriamali jijini Mbeya, wanadaiwa kufanyia shughuli zao katika mazingira magumu, hivyo kushindwa kujikwamua kwenye umaskini.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi wa Shirika lisilokuwa la kiserikali la Equality For Growth lenye makao makuu Jijini Dar es salaam, Dk. Jany Magigita, alipokuwa anawasilisha taarifa ya utafiti wa shirika hilo kuhusu mazingira ya kufanyia shughuli za ujasiriamali.

Alisema maeneo ya kufanyia shughuli ni machache kuliko mahitaji na kwamba hata yaliyopo yana miundombinu mibovu inayopelekea shughuli za wanawake kudorora, hivyo kushindwa kunufaika na shughuli zao.

Alisema kutokana na hali hiyo, Shirika linaishauri Halmashauri ya Jiji kwa kushirikiana na wajasiriamali kuboresha maeneo hayo kwa kuhakikisha yanafikika na yanakuwa na miundombinu yote inayochochea biashara zao.

"Wanawake ni kundi kubwa linalochochea uchumi uliofichika, lakini linafanya shughuli zake kwenye mazingira yasiyo rafiki, shughuli zao za ujasiriamali zinaonekana kama vile ni sekta isiyothaminiwa, hivyo lazima mabadiliko yafanyike," alisema Dk. Magigita. Alisema Shirika hilo linaishauri Serikali kuzingatia vigezo muhimu wakati wa kutenga maeneo ya wajasiliamali ikiwamo kulifanya eneo kufikika na wateja.

Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Jiji la Mbeya, Vincent Msola, alikiri kuwapo kwa changamoto hizo, huku akieleza kuwa Serikali inaendelea kupambana nazo ili kuhakikisha wajasiriamali wote bila kujali jinsia zao wanafanya shughuli zao katika maeneo rafiki.

Alisema moja kati ya jitihada wanazozichukua ni pamoja na kuanza kulitumia eneo la uwanja wa ndege wa zamani uliopo katika Kata ya Iyela ambao Rais Dk. John Magufuli aliidhinisha utumike kwa ajili ya wamachinga.

Alisema Ofisi yake imepokea majibu ya utafiti huo na kwamba mbali na mazingira ya wajasilimali kutokuwa rafiki kwao, pia inaonyesha kuwa wana mitaji midogo pamoja na elimu ndogo ya ujasiriamali hali inayosababisha washindwe kunufaika na shughuli zao.

"Hizi changamoto tulikuwa tunazifahamu na sisi kama wataalamu wa Jiji baadhi tulishaanza kuzitatua ikiwamo ya maeneo ambayo tulianza kuishughulikia tangu mwaka 2013," alisema Msola.

Nao baadhi ya wajasiliamali waliomba Serikali pamoja na mashirika mbalimbali kuendelea kutoa elimu ya biashara kwao kwa madai kuwa wanashindwa kuendelea kutokana na kukosa elimu ya biashara.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Maria Mwaitenda, alisema wakati mwingine huwa wanaitwa kwenye mafunzo ya ujasiriamali, lakini hawaendi kwa sababu hawajui umuhimu wa mafunzo hayo.

Alisema wakati mwingine wanajiamulia kupanga biashara zao hata katika maeneo hatarishi kwa sababu wanaona watu wengi wanapita, hivyo akaiomba Serikali kuendelea kutoa elimu.

## Wajawazito washauriwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAJAWAZITO wameshauriwa kuhudhuria Kliniki mara kwa mara kufuatilia maendeleo ya ujauzito wao ili kuepuka madhara yanayoweza kuwapata ikiwamo kuathiriwa na kifafa cha mimba ambacho kinasababisha vifo vya wajawazito wengi. Ushauri huo ulitolewa na Daktari Bingwa wa magonjwa ya wanawake katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya Kitengo cha Wazazi Meta, Dk. John Francis, alipokuwa anazungumza na gazeti hili kuhusu ugonjwa wa kifafa cha mimba.

Alisema ugonjwa huo husababisha vifo vya wajawazito wengi, hivyo akawashauri kuwa njia pekee ya kuepuka madhara yake ni kuhudhuria kliniki ili kufuatilia maendeleo ya afya yake pamoja na mtoto aliyeko tumboni. Alisema ugonjwa huo una dalili nyingi ambazo madaktari wana uwezo wa kuubaini endapo mjamzito atahudhuria kliniki, na kwamba kabla ya kutokea ugonjwa huo, huwa unatanguliwa na tatizo la shinikizo la damu ya mimba ambayo huwa inapanda.

Dk. Francis alisema shininizo hilo ni dalili mojawapo ya mjamzito kuwa katika hatari ya kupata kifafa cha mimba, na kwamba endapo ikibainika wataalamu wa afya wana uwezo wa kumshauri mama pamoja na kumpatia matibabu sahihi na akapona.

"Tatizo hilo linaweza kuathiri figo, mapafu, ubongo, mishipa ya damu na kusababisha mtu akavimba mwili mzima na hali hiyo isipotibiwa mapema inapelekea kupata kifafa cha mimba," alisema Dk. Francis.

Alisisitiza kuwa kabla kifafa hicho hakijatokea kuna dalili zingine ambazo huwa zinatangulia ikiwamo kusumbuliwa na kipanda uso, mjamzito kutoona vizuri ama kuona maruwe ruwe pamoja, kutapika na kusumbuliwa na tumbo la juu (chembe ya moyo). Alisema pia wanawake wanashauriwa kuhudhuria kliniki ili kuepuka matatizo mengine yanayosababishwa na ujauzito, na kwamba huwa wanashauriwa hata aina ya vyakula wanavyostahili kula kwa ajili ya afya ya mama na mtoto.





# NSSF kutanua wigo kusajili wanachama

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SHIRIKA la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), limepanga kutumia vitambulisho vya wajasiriamali vilivyotolewa na serikali kwa ajili ya kuwasajili wanachama wapya wa mfuko huko kwa upande wa sekta isiyo rasmi.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, William Erio, alipokuwa akielezea utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) yaliyotolewa Oktoba 31, mwaka jana kwa hesabu za mwaka wa fedha 2016/17.

Alisema kupitia mfumo huo, wanatarajia kuandikisha waendesha bodaboda na bajaj wapatao 22,000 na kuwa kati ya Januari hadi Aprili, mwaka huu wameandikisha wanachama 4,300.

"Tumepanga kuyafikia makundi mengine kwa kutumia vitambulisho vya wajasiriamali vilivyotolewa na serikali kwa kuwasiliana na mamalaka za serikali za mitaa na mikoa," alisema.

Hata hivyo, alisema moja ya mafao watakayotoa ni bima ya afya na tayari wameanza mazungumzo na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ili fao hilo litolewe na mfuko huo.

Alisema pamoja na mpango huo, pia tayari shirika limeweka mfumo wa TEHAMA utakaotumika kutunza kumbukumbu za fedha na hivyo kuongeza udhibiti wa ndani na usahihi wa taarifa.

"Shirika limetekeleza agizo la kutunza kumbukumbu za fedha kwa kutumia mfumo wa TEHAMA ili kuongeza udhibiti wa ndani na usahihi wa taarifa zinazotolea," alisema.

Alibainisha mfumo wake huo umesimikwa rasmi Aprili 8, mwaka huu ambapo kwa sasa kumbukumbu zake zote za fedha zitatunzwa kielektroniki na hesabu za mwaka wa fedha unaoishia Juni mwaka huu yatatolewa ndani ya mfumo huu.

Aidha, alisema kuanzia Mei 2, mwaka huu, Mfuko umeanza rasmi kufanya usuluhishi wa kibenki kwa kutumia mfumo mpya wa kieletroniki.

"Masuala haya yalikuwa na changamoto kutokana na zoezi la usuluhishi kufanyika pasipo kutumia mfumo wa kieletroniki na usuluhishi ulikuwa ukifanyika katika ofisi za mikoa na hivyo kufanya utaratibu wa ufuatiliaji kuchukua muda mredu katika kutatatua," alisema.

Kadhalika, alisema tangu Machi 25, mwaka huu, NSSF imejiunga na mfumo wa Serikali wa Malipo kwa njia ya kieletroniki jambo ambalo litasaidia kuondoa tatizo la hundi zinatokataliwa na upotevu wa fedha.

Kuhusu utekelezaji wa agizo la kuharakisha upimaji wa ardhi yote iliyonunuliwa bila kupimwa, Mkurugenzi huyo alisema hadi kufikia Aprili 2019, maeneo yenye jumla ya viwanja 3,185 yalikuwa yameshapimwa na ufuatiliaji wa hati unaendelea katika manispaa za Ubungo, Kinondoni, Kigamboni, Ilemela Kibaha na Wizara ya Ardhi.

# Waislamu watakiwa kusaidia wasiojiweza

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHEIKH wa Mkoa wa Dodoma, Mustapha Rajabu, amewataka waumini wa dini ya kislamu kuutumia mwezi Mtukufu wa Ramadhani kuwakumbuka wasiojiweza ili nao waweze kufunga vyema.

Kauli hiyo aliitoa juzi alipokuwa akizungumza na waumini wa dini hiyo katika harambee ya kuchangia ujezi wa uzio wa majengo ya madrasa ya Jahislimia jijini hapa.

Aliwataka waumini wale wenye uwezo katika kipindi hiki cha mwezi mtukufu kutowasahau wasio kuwa na kipato. "Ninawaomba waumini wenye uwezo kuwakumbuka kwenye kufuturu na waumini wasiokuwa na uwezo, ukizingatia kuwa mwezi huu ni kupendana bila kujali itikadi yeyote ya kidini," alisema.

Aidha, aliwataka waumini hao kutoa mali na fedha ili waweze kufanikisha ujenzi huo wa uzio ambao utawafanya wanaosoma kuwa huru tofauti na sasa ambapo kuna muingiliano wa watu.

Pamoja na hayo, kiongozi huyo alisema jukumu la kuendeleza miradi ya dini ya Kiislamu lipo mikononi mwa waumini wenyewe, hivyo hakuna sababu ya kusubiri wahisani kwa ajili ya kufadhiliwa ambapo imekuwa ikichelewesha maendeleo yake.

Aliomba wafanyabiashara kutopandisha bei za bidhaa katika kipindi hiki.



Kaimu Kamishna Msaidizi Idara ya Sera katika Wizara ya Fedha na Mipango, Michael Nyagoga (kushoto), akijadili jambo na mchumi kutoka Wizara hiyo, Dk. Lorah Madete, wakati wa kikao cha kujadili taarifa ya utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG's), jijini Dodoma juzi. **PICHA: WFM**

# Bunge lampa wiki moja Mkurugenzi TPA

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imetoa wiki moja kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Deusdedit Kakoko na Msajili wa Hazina kufika mbele ya kamati hiyo ili kueleza utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa Agosti mwaka jana.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka jijini hapa, baada ya Mkurugenzi huyo kushindwa kufika mbele ya kamati hiyo ili kuelezea utekelezaji wa maagizo ya kamati yaliyotolewa kipindi hicho.

Kaboyoka alimtaka Mkurugenzi huyo pamoja na menejimenti yake kufika mbele ya kamati hiyo Mei 24, mwaka huu.

"Kama atashindwa kufanya hivyo basi kamati itajua mapendekezo tutakayoyatoa kwa mamlaka yake ya uteuzi," alisema na kuongeza:

"Sisi Kamati tulikaa naye hapa, na taarifa za kuitwa mbele ya kamati anazijua muda mrefu, kitendo cha dharau aliyoifanya akutume wewe bosi wake (Katibu Mkuu), bila kumtuma Mkurugenzi wa fedha, mkaguzi wa ndani au wasaidizi ni adharau ambayo haikubaliki."

Alisema Mkurugenzi huyo anajua kuwa fedha hizo za umma anaweza kuzitumia anavyotaka kwa kuwa kuna malalamiko juu ya mfumo wake wa Tehama.

"Tuna details (taarifa) ya yote yanayofanyika bandarini, lakini tulitaka kusikia kutoka kwake, sasa wewe (Katibu Mkuu Uchukuzi ) tukihitaji majibu ya nyongeza hatuna uhakika kama utaweza kuyajibu," alisema.

Mwenyekiti huyo alisema mamlaka hiyo imepata hati chafu, fedha nyingi zinapotelea bandarini, Tehama haifanyi kazi.

"Anatuletea kaimu wa Tehama? Hatukubali.

Kwa hiyo nasema kwa machungu maana kamati hii imesikitika sana na tunataka Spika ajue kwamba kwakweli tumechukia sana," alisema. Naye Mbunge wa Magomeni (CCM), Jamal Kassim, alibainisha kuwa moja ya maagizo ambayo kamati ilitoa kwa TPA ni kuboresha udhaifu katika mfumo wa TEHAMA ambao umekuwa ukisababisha upotevu wa mapato ya nchi.

Kufuatia hali hiyo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano (anayeshughulikia Uchukuzi), Dk. Leonard Chamuriho, ambaye katika kikao hicho alimwakilisha Mwenyekiti wa bodi aliyemaliza muda wake, aliomba radhi na kueleza kuwa nia ya Wizara si kupeleka kwenye kamati uwakilishi ambao haujakamilika.

"Tulipata maswali matatu ambayo tuliyapitia na tulipata dharura ya kiafya ya mtendaji mkuu tukaona bado tunaweza kuja kuwakilisha, kwa hilo tunaomba radhi," alisema.





Mkuu wa Zantel Zanzibar, Mohamed Khamis Mussa (katikati), akiwaonyesha waandishi wa habari kipeperushi cha maelezo ya ofa za mfungo wa mwezi mtukufu wa Ramadhan, zilizotolewa na kampuni hiyo, wakati wa uzinduzi wake uliofanyika mjini Zanzibar jana. Wengine ni Mkuu wa Bidhaa wa Zantel, Aneth Muga (kushoto ), na Katibu wa Mufti za Zanzibar, Fadhil Soraga. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

# RC aagiza kufungwa baa, kumbi za starehe mwezi wa Ramadhani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, ameagiza kuwa baa zote na kumbi za starehe zinazopiga mziki katika mkoa huo zifungwe katika kipindi hiki cha Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Akizungumza na waandishi wa habari, alilitaka Baraza la Manispaa kusimamia zoezi hilo ili waumini wa dini ya kiislamu kufunga Mwezi wa Ramadhni bila ya buguza.

Mkuu huyo wa Mkoa amegiza pia migahawa yote inayotoa huduma za chakula ambayo siyo ya kitalii ifungwe katika Mkoa huo.

Alisema kwa wale waumini wa dini ya Kikristo watawekea sehemu maalum ya mgahawa kwa ajili ya kwenda kupata chakula kwa utaratibu unaokubalika. Aidha, aliwataka watembeza watalii kuwapa maelekezo watalii kuhusu mavazi wanayostahiki katika kipindi hiki cha Ramadhani.

"Niwaombe ndugu zangu wanaotembeza watalii kutoa maelekezo kwa wageni wanaofika Zanzibar kuhusu mavazi yanayoostahiki hasa katika kipindi hiki cha mfungo," alisema.

# Mikakati kuwezesha wanawake na vijana

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWAKILISHI wa Jimbo la Jang'ombe, Ramadhani Hamza Chande, amesema uongozi wa Jimbo hilo umeweka mikakati ya kuhakikisha wanawezesha wanawake na vijana kujiajiri kupitia vikundi vya ushirika na ujasiriamali ikiwa ni kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015-2020.

Ameyasema hayo wakati akikabidhi fedha taslim Sh. milioni 7.5 kwa ushirika wa Mwendo na Sh. milioni 14 kwa ushirika wa Nuru Njema katika Jimbo la Jangombe zilizotolewa na uwezeshaji Sacos ili kuwasaidia kuanzisha miradi ya kimaendeleo.

Alisema kitendo cha kuanzishwa kituo maalum cha ujasiriamali na kutoa mikopo ni miongoni mwa juhudi wanazozichukuwa katika kuwanyanyua Wananchi kiuchumi na kijamii.

Aidha aliipongeza uwezeshaji Sacos kwa kutoa mikopo bila ya kuwa na riba jambo ambalo litawawezesha kupata pesa za kuendesha miradi yao itakayoweza kujikwamua na tatizo la umasikini na kufikia malengo yaliokusudiwa ya kujikwamua kiuchumi.

Naye Ofisa wa vyama vya ushirika Zanzibar, Zuhura Suleiman Mnoga, alisema kwa kipindi cha miezi minne wametoa mikopo zaidi ya milioni 30 kwa vikundi vya Jangombe pekee na kuwaomba wanakikundi hao kurejesha kwa wakati ili wapate kuchukuwa mikopo mingine.

Alisema baadhi ya vikundi vya ushirika vinavyopewa mikopo huchelewa kulipa hali ambayo imekua ikikosesha fursa wengine kupata mikopo kwa wakati.

Kwa upande wao viongozi wa ushirika wa Mwendokasi na Nuru Njema katika Jimbo hilo, wamepongeza uwezeshaji Sacos kwa kutoa mkopo hiyo lakini tatizo kubwa ni ukosefu wa Ofisi na mitaji midogo na kuwaomba kuwasaidia kwa hali na mali.

# Mamia wakimbia makazi kisa nyumba kuzingirwa mafuriko

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAMIA ya wakazi katika Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, wamehama makazi yao kutokana na maji ya mvua kuzingira nyumba zao. Hali hiyo imesababishwa na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha, Mkuu wa mkoa huo, Ayoub Muhammed Mahmoud, amesema.

Akizungumza na waandishi wa habari, Ayoub aliwataka wananchi kuchukua tahadhari kutokana na mvua kubwa inayoendelea kunyesha ambayo tayari imeshaleta madhara kwenye mkoa huo na nyumba 134 kuathirika, huku wananchi walilazimika kuzihama baada ya kuzingirwa na maji.

Mkuu huyo wa mkoa alisema kuwa nyumba hizo ni katika maeneo ya shehia za Sebleni, Jangombe, Chuwini na kwa Mtumwa Jeni katika Mkoa huo.

Alieleza kuwa wananchi wanaoishi katika nyumba hizo wamelazimika kuhama wa wamehifadhiwa kwa ndugu na jamaa zao. Ayoub aliwataka wananchi wanaoishi mabondeni kuhama ili kuweza kunusirika na maafa ambayo yanaweza kutokea kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha. "Niwaombe wananchi kuchukua tahadhari na maradhi ya mlipuko kwani kipindi cha mvua huibuka maradhi ya mlipuko,"alisema Ayoub.

# Katibu Mkuu afa katika ajali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATU watatu wamefariki dunia katika Mkoa wa Mjini Magharib Unguja katika wiki iliyopita kutokana na sababu mbalimbali, akiwamo katibu mkuu wa wizara.

Akizungumza na waandishi wa habari Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharib Unguja, Thobias Sedeyoka, alisema kuwa watu hao walifariki dunia ni Katibu Mkuu Wizara ya Biashara na Viwanda Juma Ali Juma aliyepata ajali ya kugongwa na gari na kusababisha kifo chake.

Alisema kuwa ajali hiyo ilitokea April26, majira ya saa saba mchana huko Mwakaje ambapo aligongana na gari yenye namba Z 968 GQ P/V iliyokuwa ikiendeshwa na Amour Suleiman Ali.

Kamanda huyo alisema majira ya saa nane mchana katika bwawa la Sebleni alikutwa mzee mwenye miaka 50 ambae ametambulika kwa jina la Suleiman Mzee akiwa amefariki dunia.

Aidha, alisema taarifa nyengine ya kifo ni cha Ramadhan Shaaban miaka 40 ameonekana akiwa ameshafariki dunia eneo la Mwanakwerekwe ambapo mwili wake ulikuwa na majeraha kwa kushambuliwa na watu wasiojulikana, na chanzo cha tukio hilo hakijajulikana.

Kamanda huyo aliwataka wananchi kuacha kuchukua sheria mikononi mwao, badala yake wahalifu wawapeleke katika sehemu husika ili hatua zak isheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao.

"Niwaombe wananchi kuacha kuchukua sheria mikononi mwao kwa kuwapiga na kuwaua wahalifu, badala yake

# Simiyu yapiga hatua tohara ya wanaume

**Na Happy Severine,**
SIMIYU

JUMLA ya wanaume 33,950 katika Mkoa wa Simiyu wamefanyiwa tohara kinga kwa miezi saba, kuanzia Oktoba 2018 hadi Aprili, 2019 ikiwa ni asilimia 57 ya lengo la kuwafikia wanaume 59,130.

Hayo yalisemwa na mshauri wa huduma za tohara wa Mkoa kutoka Shirika la Intrahealth International, Dk. Kentgen Evarist, wa mahojiano maalum na Nipashe.

Dk. Evarist alisema shirika hilo lina malengo ya kuwafikia wanaume 59,130 ambao hawajafanyiwa huduma hiyo, katika kipindi cha kuanzia Oktoba 2018 hadi Septemba 2019.

"Tumefanikiwa kuvuka nusu ya lengo letu ambalo tulijiwekea katika Mkoa wa Simiyu, tuna imani hadi kufikia Septemba 2019 tutafanikiwa kuwafanyia tohara kinga wanaume wote ambao tuliwalenga," alisema Dk. Evarist.

Alisema shirika hilo kupitia mradi huo chini ya ufadhili wa Mfuko wa Rais wa Marekani wa kupambana na VVU (PEPFAR) kupitia CDC Tanzania, umepata mafanikio makubwa kwa wanaume wengi kujitokeza kufanyiwa tohara.

Mshauri huyo alieleza kuwa huduma hizo zimekuwa zikitolewa katika vituo tisa vya kutolea huduma za afya vilivyoko kwenye wilaya zote za Bariadi, Itilima, Maswa, Meatu, Busega pamoja na Hospitali Teule ya mkoa.

Kwa mujibu wa Dk. Evarist, mwitikio umeongezeka zaidi kwa wanaume kwenda kufanyiwa tohara, kutokana na shirika hilo kutoa elimu zaidi kwa wanawake kwenda, kuwashawishi waume zao kufanyiwa huduma hiyo. "Mwanzoni vilikuwapo vikwazo vingi hasa imani potofu, lakini baada ya kuwaelimisha wanawake wakatambua umuhimu wa jambo hilo, wengi huwashawishi wenzi wao na wanakuja kwa wingi kufanyiwa tohara," alisema Dk. Evarist.

Hata hivyo, alisema bado wanakabiliwa na idadi ndogo ya wanaume wenye umri wa kuanzia miaka 25 hadi 29 ambao ndiyo walengwa wakuu kufanyiwa huduma hiyo kutokana na kukabiliwa na majukumu mengi hasa kilimo na ufugaji.

Shirika la IntraHealth International kwa kushirikiana na Kamati za Afya za mikoa na wilaya linatoa huduma ya tohara kama kinga kwa wanaume katika mikoa ya Simiyu, Mwanza, Mara, Geita, Shinyanga, Kagera na Kigoma.



Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu (Kulia), akizungumza na baadhi ya wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi na wafanyakazi wa benki hiyo wakati wa hafla hiyo jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA:MPIGAPUCHA WETU**

# Usambazaji majiko nishati mbadala Dar waiva

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo TIB, imeingia makubaliano na Kampuni ya Consumer Choice ya mradi wa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala na safi ya 'bioethanol' ya kupikia kwa kaya milioni moja jijini Dar es Salaam ambao utagharimu dola za marekani milioni 1.2

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa utilianaji saini mradi huo uliodhaminiwa na Shirika la Maendeleo ya Viwanda la Umoja wa Mataifa (UNIDO), Mkurugenzi wa fedha za Uwakala kutoka TIB, Lilian Mbassy alisema mradi huo unaumuhimu mkubwa kwa kuwa ni rafiki kwa mazingira na pia utatoa fursa za ajira kwa Watanzania. "Mradi huu ni muhimu sana kwa TIB na Taifa kwa ujumla kwa kuwa taasisi hii ya fedha ndiyo yenye mamlaka ya kuendesha mipango ya kukuza uchumi na kutambua sera mbalimbali za maendeleo ya taifa kwa niaba ya serikali, hivyo ni furaha kwetu kuona wadau wa maendeleo kama UNIDO wakiwa na imani kwetu na kuwekeza katika miradi kama hii," alisema Mbassy ambaye katika makubaliano hayo alimwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa TIB

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Consumer's Choice Frida Mlingi, alisema wamejipanga kuzifikia zaidi ya kaya milioni jijini Dar es salaam kwa lengo la kuwapa elimu juu ya matumizi ya majiko hayo yanayotumia nishati mbadala ya 'bioethanol' ambapo gharama zake zipo chini ukilinganisha na matumizi ya nishati zingine kwa kupikia.

Aliongeza kuwa majiko hayo hayana milipuko na ni salama kwa watumiaji, hivyo hawana sababu ya kuwa na wasiwasi wakati wa kuyatumia na tayari katika hatua ya mwanzo wameandaliwa vijana 60 ambao watafanya kazi ya kutoa elimu na kusambaza kwa watumiaji

"Usambaji wa majiko haya ni fursa kwa vijana wengi wa Kitanzania kupata ajira, lakini tutatumia nafasi hiyo kutumia elimu ya matumizi sahihi ya majiko hayo ili iwe rahisi kwa watumiaji kuelewa namna ya kuyatumia na muhimu saidi ni juu ya usalama wa majiko yenyewe," alisema Mlingi

Naye Mwakilishi Mkazi wa UNIDO nchini, Stephen Kargbo, alisema mradi huo utasaidia kupunguza hatari zinazohusiana na uchafuzi wa mazingira ambazo huathiri sana wanawake na watoto.

"UNIDO tunafuraha kushirikiana na TIB kwa kuwa tunaamini mradi huu unawasaidia watu ambao tumewalenga hususani akina mama na watoto ambao wamekuwa wahanga wakubwa wa mazingira ya jikoni," alisema Kargbo

# NGO yajitosa elimu Ukimwi na kifua kikuu

**Na Mary GEOFREY**

TAASISI isiyo ya kiserikali ya Kupinga Unyanyasaji wa Kijinsia (CAGBV), imeanzisha utaratibu wa kutoa elimu, upimaji, ushauri na jinsi ya kuzuia maambukizi ya magonjwa ya Ukimwi, kifua kikuu (TB) na masuala ya jinsia katika maeneo zinakojengwa barabara za mwendokasi awamu ya pili.

Wananchi wanaoishi pembezoni mwa barabara inayopitiwa na mradi huo, watanufaika wakiwamo watu wa kawaida, wafanyabiashara wakubwa na wadogo kama, wamachinga, bodaboda, mama lishe, wafanya biashara kwenye nyumba za wageni na wengine.

Akizungumza katika warsha ya ufunguzi wa mradi wa uelimishaji, upimaji,ushauri na uzuiaji maambukizi ya magonjwa mbalimbali, jijini Dar es Salaam Mkurugenzi Mtendaji wa CAGBV, Sophia Komba, alisema mradi huo ni wa miezi mitatu kwa kuanzia.

"Mradi huu umekuja kutokana na ukweli kuwa, mara nyingi katika ujenzi mkubwa wa barabara kama huu unakuwa na muingiliano mkubwa wa watu kutoka sehemu mbalimbali, hivyo wanajamii wanakuwa katika hatari ya kupata magonjwa ya kuambukizwa kama hayo yaliyotajwa," alisema Komba.

Alieleza kuwa waliona usawa wa jinsia ni muhimu kwa sababu kunakuwa na kundi la watu wanaoathirika kwa kutokujitambua yakiwamo makundi ya wanawake, watoto na watu wenye ulemavu.

"Mfano mzuri tumeshuhudia wa sasa hivi wa kinamama kuachiwa watoto na kutelekezwa ni kwa ajili ya watu wanaokuja kwa muda na kwenda zao. Vilevile kunaweza kutokea kutelekezwa kwa familia na mengineyo ambayo itaathiri zaidi wanawake na watoto. Kutokana na muingiliano huu, watu wenye ulemavu wanaweza kupata madhara kutokana na hali yao ya ulemavu," alisisitiza.

Alisema lengo kuu la warsha hiyo lilikuwa ni kujengeana uwezo na kuwashirikisha viongozi ili kuelewa mradi na kutoa ushirikiano katika kipindi chote cha mradi utakapokuwa unaendelea.

"Mradi huu wa uelimishaji utaenda katika ngazi ya jamii kwa makundi mbalimbali na vilevile tutatoa elimu mashuleni na kwenye makundi ya watu wa kawaida wa mtaani," Komba alisema.

Alisisitiza pia malengo makuu pia ni kuhakikisha haki za binadamu zinaheshimiwa kwa watu wote wanawake, watoto, watu wenye ulemavu na wanaume. "Tusingependa kuona kundi moja la binadamu haliishi vizuri kwa sababu ya kitu fulani."

Ujenzi wa barabara za mwendokasi awamu ya pili, utaanza katika barabara ya Kilwa kuanzia katikati ya jiji la Dar es Salaam hadi Mbagala Rangi Tatu, barabara ya Kawawa kuanzia Magomeni, barabara ya Chang'ombe kuanzia Mgulani hadi makutano ya barabara ya Kilwa na eneo la Mgulani JKT.

HABARI KIMATAIFA

## Marekani yaanza mpango kubana wahamiaji

**WASHINGTON,** Marekani

IDARA ya uhamiaji na forodha ya Marekani-ICE imeanzisha mpango wa ushirikiano kati ya serikali kuu, serikali za wilaya pamoja na majimbo ambao utaondoa kanuni za kuwapatia hifadhi wahamiaji wasio na vibali na kuwapatia mamlaka maafisa wa wilaya kuwakamata.

Kanuni mpya itawaruhusu maafisa wa miji kuwakamata washukiwa wa uhalifu badala ya kuwaachia washukiwa hao.

Kwa sasa wataipatia ICE saa 48 za ziada kuwafikisha washukiwa kwenye kizuizi cha serikali kuu.

Chini ya mpango huo unaofahamikia kama Warrant Service Officer-WSO uliotangazwa mwanzoni mwa wiki katika wilaya ya Pinellas kwenye jimbo la Florida nchini Marekani, Maafisa wa miji na wilaya wataruhusiwa kuwakamata watu kuhusiana na masuala ya uhamiaji. **VOA**

# Iran yajiondoa kwenye mkataba wa nyuklia

**TEHRAN,** Iran

IRAN imesema itaongeza urutubishaji wa madini ya uranium baada ya siku 60, mwaka mmoja baada ya Marekani kujiondoa kwenye mkataba huo wa kimataifa.

Rais wa Iran, Hassan Rouhani amesema baada ya siku 60 Tehran itaongeza zaidi urutubishaji wa madini ya uranium yanayotengeneza nyuklia ambayo yamezuiwa na mkataba huo.

Mkataba huo unalenga kukabiliana na utengenezaji wa nyuklia ili iweze kuondolewa vikwazo vya misaada, lakini uhasama umeongezeka tangu Marekani ijiondoe.

Uchumi wa Iran umeyumbishwa na vikwazo vipya vya Marekani dhidi yake.

Mkataba wa nyuklia uliokubaliwa na Iran na mataifa mengine matano wanachama wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Nchi zinazounda baraza hilo ni pamoja na Marekani , Uingereza , Ufaransa , Uchina na Urusi, pamoja na Ujerumani, ambapo mkataba huo uliingia dosari baada ya Rais wa Marekani, Donald Trump alipotangaza kujiondoa mwaka mmoja uliopita.

**Nchi zinazounga mkono mkataba huo kutoka Ulaya, ambazo zilipinga vikwazo vipya dhidi ya Iran zimekuwa zikijaribu kutafuta njia za kuendeleza.**

Tangu wakati huo thamani ya fedha ya Iran iliporomoka kwa kiwango ambacho hakikuwahi kushuhudiwa, viwango vya mfumuko wa kiuchumi vya mwaka vilikuwa vikubwa na wawekezaji wa kigeni wakaihama nchi.

Nchi zinazounga mkono mkataba huo kutoka Ulaya, ambazo zilipinga vikwazo vipya dhidi ya Iran zimekuwa zikijaribu kutafuta njia za kuendeleza.

Hilo ni pamoja na kuanzisha mfumo maalumu wa malipo ya kusaidia makampuni ya kimataifa yanayotaka kuendelea kufanya biashara na Iran kwa kukiuka vikwazo.

Lakini nchi hizo ziliionya Iran kwamba inapaswa kuendelea kuheshimu vipengele vyote vya mkataba, hususani kipengele kinachohusiana na shughuli za nuklia.

Hata hivyo, chini ya mkataba unaofahamika kama mpango wa pamoja wa utekelezaji (JCPOA) - Iran ilisema kuwa itachukulia kuanzishwa upya kwa vikwazo kama sababu ya kuacha utekelezaji wa mkataba.

Hali ya uhasama kati ya Marekani na Iran ilianza miaka mingi iliyopita wakati wa mapinduzi ya Iran mwaka 1979.

Rais Trump amechukua msimamo mkali dhidi ya Iran tangu alipoingia madarakani mwaka 2016 ambapo utawala wake unataka kuanzisha upya mazungumzo ya mkataba wa nyuklia na kupanua mapendekezo yake ili ikabiliane na mpango wa makombora ya masafa marefu ya Iran ya kudhibiti shughuli za kijeshi katika eneo zima la Mashariki ya Kati. **BBC**



Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa ambaye pia ni kiongozi wa Chama tawala cha African National Congress (ANC), akipiga kura kwenye uchaguzi uliofanyika jana. **PICHA: REUTERS**

# ANC yapewa nafasi kubwa ya kushinda uchaguzi

**JOHANNESBURG,** Afrika Kusini

WANANCHI wa Afrika Kusini jana walipiga kura kuwachagua wabunge, maseneta, wakuu wa mikoa, ambapo chama cha ANC kinaongozwa na Rais Cyril Ramaphosa.

Wananchi hao wanashiriki katika uchaguzi ambao unafanyika tena miaka 25 tangu kumalizika kwa enzi ya ubaguzi na huenda ukawa na changamoto kubwa kwa chama cha Rais wa zamani, Nelson Mandela, African National congress (ANC) ambacho kinaendelea kusalia madarakani.

Chama cha ANC kinatarajiwa kupata viti vingi bungeni, na kumteua Rais Cyril Ramaphosa kuendelea kushikilia uongozi wa nchi hiyo.

Hata hivyo, chama hiki kongwe cha ukombozi barani Afrika kinaendelea kupoteza umaarufu wake.

Tangu alipochukua hatamu ya uongozi wa chama cha ANC mwaka mmoja uliopita, Rais Ramaphosa amekuwa akisema kuwa yeye ni mtu wa mabadiliko, atafufua uchumi.

Rais Ramaphosa anakabiliwa na upinzani mkali kutoka kwa washirika wa Jacob Zuma ndani ya ANC - na wapiga kura wamechoshwa na kashfa za ufisadi, kukua pole pole kwa uchumi, ukosefu wa kazi ambao sasa umefikia asilimia 27 na visa vya mara kwa mara vya kupotea kwa nguvu za umeme.

Gazeti la kimataifa la Forbes, lilimnukuu Rais Ramaphosa kuwa aliachana na shughuli za biashara ili kuepuka migogoro ya riba baada ya kuwa Naibu wa Rais wa Afrika Kusini mwaka 2014.

Chama tawala nchini humo, Africa National Congress (ANC) ndicho kilipambana dhidi ya utawala wa kibaguzi chini ya uongozi wa Nelson Madela. Kutokana na hilo, kinaungwa mkono kwa kiasi kikubwa na watu weusi. Chama Kikuu cha upinzani, Democratic Alliance (DA) kinaungwa mkono kwa kiasi kikubwa na wazungu ambao ni raia wa nchi hiyo.

Hata hivyo, Maimane, ambaye ni mtu mweusi wakosoaji wake wanamwita Kibaraka wa Wazungu. Naye Julius Malema, kiongozi wa chama cha pili kwa ukubwa cha upinzani Afrika kusini mwenye umri wa miaka 38, anatazamwa kama mwanasiasa mwenye ushawishi mkubwa nchini humo.

Malema, au "Juju" kama anavyoitwa wakati mwingine amekiweka EFF katika nafasi ya kuwa mrithi wa ajenda kali ya ANC na amefichua madhaifu ya chama hicho tawala.

Chama cha EFF kilijinyakulia asilimia sita ya kura zilizopigwa mnamo 2014 katika awamu ya kwanza ya uchaguzi mkuu, lakini ushawishi wake unaonekana kuzidi nguvu takwimu hizo. **RFI**

# Wanasiasa marufuku kuingilia kazi kitabibu

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amewataka viongozi wa serikali kuacha mara moja kuingilia majukumu ya wataalamu wa afya, akieleza kuwa vitendo hivyo vina athari kubwa kwa wananchi wanaohitaji huduma hizo.

Mwalimu alitoa rai hiyo jana bungeni jijini Dodoma alipohitimisha mjadala wa makadirio ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Aliagiza kuwa daktari akifanya makosa, afikishwe mbele ya Chama cha Madaktari ili achukuliwe hatua ikiwa ni pamoja na kufutiwa usajili.

Alisema hatua kama hiyo ichukuliwe dhidi ya mkunga anayeonekana kukiuka maadili ya kazi yake.

Alisema vitendo vya baadhi ya viongozi wa serikali kuchukua hatua dhidi ya wataalamu wa afya wanaoona wamekiuka maadili ya kazi zao, vimekuwa vikiwadhalilisha wataalamu hao na kuathiri utoaji wa huduma za afya nchini.

"Mbaya zaidi, mambo haya yanakuwa na madhara makubwa kwa wananchi wa kawaida ambao hawana uwezo wa kulipia gharama za matibabu kwenye hospitali binafsi," Mwalimu alisema huku akiibua shangwe bungeni.

Machi 2017, Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Christopher Ngubiagai, alitangazwa na Jumuiya ya Madaktari Tanzania kuwa adui wa afya baada ya kumweka ndani Mganga Mkuu wilaya hiyo, Dk. Vitalis Katalyeba kwa tuhuma za kuchelewesha gari la wagonjwa na kusababisha kifo cha mgonjwa.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Rehema Nchimbi, pia aliagiza kuwekwa ndani kwa Mganga Mkuu wa Wilaya ya Singida Mjini, Dk. Erivk Bakuza, kutokana na upungufu wa kiutendaji.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo, pia alimtaka Mganga Mkuu wa Wilaya ya Monduli kutoa maelezo ya malimbikizo mbalimbali ya stahiki za watumishi ilhali si jukumu la mganga huyo.

Septemba mwaka jana, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, alimsimamisha kazi Mganga Mkuu wa Mkoa wa Kituo cha Afya Ukami, Dk. Andrew Kitwanga, kwa madai ya wananchi kudhalilishwa na mganga huyo.

Aprili mwaka huu, alimsimamisha kazi Daktari wa Kituo cha Afya Ngarenaro mkoani Arusha, Dk. Japhet Kivuyo, baada ya kamati ya kisiasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutomkuta ofisini.




Mkurugenzi wa Fedha za Uwakala wa Benki ya Maendeleo TIB, Lilian Mbassy (wapili kulia), akitiliana saini randama ya makubaliano na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Consumer's Choice, Frida Mlingi (wapili kushoto), juu ya mradi wa kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala nasafi ya bioethanol ya kupikia majumbani kwa kaya zaidi ya milioni moja jijini Dar es salaam wenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1.2. Mradi huo umefadhiliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linashughulikia Maendeleo ya Viwanda (UNIDO). **NA MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wapigiwa debe uchaguzi mitaa

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama, Annamringi Macha, amesema wanawake wamekuwa wakiongoza kujitokeza kwa wingi katika upigaji kura tofauti na wanaume, huku akisisitiza pia wajitokeze kuwania nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari alipokuwa akitoa taarifa juu ya ujio wa Mwenge wa Uhuru mkoani Shinyanga utakaopokelewa katika kijiji cha Namba tisa kata ya Bulyanhulu Halmashauri ya Msalala, Macha alisema wanawake wamekuwa wakiongoza kujitokeza katika zoezi la upigaji kura tofauti na wanaume huku akisisitiza pia wajitokeze kuwania nafasi kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka huu ni mitaa kushauri jamii wasiangalie jinsia bali waangalie uwezo wao wa kuwatumikia wananchi.

"Ujumbe wa Mwenge wa Uhuru kwa mwaka huu ni wananchi kushiriki katika uchaguzi wa serikali za mitaa... ningependa wakati ukifika wajitokeze kwa wingi ila nawasifu wanawake wamekuwa wakijitokeza kwa wingi kila chaguzi zinapowadia ukilinganisha na wanaume, sijui kwanini huwa hawashindi sababu wao ni wengi," alisema Macha.

Alisema kuwa Mwenge wa Uhuru utatokea mkoani Geita na kuingia Kata ya Bulyanhulu Halmashauri ya Msalala ikiwa kwa wilaya ya Kahama itazindua, kuona na kuweka jiwe la msingi, jumla ya miradi 23 yenye thamani ya Sh. bilioni 31.6.

Aidha, alisema kuwa Halmashauri ya Msalala ina miradi sita yenye thamani ya Sh. bilioni 2.09, Ushetu miradi saba yenye thamani ya Sh. milioni 304 na Kahama Mji miradi kumi yenye thamani ya Sh. bilioni 29 ambapo miradi yote kwa ujumla itahusiana na kilimo, afya na mazingira ikiwamo utawala bora.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, alisema wanawake wanatakiwa kujitokeza kuwania nafasi za uongozi wasiwaachie wanaume na kubaki kuwa wapigakura katika uchaguzi wa serikali za mitaa, huku akisisitiza uchaguzi kuwa wa haki na kila eneo kuwa salama tofauti na wanavyofikiria.

## Mkataba huduma za wateja TCRA

INATOKA UK. 5

"Tutawakamata kiurahisi, mkataba wa huduma kwa mteja wa TCRA ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, ambayo imekuwa ikisisitiza usalama kwenye njia za mawasiliano,"alisema.

Naye, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora), George Mkuchika, aliagiza taasisi za umma kuwa na mikataba ya huduma inayoendana na wakati na utekelezaji wake uwe kwa mujibu wa viwango vilivyotolewa na wadau.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, alisema kuwa mkataba huo utaongeza uwazi na uwajibikaji kwenye utumishi wa umma na wateja watatambua haki zao na wajibu wa TCRA.

Alisema TCRA watoe elimu kwa Watanzania ili wafahamu mkataba huo wa huduma kwa mteja kwa kuwa kuzinduliwa kwake kutakuza sekta ya mawasiliano na kuifanya kuwa bora zaidi.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Mhandisi James Kilaba, alisema mkataba huo utadhibiti vitendo vya rushwa kwenye sekta ya mawasiliano nchini na kutatua malalamiko ya watumiaji wa huduma za mawasiliano ikiwemo rushwa.

Alisema mkataba huo wa huduma kwa mteja una lengo la kuwezesha TCRA kutekeleza majukumu yake kwa uwazi ili kutimiza dhana ya uwajibikaji.

Alieleza madhumuni ni kubainisha viwango vya utoaji huduma kwa wateja na kuuarifu umma kuhusu TCRA, huduma zinazotolewa pamoja na viwango vyake.

## Wabunge walia

INATOKA UK. 5

ya uchaguzi ambayo inahimiza kwamba kila kijiji kiwe na zahanati. Kwa hiyo, zahanati hizi, lazima ziwe na waganga pamoja na manesi wa kutosha," alisema.

Mbunge wa Muleba Kusini, Ana Tibaijuka (CCM), alimpongeza Waziri Ummy Mwalimu kwa kazi nzuri anayoifanya katika wizara yake, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vituo vya afya na zahanati.

"Sina budi kusema kwamba hospitali siyo majengo ila ni huduma na katika hili waziri pia aangalie hali halisi ya hospitali za rufaa.

"Napongeza juhudi za serikali ya awamu ya nne iliyokamilisha hospitali ya Mloganzila, lakini hospitali hiyo ni hospitali majengo kwani hakuna majengo 'town' (mjini) pale kwa ajili ya madaktari kukaa karibu na hospitali.

"Na hata huyu Prof. Mabele ambaye amefia Mloganzila, nilikwenda kumwangalia tu juzi nikakuta kwamba kama kuna dharura, daktari anafikaje Mloganzila? Kwa hiyo, naona kuna haja ya kufanya uwekezaji kuhakikisha kwamba kituo kinafanya kazi," alisema.

Mbunge wa Urambo, Magreth Sitta (CCM), alisema ipo haja serikali kuongeza watumishi wa sekta ya afya ili kukabiliana na uhaba watumishi katika kada hiyo.

Sitta pia aliiomba serikali kuboresha huduma za upasuaji na matibabu ya dharura katika Hospitali ya Wilaya ya Urambo mkoani Tabora.

Mbunge wa Mpanda Vijijini, Moshi Kakoso (CCM), pia aliitaka serikali kuongeza madaktari kwenye vituo vya afya na hospitali, akieleza kuwa Wilaya ya Tangayika ina daktai mmoja tu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI NA VIPURI

**BASI LINAKODISHWA,** Basi aina Toyota HIACE dungu liko Dar linakodishwa kwenda mahali popote. Piga simu: 0784 316570 au 0754 316570 au 0715 316570 au 0629 316570.
Baruapepe: ceo@kses.co.tz.


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**JAUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya MWANZO DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa mirathi NA. 31/2019**

**Ombi la MTEMI RAMADHANI kuteuliwa**

Msimamiliz wa mirathi ya marehemu **FATUMA GWAO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanatakiwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano 23/5/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyoupo mahakamani waweza kukaguliwa Tarehe 07/05/2019.

Tarehe ...7/5/...20 19...........

PRINCIPAL..........
PRIMARY COURT MAGISTRATE
URBAN DODOMA
Sahihi ya Hakimu

115218902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 08/05/2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya ALHAMISI tarehe 09/05/2019 kampuni ya **TARIMO REMI STANSLAUS** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka ARUSHA kuelekea LONGIDO na kutoka LONGIDO kuelekea ARUSHA gari hilo lenye namba za usajili: **T155BJM/ T916DCG.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
Urefu-mita 17.50
Upana –mita 3.28
Kimo – mita 4.60

3. Njia itakayotumika ARUSHA hadi **LONGIDO kupitia OLDONYOSAMBU** na kurudi ARUSHA kupitia **OLDONYOSAMBU** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215217802

**KUPOTELEWA NA KADI YA GARI**

**JOEL ROMEL MOSHI,**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 723 BZL** aina ya **SUZUKI CARRY** yenye chassis namba **DC51T234262** na Injini namba **F6AEAA4262**

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .

Polisi Taafifa :
**MOS/TR/RB/2983/2016**

215218101

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:63..2012**
**Mdai: NAVONE A.KAZOKA**

**DHIDI YA**
**Mdaiwa: NICOLAUS DOMINIC MPIGO**
**Kwa:**
**NICOLAUS DOMINIC MPIGO**

Ombi la Mdai:
NAVONE A.KAZOKA
Madai ya: **MGAWANYO WA MALI NA MATUNZO YA WATOTO 3 NA SH.100,000/= KWA MWEZI**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 30 mwezi 05 mwaka 2019 saa 08:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 08 mwezi 05 mwaka 2019.

215218402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KTK MAHAKAMA YA MWANZO MJINI**
**ILIYOPO MOROGORO**
**TANGAZO LA KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA MADAI NAMBA:238..2018**
**Mdai: RAJABU ALLY**
**DHIDI YA**
**Mdaiwa: HALIFA ISIHAKA**
**Kwa:**
**HALIFA ISIHAKA**

**Ombi la Mdai:**
**RAJABU ALLY**

**Madai ya: PESA SH. 2,200,000/=**

Unatakiwa kuudhuria hapa mahakamani ktk shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 30 mwezi 05 mwaka 2019 saa 08:30 Asubuhi.

Angalia kama hukuudhuria/hamkuudhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mme-pokea kuitwa shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 08 mwezi 05 mwaka 2019.

215218502


JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# POGBA BADO PASUA KICHWA



**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid, inaamini kuwa ina nafasi kubwa ya kumnasa kiungo wa Manchester United, Paul Pogba, lakini dau lililowekwa na klabu yake kumuuza nyota huyo linawapa wasiwasi kumpata.

Maisha ya Pogba ndani ya Manchester United yanaonekana kuelekea ukingoni kutokana na kile kinachotajwa tabia zake zilizokithiri za utovu wa nidhamu na inasemekana kuwa klabu hiyo ipo tayari kupokea ofa kutoka klabu nyingine ili imuachie kiungo huyo wa Ufaransa.

Real Madrid inaonekana ndio timu yenye nafasi kubwa kutokana na mahaba ambayo kocha wake Zinedine Zidane anayo kwa nyota huyo ambaye ni mshindi wa medali ya dhahabu aliyoipata baada ya Ufaransa kutwaa Kombe la Dunia mwaka jana.

Lakini pamoja na Real Madrid kutaka kutumia ushawishi wa Zidane ili kumnasa kiungo huyo wakati wa usajili wa majira ya kiangazi, timu hiyo ya Hispania inadaiwa kuwa haiko tayari kutoa kitita cha Pauni milioni 150 ambazo Manchester United inahitaji ili kumuachia kiungo huyo.

# *Liverpool haielewi ilivyoichapa Barcelona*

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp amesema alikuwa kwenye hali ya ajabu baada ya wachezaji wake kushinda dhidi ya Barcelona mabao 4-0 kwenye mchezo wao wa pili wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya uliochezwa Uwanja wa Anfield na kujikuta akitokwa na machozi.

Liverpool inatinga hatua ya fainali kwa jumla ya ushindi wa mabao 4-3 baada ya mchezo wa kwanza kupoteza wakiwa ugenini kwa kufungwa mabao 3-0 na wao wakashinda 4-0, mabao yaliyofungwa na Georginio Wijnaldum na Divock Origi.

Sasa wanasubiri kucheza fainali na mshindi wa mchezo kati ya Ajax ama Tottenham.


"Kama ingekuwa ni kuichanganua timu yangu kwa matokeo iliyopata, moyo wangu ulikuwa unanisumbua kama mjinga fulani hivi ningeshindwa kutoa tathmini, dunia nzima ingejua kwamba mimi ni mjinga.

"Nina furaha kupita kiasi kupenya hatua hii ngumu na yenye ushindani kwangu, mchezo wote mwanzo mwisho ulikuwa ni mgumu usioelezeka, kuna vitu vingi duniani vya muhimu, niliwaambia wachezaji kushinda ni jambo rahisi ila ugumu upo kuzuia kufungwa hapo ndipo hofu ilipojificha, ukichanganya na kutoamini pamoja na furaha unapata vitu vya ajabu ambavyo sijawahi kuvipata.

"Awali niliwaambia wachezaji itakuwa ngumu kwangu kupata matokeo, lakini kwa kuwa nafikiria juu yenu nina amini tunaweza kupata matokeo ila mwisho wa siku tumeshinda siamini kama tumeshinda," alisema Klopp.



# Guardiola: Nilimzuia Kompany kupiga shuti



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema kuwa alimzuia nahodha wa kikosi hicho, Vincent Kompany kupiga shuti ambalo lilileta bao la ushindi mbele ya Leicester City.

Ushindi huo umeirejesha City kileleni baada ya kufikisha jumla ya pointi 95 na kuishusha Liverpool yenye pointi 94 ikiwa nafasi ya pili, kama watashinda mbele ya Brighton Jumapili basi watatetea Kombe lao la Ligi Kuu England msimu huu.

"Nilimwambia Kompany, hapana usipige shuti, usipige shuti ukiwa nje ya 18," alisema Guardiola.

Kompany alipuuzia sauti ya bosi wake huyo na kuachia shuti akiwa nje ya 18 ambalo lilizama nyavuni, na hili ni bao lake la kwanza akiwa nje ya 18 baada ya kupita miaka 11.

"Nilisikia sauti ikinizuia kupiga shuti, usipige shuti, usipige shuti ndivyo nilivyoskia ila nikaiambia nafsi yangu, sikuwa na namna zaidi ya kufanya kile ambacho nilikifanya wakati nikiwa bado kijana sana," alisema.

## HABARI MICHEZO




# MESSI, RONALDO KUKOSEKANA FAINALI UEFA MARA YA KWANZA

**MADRID,** Hispania

KWA mara ya kwanza tangu mwaka 2013, si Lionel Messi au Cristiano Ronaldo atakayecheza kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu hu.

Messi na Barcelona walitolewa juzi usiku kwenye nusu fainali ya pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kichapo cha 4-0, baada ya mchezo wa kwanza kupata ushindi wa 3-0.

Matokeo hayo ya kushitukiza yamemaliza msimu ambao sasa wawili hao wanakosekana kwenye michuano hiyo mikubwa zaidi kwa ngazi ya klabu.

Tangu mwaka 2013, mmoja kati ya Messi au Ronaldo walihusika kwenye fainali tano, huku Madrid ikishinda mara tatu mfululizo.

Lakini Ronaldo, ambaye aliondoka Real Madrid mwanzoni mwa msimu huu na kutimkia Juventus, timu yake hiyo ilitolewa kwenye robo fainali na Ajax.

Na Messi ameshindwa kushinda taji hilo tangu mwaka 2015 baada ya kukubali kichapo cha Jumanne usiku.

Messi na Ronaldo pia wamekuwa wachezaji wawili ambao wameshinda tuzo ya Ballon kwa kipindi cha miaka 10 na kila mmoja alitwaa mara tano ambapo mwaka jana Luka Modric aliitwa tuzo hiyo.

Liverpool itakutana na kati ya Ajax au Tottenham kwenye fainali ya mwaka huu mjini Madrid.

## Mourinho asifu morali Liverpool



**LIVERPOOL,** England

JOSE Mourinho anaamini kwamba, Liverpool walikuwa na kumbukumbu nzuri kwa kuweza kupindua matokeo dhidi ya Barcelona na kukiona kikosi hicho cha Jurgen Klopp kinaweza kufanya kweli msimu huu.

Msimu uliopita Liverpool ilifuzu kwa fainali ya michuano hiyo na ikafungwa kwenye fainali na Real Madrid.

Mabao mawili kutoka kwa Divock Origi na Georginio Wijnaldum yaliwawezesha Liverpool kupata ushindi wa 4-0 juzi usiku.

Kocha wa zamani wa Manchester United, Mourinho alimsifu Klopp mara baada ya mchezo huo akiiambia beIN SPORTS.

"Naweza kusema kwamba huku kutokea nyuma kuna jina moja, Jurgen.

"Nafikiri ilikuwa mbinu nzuri na falsafa ya kuwezesha kushinda mchezo kiurahisi."

## Van Dijk: Liver inaweza kuifunga timu yoyote

**LONDON,** England

VIRGIL van Dijk amesisiitiza kwamba alikuwa akiamini Liverpool ambayo imetiga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya inaweza kuifunga timu yoyote.

Van Dijk aliwasaidia vijana hao wa Jurgen Klopp kufuzu kwa mara ya pili mfululizo fainali ya michuano hiyo baada ya kuifunga Barcelona Jumanne.

Divock Origi na Georginio Wijnaldum kila moja alifunga mabao mawili kwenye ushindi wa 4-0 katika dimba la Anfield, na kuwafanya wafuzu kwa uwiano wa mabao 4-3.

Na sasa watacheza ama na Tottenham au Ajax katika fainali itakayopigwa mjini Madrid Juni Mosi, mwaka huu, lakini Van Dijk hana hofu na mshindani yoyote atakayekutana na Liverpool.

"Tunahisi kama tunaweza kumfunga yeyote wakati wowote tukiingia uwanjani," alisema beki huyo wa kati.

"Hatutaenda uwanjani kufikiri kwamba hatuwezi kumfunga yeyote. "Utakuwa mchezo mgumu na tutaona jinsi itakavyokuwa huko jijni Madrid na tumejiandaa kwa lolote."



## DOND A SOKA
## MAGA A ULAYA




# KLOPP: MUUJIZA WA ANFIELD

●●● Katika maisha yangu nimetazama mechi nyingi za soka, lakini sikumbuki nyingi kama hii...

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesisitiza hawezi kukumbuka siku aliyotazama mechi kama hii ya ushindi wa kishindo wa mabao 4-0 dhidi ya Barcelona na kutinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kufungwa mabao 3-0 kutoka mechi ya mkondo wa kwanza, Liverpool ilifanya kitu kisichotarajiwa kufuatia mabao mawili kupitia kwa Divock Origi na idadi kama hiyo yalíyotupiwa na Georginio Wijnaldum na kufanya kusonga mbele kwa jumla ya tofauti ya mabao 4-3 katika Uwanja wa Anfield juzi, hivyo kuwa timu ya tatu katika historia ya michuano hiyo kuweza kupindua matokeo ya mabao matatu kwenye hatua ya nusu fainali.

**Klopp karibia apoteze maneno ya kuzungumza wakati akijaribu kuelezea hisia zake baada ya mechi, akikiri pengine tunaweza tusione tena mchezo kama huo.**

Aliiambia BT Sport "mchezo mzima, kiwango kwa ujumla kilikuwa kikubwa mno. Ilikuwa kubwa sana. Katika maisha yangu nimetazama mechi nyingi za soka, lakini sikumbuki nyingi kama hii.

"Kushinda tayari ni vigumu lakini kushinda bila kuruhusu bao ['clean sheet'] Sijui ni kwa namna gani wavulana wamelifanya hili. Nilimuona James Milner akilia baada ya mechi uwanjani, inamaana sana kwa sisi sote.

"Kuna mambo mengi zaidi muhimu duniani, lakini kutengeneza aina hii ya mashabiki ni ya kipekee.

"Ni saa 4 na dakika 10, watoto wako walio wengi huenda wamelala, lakini wavulana hawa wenye vipaji. Ni jambo lisilowezekana. Nzuri kwangu kama unataka, mimi si asili hivyo sina maneno mazuri kwa hilo. "

Klopp kisha alisema katika mkutano na wanahabari baada ya mechi kwamba aliwaambia wachezaji wake "hakuamini" wangeweza kupindua matokeo, lakini tabia ya timu yake hatimaye ilimpa matumaini.

Katika mechi ya fainali, Liverpool sasa itaivaa Tottenham ama Ajax, mojawapo ambayo ilipata matokeo mazuri ya jumla jana usiku, na Klopp anasema kikosi chake kinatazama uwezekano wa kufuta kumbukumbu ya fainali ya msimu uliopita iliyokutana na Real Madrid jijini Kiev, Ukraine.

**MOURINHO AUMBUKA**

Baada ya kueleza hawezi kubeti "hata shilingi" kwa Liverpool kutinga fainali, Jose Mourinho aliuelezea ushindi wa Liverpool kwa "mawazo ya Jurgen".

Kabla ya mechi, Mourinho alisema kupitia beIN Sport: "Siwezi kubashiri katika soka, sipendi kubashiri lakini siwezi kubeti hata shilingi moja kwa Liverpool kucheza fainali.

"Anfield inaweza kufanya miujiza. Lakini hili linaweza kuwa zaidi ya hilo. 3-0 inaweza kuwa zaidi ya hayo."

Lakini baada ya mechi akasema: "Nadhani hii si kuhusu mbinu, si kuhusu falsafa. Hii ni juu ya moyo na nafsi. Na uelewa wa ajabu ambao aliutengeneza na kundi hilo la wachezaji.

"Nadhani Jurgen ni mhusika mkubwa kwa mafanikio haya, kwa utu wake wa ajabu, kwa mawazo yake ya ajabu. Timu ilikuwa pale na timu iliamini. "

## ZISIKUPITE

### MBAPPE KUVUNJIWA BENKI

REAL Madrid inajiandaa kuweka rekodi kwa kutoa ofa ya pauni milioni 240 kwa Paris St-Germain ili kuipata saini ya Kylian Mbappe. ***(France Football, via Sport)***

### SANCHO BASI TENA UNITED

UWEZEKANO wa Manchester United kumfuata winga wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, 19, ikiwa na pauni milioni 100 mkononi ili kumrejesha EPL, umetoweka baada ya miamba hiyo ya Old Trafford kushindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mail)***

### EDU KUULA TENA ARSENAL

ARSENAL itamteua mchezaji wao Edu kuwa mkurugenzi mpya wa michezo majira haya ya joto. ***(Mail)***

### HAZARD KUOMBA KUSEPA

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Eden Hazard, 28, anapanga kutoa ombi la kuondoka ili kulazimisha kujiunga na Real Madrid. ***(AS - in Spanish)***

### KLOPP AMUWINDA ASENSIO

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp atajaribu kumsajili kiungo Mhispania Marco Asensio, kutoka Real Madrid. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### KOMPANY ATEGWA MWAKA

MANCHESTER City inatumai beki wa kati raia wa Ubelgiji, Vincent Kompany, 33, atabaki katika klabu hiyo kwa kukubali kuongeza mkataba wa mwaka mmoja. ***(Times)***

### YAMFUATILIA HUDSON-ODOI

MAJERA ya goti yanayomkabili winga wa Chelsea, Callum Hudson-Odoi, 18, yanapona kwa kasi na miamba ya Ujerumani, Bayern Munich imekuwa ikifuatilia maendeleo ya nyota huyo wa kimataifa wa England. ***(Sun)***

### UNITED KUMRUDIA MAGUIRE

MANCHESTER United itarejea tena mchakato wake wa kumsajili beki wa Leicester City na England, Harry Maguire, 26, majira haya ya joto. ***(ESPN)***

### LOPETEGUI KUMRITHI KOVAC?

KOCHA wa Ajax, Erik ten Hag na yule wa zamani wa Real Madrid, Julen Lopetegui, wanawaniwa kurithi mikoba ya Niko Kovac Bayern Munich. ***(Marca)***

### DE LIGT BEI JUU SOKONI

BARCELONA bado ina kazi ya kufanya kama inataka kukamilisha dili la kumsajili beki wa kati wa Ajax, Matthijs de Ligt, 19, baada ya wakala wake kuongeza dau kwa Mholanzi huyo. ***(ESPN)***

### CONTE AUKANA MPANGO ROMA

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte ameikana Roma kama klabu mpya ijayo kwake atakayotua kufanya kazi. ***(La Gazzetta dello Sport - in Italian)***

### AWAKATAA LLORENTE, CEBALLOS

MSHAMBULIAJI wa Wales, Gareth Bale, 29, na viungo wa Wahispania Marcos Llorente, 24, na Dani Ceballos, 22, wameambiwa mustakabali wao wa baadaye haupo tena Real Madrid na kocha wa klabu hiyo, Zinedine Zidane. ***(Marca - in Spanish)***

HABARI MICHEZO

# Vijana 60 kufundishwa uzalishaji vipindi vya TV

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya vijana 60 kutoka kila pembe barani Afrika – ikiwamo Tanzania watapata fursa ya udhamini wa kujifunza uzalishaji wa filamu na vipindi vya televisheni kwa mwaka mzima katika awamu ya pili ya program ya MultiChoice Talent Factory.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso, kuanzia Mei 7 hadi Juni 14, mwaka huu, vijana wenye uchu wa kuwa wabobezi wa filamu watapata fursa ya kujiandikisha kwa ajili ya usaili utakaotoa wanafunzi 60 ambao watadhaminiwa kwa mafunzo hayo ya kitaalamu ya mwaka mzima yanayoendeshwa katika vituo vitatu barani Afrika vilivyopo Nairobi, Lusaka na Lagos.

Woiso alisema kwa upande wa Tanzania, kuna nafasi nne za udhamini katika awamu hii ya pili ambapo wanafunzi hao wataungana na wenzao kutoka Kenya, Uganda na Ethiopia katika Kituo cha mafunzo cha Nairobi.

Alisema vituo hivyo vya mafunzo vinaongozwa na wakufunzi mahiri wenye ujuzi mkubwa na pia vina vifaa na miundombinu ya kisasa kuwawezesha wanafunzi kujifunza uzalishaji filamu wa kisasa na wa kibiashara.

Aidha, kama sehemu ya programu, alifafanua kuwa watengenezaji wa filamu wadogo watapatiwa mafunzo na uzoefu wa vitendo katika tasnia ya filamu, kwa kuzingatia simulizi za visa, uzalishaji, sauti na kuongoza na maeneo mengine muhimu. Vituo hivi pia vinatoa fursa kwa wanafunzi ya kujifunza moja kwa moja kutoka kwa wataalamu wa sekta hiyo, kufanya kazi za kuzalisha vipindi vya televisheni, maigizo na kuanda maudhui asilia ambayo yatakuwa yakirushwa hewani kwa njia mbalimbali ndani ya M-Net kwa kupitia (DStv).

"Darasa la kwanza la programu hii ambalo litakamilika Oktoba mwaka huu, tayari limeonyesha mafanikio makubwa ambapo wanafunzi wameshiriki katika kazi mbalimbali ikiwamo utengenezaji wa vipindi halisia vya muziki kama Coke Studio, Pambio, Turn-Up na telenovela ya kiswahili maarufu kama Selina"Nawasihi vijana wetu wa Tanzania wenye ari na nia ya kuwa nyota wa uzalishaji wa filamu duniani kuhakikisha kuwa hawakosi nafasi hii. Wajiandikishe ili waweze kupata fursa hiii muhimu. Kwa wanaotaka kushiriki ni rahisi sana. tembelea www.multichoicetalentfactory.com kabla ya Juni 14, mwaka huu na kisha fuata maelekezo ya namna ya kujisajili. Kwa watakaopata tatizo lolote wanaweza kutuma e-mail info@multichoicetalentfactory.com ," alisema Woiso.

# KAGERA SUGAR WAISOMA SIMBA

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Kagera Sugar kutoka Bukoba, mkoani Kagera kiko jijini Dar es Salaam tangu Jumatatu na lengo la kuwasili mapema ni "kuwasoma" wapinzani wao Simba, imeelezwa.

**Simba itawakaribisha Kagera Sugar katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho Ijumaa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.**

Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Maxime, aliliambia gazeti hili kuwa lengo la kuja jijini mapema ni kupata nafasi ya kupumzika na kujipanga upya kuwakabili mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu.

Maxime alisema anafahamu mechi ya kesho itakuwa ngumu zaidi kwa sababu Simba haitakubali kupoteza mchezo huo wa marudiano ili waendelee kujiweka katika nafasi nzuri ya mbio za kutwaa ubingwa.

"Tunajua mchezo utakuwa mgumu kuliko ule tuliocheza Bukoba, ndio maana nilipendekeza tuje mapema Dar es Salaam kwa ajili ya kurekebisha makosa yetu madogo madogo tuliyonayo, kila upande utaingia uwanjani kwa lengo la kusaka ushindi na si kitu kingine, sisi bado tunahitaji kujinusuru wakati wenzetu wanataka ubingwa, soka litapigwa," alisema Maxime.

Beki huyo wa zamani wa Taifa Stars na Mtibwa Sugar alisema pia endapo Simba itakosa utulivu, kwake itakuwa faida na amewaandaa wachezaji wake kuongeza umakini kila wanapokuwa na mpira.

"Hali ya hewa ni nzuri, haisumbui wakati wa kufanya mazoezi, leo (jana) pia tutawaangalia tena katika mechi yao na Coastal Union, itatusaidia zaidi kujipanga kiufundi," Maxime alisema.

Kagera Sugar ilipata ushindi wa mabao 2-1 katika mchezo wao wa kiporo dhidi ya Simba uliochezwa Aprili 20, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.




Mshindi wa Jackpot Bonus, Isaya Millanzi (kushoto) mkazi wa Kiluvya, Dar es Salaam, akikabidhiwa hundi ya Sh. 3,328,906 na Mkurugenzi wa Utawala na uthibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 11 kati ya 13 wiki iliyopita. **PICHA: SPORTPESA**

# SportPesa sasa kugawa magari

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inazidi kuwafurahisha wateja wake, Kampuni ya Michezo ya Kubashiri ya SportPesa Tanzania, imezindua promosheni mpya inayofahamika kama 'Usibahatishe Cheza na SportPesa'.

Promosheni hiyo itakuwa ya kushindania gari ndogo tatu aina ya IST, Simu janja za kisasa Smartphone 200, tiketi 45 za mechi ya Simba dhidi ya Sevilla FC inayoshiriki Ligi Kuu ya Hispania (La Liga) na tiketi 10 za mchezo wa Kariobangi Sharks na Everton ya England utakaochezwa nchini Kenya.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti wa SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, alisema wamezindua promosheni hiyo ambayo imeanza tangu Mei Mosi, mwaka huu na itadumu kwa wiki 15, lengo likiwa ni kampuni kuzidi kuwa karibu na wateja wake.

"Tumezindua promosheni mpya inayokwenda kwa jina la 'Usibahatishe Cheza na SportPesa', ambayo tutatoa magari matatu ya kisasa kabisa aina ya IST.

"Lakini tutatoa zawadi ya simu za kisasa pia Smartphone 200 ambazo zitaenda kwa wateja wetu watakaoshinda katika droo tutakazochezesha," alisema Tarimba na kuongeza.

"Pia tutatoa tiketi 45 za mechi ya Simba ambayo Mei 23, mwaka huu itacheza na miamba inayoshiriki La Liga, Sevilla kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam. Lakini tutatoa tiketi zingine 10 za kwenda kuangalia mechi ya timu ya Kariobangi Sharks watakaocheza na Everton ya England kule Kenya.

"Promosheni hii itachezeshwa kwa droo 15 kwa wiki 15 kwa kuwapata washindi. Hivyo kila siku ukibeti unashinda zawadi, sasa huu ni wakati wa Watanzania kuchangamkia fursa hiyo," alisema.

Tarimba alisema jana walianza kwa kutoa simu za Smartphone sita na tiketi 13 za mechi ya Simba dhidi ya Sevilla, baada ya washindi wa droo ya kwanza kupatikana.

"Tunajisikia faraja kurudisha fadhila kwa Watanzania, hasa wateja wetu, sasa huu ni wakati wao kucheza zaidi na SportPesa ili kujishindia zawadi zetu hizi mpya za gari, simu na tiketi za mechi hii kubwa ya Simba na Sevilla," alisema.

Sevilla inatarajia kuwasili nchini Mei 21, kisha kucheza na Simba Mei 23, mwaka huu, kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, kufuatia mwaliko SportPesa Tanzania.

Michezo
Alhamisi Mei 9, 2019
Nipashe



Klopp: Muujiza wa Anfield

HABARI UK.30

KWISHINE...



Mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi (kushoto), akidhibitiwa na kiungo wa Liverpool, Fabinho, wakati wa mechi ya nusu fainali ya pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyopigwa Uwanja wa Anfield juzi na Liver kushinda 4-0 hivyo kutinga fainali kwa tofauti ya mabao 4-3. **HABARI UK. 28**

# Yanga, Biashara vitisho vyatawala

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI kikosi cha Yanga kimetua salama Mara, wamewataka wenyeji wao Biashara United kujiandaa kisaikolojia kupoteza mchezo wao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaowakutanisha hapo kesho kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema kuwa wamefika salama na wanatarajia kufanya vizuri katika mchezo huo baada ya kurekebisha makosa yaliyotokea Iringa.

Saleh alisema wachezaji wametakiwa kusahau mashindano ya Kombe la FA na sasa akili yao ni kushinda mechi hiyo dhidi ya Biashara United na michezo mingine iliyobakia ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema wanajua bado taji la ligi hiyo ya juu inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika bado halina mwenyewe na wanaweza kulitwaa kama watashinda mechi zote zilizosalia na watani zao Simba kuboronga.

"Sisi tunaangalia mechi zetu tu, tunajipanga kushinda, hakuna mechi rahisi iliyobakia kwa timu zote, ligi yetu imekuwa ngumu na matokeo yamekuwa yanashangaza sana, hatujakata tamaa, tutazidi kupambana," alisema kiongozi huyo.

Alisema wachezaji wameahidi kumaliza mechi za Kanda ya Ziwa kwa ushindi na "kuwapoza" mashabiki baada ya kutolewa katika mashindano ya Kombe la FA na Lipuli FC ya Iringa.

Naye Kocha Mkuu wa Biashara United, Amri Said, aliliambia gazeti hili kuwa kikosi chake kimejipanga kucheza kwa 'jihadi' ili kuhakikisha hawapotezi mchezo huo na kurejesha matumaini ya kubakia kwenye Ligi Kuu.

Said alisema kuwa wamejiimarisha kila idara na wachezaji wake wanafahamu kwamba wakipoteza mechi hiyo watajiweka katika hali ya hatari kwa sababu nafasi waliyopo katika msimamo wa ligi ni mbaya.

# *Okwi, Kagere kumaliza mipira TFF*

## ●●● Waishusha Yanga kileleni kwa hat-trick kila mmoja, Bocco na Aussems wapewa tuzo ya...

**Na Adam Fungamwango**

MASTRAIKA Emmanuel Okwi na Meddie Kagere wa Simba, kila mmoja jana alifunga mabao matatu ['hat-trick'], wakati timu yao ikiisasambua bila huruma Coastal Union kutoka Tanga kwa mabao 8-1 kwenye mechi kali ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

**Hii ni 'hat-trick' ya pili kwa Okwi msimu huu ya kwanza akiifunga Oktoba 28 mwaka jana, mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, akifunga dakika ya nane, 53 na 77 dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.**

Na ni 'hat-trick' ya kwanza kwa Kagere tangu alipojiunga na Klabu ya Simba msimu huu akitokea Gor Mahia ya Kenya, hivyo kufanya wachezaji hao wawili hadi sasa kuondoka na mipira mitatu kutoka Shirikisho la Soka nchini, TFF.

Kwa matokeo hayo Simba sasa imeiengua Yanga iliyokuwa na pointi 80 kileleni kwa kufikisha pointi 81, pointi moja zaidi.

Simba ilianza pambano hilo kwa kasi, pamoja na changamoto ya uwanja kuwa na maji, kutokana na mvua kubwa kuendelea kunyesha jijini Dar es Salaam.

Dakika ya kwanza tu, Emmanuel Okwi alipiga shuti lililomgonga beki mmoja wa Coastal Union na kuwa kona ambayo haikuzaa matunda. Dakika ya tano baadaye, Okwi alipiga krosi, lakini Meddie Kagere akaukosa na mpira ukatoka nje.

Dakika ya 10, Okwi aliifungia Simba bao la kwanza akimalizia piga nikupige iliyotokea langoni mwa Coastal Union.

Coastal walizinduka dakika ya 14 baada ya Haji Ugando kuachia shuti kali akiwa nje ya eneo la hatari, lakini mpira huo uligonga mlangoni mwa goli na kurudi uwanjani. Okwi aliifungia Simba bao la pili dakika ya 19, alipoupata mpira katikati ya uwanja na kuukokota akampasia Kagere, aliyemrudishia tena mfungaji, kabla ya kumpiga chenga kipa Sudi Abdallah na kujaa wavuni.

Coastal ilipata bao la kufutia machozi dakika ya 34 kupitia kwa Raizin Hafidh kwa shuti kali lililompita Aishi Manula na kujaa wavuni. Mvua ya mabao kwa Coastal ilianza kunyesha kipindi cha pili, kwani dakika moja tu baada ya kuanza Okwi alikamilisha hat-trick yake, lakini baadaye alitoka na nafasi yake ikachukuliwa na Hassan Dilunga.

Utawala wa Kagere ukaanza kwani alifunga bao la nne dakika ya 69 akiunganisha kwa kichwa kona ya Cleotus Chama, kabla kupachika tena bao la tano dakika ya 74. Dilunga alifunga la sita dakika ya 80 baada ya kupokea krosi ya Mohamed Ibrahim, kabla ya Kagere kukamilisha hat-trick yake likiwa ni bao saba kwenye mechi hiyo na la 20 kwake msimu huu.

Chama aliyekuwa muda wote anatafuta bao kwa udi na uvumba, alifanikiwa kufunga bao la nane dakika ya 88.

Wakati huo huo, mshambuliaji wa Simba, John Bocco, ametangazwa Mchezaji Bora wa mwezi Aprili wa Ligi Kuu Tanzania Bara (TPL) msimu wa 2018/2019.

Bocco ametwaa tuzo hiyo baada ya kuwashinda wenzake wawili, Emmanuel Okwi wa Simba na Heritier Makambo wa Yanga walioingia fainali katika kinyang'anyiro cha tuzo hiyo inayotolewa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

Kwa mwezi huo wa Aprili, Simba ilicheza michezo sita na kushinda mitano na kupoteza mmoja, ambapo Bocco alitoa mchango mkubwa kwa timu yake akifunga mabao matatu na kuifanya Simba ipande hadi nafasi ya pili ikitoka ya tatu iliyokuwao mwezi uliopita.

Kwa upande wa Makambo yeye aliongoza Yanga iliyocheza michezo mitano ikishinda mitatu, sare moja na kupoteza moja, ambapo alifunga mabao matatu na alikuwa na mchango mkubwa katika mafanikio ya Yanga kuendelea kubaki nafasi ya kwanza mwezi huo, wakati Okwi aliyefunga pia mabao matatu alikuwa chachu ya mafanikio ya Simba.

Kadhalika, Kocha Mkuu wa Simba, Patrick Aussems ametangazwa kuwa Kocha Bora wa mwezi Aprili akiwashinda Kocha Mkuu wa Azam, Abdul Mingange na Kocha Mkuu wa Yanga, Mwinyi Zahera.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042